< ? Attested in older Swahili slang as *apecha alolo 'penniless, broke' (Ohly 1987a: 21). *Arosto is now more in fashion.

Nipo apeche alolo.

Nimeishiwa pesa.

> *arosto, chalala, mabaga, majalala, waka*

arosto, rosto n *ishiwa pesa, kosa pesa*
bankrupt, broke

< ? Attested in variations ranging from

*arosto/alosto to *rosto/losto. Probably derived from Sheng *lostia 'get lost' (Mbaabu & Nzuga 2003: 16).

Niko arosto.

Nimeishiwa pesa.

Niko rosto kweli.

Nimeishiwa hela kweli.

> *rosti*

asali wa moyo n.phr *mpenzi wa kike au wa kiume* girlfriend, boyfriend

Metaphorical extension of SS *asali 'honey' plus *moyo 'heart', which is also reflected in the transfer of *asali from class 9 to class 1. Popularised by Bongo Fleva song "Asali wa moyo" (Gangwe Mobb 2001).

Karibu chakula asali wangu wa moyo.

Karibu chakula mpenzi wangu.

> *laazizi*

baba askofu n.phr 1. *mfiraji* 2. *kind and generous man* 1. homosexual man 2. mtu mwenye roho nzuri ambaye yu tayari kutoa msaada

1. Metonymic hyperbolic extension of SS *baba askofu 'father bishop', referring to scandals about homosexual and pedophile catholic priests in the USA 2. Metonymic extension of SS *baba askofu 'father bishop', based on christian altruism

1. *Ah, wewe ni baba askofu tu.*

1. *Ah, wewe ni msenge tu.*

2. *Ah, yule ni baba askofu bwana.*

2. *Ah, yule ni mtu mzuri sana, anapenda kutoa msaada.*

> *basha*

baba wa taifa n.phr *noti ya shilingi 1000* note of 1000 TSh, issued in 2003

Metonymic extension of epitheton of President Nyerere *baba wa taifa 'Father of the Nation', based on his portrait printed on the note. Since late 2003.

Bei gani? - Baba wa taifa wawili.

Bei gani? - Noti mbili za elfu moja.

> *buku, tenga*

babaake, babake n.phr *jamaa yangu, rafiki*
my friend

Semantic extension of SS *babaake (contraction of *baba yake) 'his/her

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

father', motivation of use of 3. person possessive unclear, only in direct address (vocative); expression "his father".

Sema babaake! - Poa tu!

Vipi rafiki? - Nzuri tu!

> *babu lake, kachala, kichaa wangu, mshikaji, mwana, mwanangu*

babu kubwa, bab kubwa n.phr *safi kabisa, siyo kawaida* very nice, extraordinary
Metaphorical extension of SS *babu 'grandfather' plus SS *kubwa 'big, great, large'.

Katalogi ya chuo ni babu kubwa.

Tovuti ya chuo ni safi kabisa!

Jana tulikwenda kwenye arusi, ilikuwa babu kubwa.

Jana tulikwenda kwenye arusi, ilikuwa safi kabisa.

Tangazo (Fanta 2006): Maisha bab kubwa. Bamboocha.

Commercial (Fanta 2006): Maisha ni mazuri kabisa. Ya pekee.

babu lake, babu yake n.phr *jamaa yangu, rafiki (miito miongoni mwa vijana wenye urafiki wa karibu)* my friend (address among befriended youth)

Semantic extension of SS *babu 'grandfather', motivation of use of 3. person possessive unclear, only in direct address (vocative): "his grandfather".

Chwe[e] rega, babu lake, dongo limeyeyuka.

Hakuna, jamaa yangu, ugali umeisha.

Du, babu lake, bonge la dili nikugee.

Du, rafiki, nikueleze siri kubwa.

Du, acha, babu lake, bonge la bahati.

Du, acha, rafiki, bahati kubwa.

balungi n5/6 *titi kubwa* large female breast, tit
Dysphemistic extension of SS *balungi 'grapefruit, pomelo'. Rare.

Yule ana mabalungi makubwa.

Yule ana maziwa makubwa.

> *mtindi, tikitimaji, nido*

baluni n 1. *matako makubwa* 2. *maziwa makubwa* 3. *magari aina ya Toyota "Chaser" na "Mark II", yenye sehemu ya nyuma iliyo* 1. big behind 2. big breasts 3. car models Toyota "Chaser" and "Mark II" with rounded back
Metaphorical semantic extension of transfer

from SE 'balloon', motivated by its form. Ohly (1987a: 23) has *baluni both for 'pregnancy' and 'be pregnant' in older Swahili slang.

Mohamedi kanunua gari Toyota baluni.

Mohamedi kanunua gari Toyota "Chaser" with rounded back.

Akaenda katika baluni aliyokuja nayo.

Akaenda katika Toyota "Chaser" aliyokuja nayo.

> 1. *bambataa, haja kubwa, kibinda, mkundu, ndómbolo, taarabu, tukunyema, shuzi, wowowo* 3. *macho ya samaki, mayai*

bamba v *kuwa -zuri* be nice

Semantic extension of SS *bamba 'seize'.

Mademu wa Bongo wanabamba kinoma.

Wasichana wa Dar es Salaam ni wazuri sana.

bambataa n *matako makubwa* big buttocks
Double metonymic extension of the name of Afrika Bambaataa, a US-American HipHop-DJ > the name of a popular African Music Programme, aired daily on Clouds FM, Dar es Salaam.

Du, huyu demu ana bonge la bambataa!

Du, huyu msichana ana matako makubwa!

Huyu msichana ana matako ya bambataa.

Huyu msichana ana matako makubwa.

> *haja kubwa, kibinda, mkundu, ndómbolo, taarabu, tukunyema, shuzi, wowowo*

bana v 1. *kaa kwa kujificha* 2. *jificha* 3. *wekea mtu vikwazo* 1. sit and hide 2. hide 3. hinder sb

Dysphemistically motivated extension of SS *bana 'squeeze'.

1. *Oya, naenda kubana kijiweni.*

1. *Oya, naenda kukaa na kujificha kijiweni.*

> *egasha, kaza*

bandapanda n *viatu virefu vyenye soli nene* (HipHop)-boots with thick sole
Semantic extension of SS *banda 'shed, hut' plus *panda 'climb'? Now replaced by lakuchumpa.

> *buti, ndula, lakuchumpa, la kuparama*

bangaiza v.caus *bahatisha kupata cho chote; uza cho chote chenye maslahi; bahatika kwa kuhangaikahangaika* try one's luck in making some money; sell sth for profit < ?

Nimebangaiza buku teni.

- Nimebahatisha shilingi elfu kumi.
Bwana, sasa hivi unafanya shughuli gani? - Mshikaji, sina kazi nafanya kubangaiza tu.
 Bwana, sasa hivi unafanya shughuli gani? - Rafiki, sina kazi, nabahatisha kupata cho chote.
- bangaloo** n5/6 *nyumba kubwa na nzuri* big and nice house
 Transfer from SE 'bungalow'.
Lile bangaloo ni letu.
 Nyumba ile nzuri na kubwa ni yetu.
- bania** v *punja mtu kitu ambacho anastahili kupewa, nyima mtu kitu* reduce the share of somebody
 Semantic extension of SS *bania 'press to'.
Unanibania.
 Unanipunja, hutaki niendele.
 > *kiwingu, gozigozi*
- barida** adj *baridi, shwari* cool
 Derivation from SS *baridi 'cool, cold', by change of final vowel -i to -a. Not common
Hali vipi? - Barida tu mwana.
 Hali vipi? - Poa tu rafiki.
 > *baridi, poa, shwari*
- baridi** adj *safi* good
 Semantic extension of SS *baridi 'cool', hyperbolic calque of SE 'cool'. Proper reply to greetings such as *hali vipi?
 > *barida, poa, joto*
- basha** n5/6 *mfiraji* homosexual man
 Semantic extension of SS *basha 'king in a pack of playing cards'; also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 23). In KKS 1 and 2. Basha is derived from *pasha (Shepherd 1987: 250).
 > *baba askofu*
- bastola** n9 *nyonga kubwa* large hips
 Metaphorical extension of SS *bastola 'pistol', motivated by form of pistol worn in holster on hips in "cowboy-style".
Yule ana bastola.
 Yule ana nyonga kubwa.
 > *bunduki, pisto[l], silaha, mvinyo*
- bati** n9 *sarafu ya TSh 100* coin of 100 TSh
 Metonymic extension from SS *bati (class 5/6) 'white hard metal'. Coinage by Bongo-Fleva artist Ngwair in the track "mikasi", which became popular. Mostly used by the street vendors called "Wamachinga"
Sasa we una bati usiku huu unaenda wapi, wakati hiyo bati hata soda tu hupati. Ngwair (Mikasi)
 Sasa wewe una shilingi mia, usiku huu unaenda wapi, wakati kwa hizo shilingi mia hata soda tu hupati.
 > *alasisi, hais, jiti, nyeto, pini*
- baunsa** n5/6 1. *mtu mnene, aliyepanuka kifuani, mbabe* 2. *mlinzi mlangoni* 1. fat person, sb with broad chest 2. doorkeeper, bouncer
 Semantic extension of transfer from SE 'bouncer'. Also attested for Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 2).
 2. *Baunsa akatutia ndani ya klabu bure.*
 2. *Mlinzi wa klabu alitutia ndani ya klabu bure.*
 > *njemba njemba*
- bee** numeral *mbili* two
 < ? Popularised through song of Gangwe Mobb "Mtu bee chelea bina" (2001).
Hapa ni mtu bee tu.
 Hapa ni watu wawili tu.
Nipe chumvi ya chuma bee.
 Nipe chumvi ya shilingi mbili.
 > *dala, taraa*
- bebelebebele** n *fujo, patashika* commotion, chaos
 < ? Not common. New in 2005.
Mechi ya leo itakuwa bebelebebele.
 Mechi ya leo itakuwa patashika.
 > *songombingo*
- bei ya mchekea** n.phr *bei rahisi sana* ridiculously cheap
 Metonymic extension of SS *chekea 'laugh at', motivated by context
Hii suruali nimenunua kwa bei ya mchekea.
 Hii suruali nimenunua kwa bei rahisi sana.
Mwanamke wa mchekea.
 Mwanamke ambaye anakubali kirahisi sana.
 > *maharage ya Mbeya*
- beki tatu** n.phr *msichana wa kazi, mfanyakazi wa ndani* housegirl

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Metaphorical or metonymic extension of football player on position "back 3" (sweeper).

Beki tatu wa kina Juma ni magoli!

Msichana wa kazi wa kina Juma ni mzuri sana!

bendera n9 *division "F" katika matokeo ya mitihani* division "F" in school results
Metonymic extension of SS *bendera 'flag' based on form: the silhouette of a flag resembles the shape of an "F".

bene disc *nzuri* well, good

Transfer from Italian *bene 'well, fine, alright'. Used as a reply to greetings such as *mambo vipi? Not common.

Mambo vipi? - Bene!

Habari gani? - Nzuri!

bi mkubwa n.phr *mama* mother

Metonymic extension of SS *bi mkubwa 'big lady, old lady', not used as address
> *maza*

bibisii, BBC n9 1. *Kiingereza* 2. *mtu ambaye anazungumza sana, msema ovyo* 1. English language 2. sb who talks a lot, sb who can't keep a secret

Onomastic synecdoche of SE 'BBC' (British Broadcasting Corporation).

Jamaa yule, usimwambie siri, yule ni BBC.

Jamaa yule, usimwambie siri, atasema tu.

> *radio mbao, radio saba saba, ung'eng'e, tema ngeli, sleng, ingia external*

bifu n *ugomvi* quarrel, fight

Transfer from American slang 'beef' with the meaning 'quarrel, fight'.

Wameibua bifu.

Wameanza ugomvi.

> *kosovo*

bingo n5/6 1. *pesa (ya kubahatisha)* 2. *kijana au mwanamume anayetoa au kununua kitu kwa msichana kwa lengo la mapenzi; mwanaume anayeliwa pesa na mwanamke* 1. money (got by chance) 2. man having a short term relationship with a (unmarried) woman who aims at getting money out of him
Hyperbolic extension of SS *bingo 'game of hazard, game of chance', also a TV-show.

1. *Vipi una dili gani? - Nacheza bingo.*

1. What business do you have? - I just try my luck (in the informal sector with any kind of small business).

1. *Natafuta bingo, bwana.*

1. Natafuta pesa, bwana.

1. *Juma amezikamatia bingo.*

1. Juma amepata pesa.

2. *Yule msichana ana bingo.*

2. That girl has a boyfriend whom she fleeces.

2. *Nimempata bingo wa kuchuna.*

2. Nimempata mwanamume wa kumtoza pesa.

> *buzi*

bip[u] v *kupiga simu na kukata* let mobile telephone ring, then cut

Transfer from SE 'beep'.

Umenibip.

Umenipigia simu ukakata (ili nikupigie mimi).

> *promota*

bishoo, bishololo n5/6 *mtu anayejisikia, mtu ambaye anapenda kujionesha* fly guy
Transfer from SE 'big show' or from SE 'be show off'. The ending -lolo has an emphatic meaning.

Yule mshikaji ni bishoo tu!

Yule mshikaji anapenda kujionesha tu!

> *bitozi, tozi*

biti n *kitisho, vitisho* threat

Two etymologies were offered: 1. Terminal clipping of transfer from SE 'rivet', pronounced as "ribiti", used metaphorically 2. Transfer of SE 'beat'.

Usinichimbe biti.

Usinitishie.

Unaniweka biti.

Unanitisha.

> *mkwara, chimba biti*

bitozi n5/6 *mtu anayejisikia pasi na uwezo wa mambo ambayo anajivunia* fly guy, boaster, braggart

Metonymic extension of SE 'smart beetles'; in older Swahili slang (Ohly 1987a: 24) attested with the meaning 'nice guy'. One explanation was: This is because of the VW beetle, which makes much sound but can't go fast.

Yule jamaa, bitozi kweli yule.

That guy, he pretends to have everything.
> *bishoo, tozi*

blant[ji] n *msokoto wa bangi* joint (marijuana)
Transfer from American slang "blunt",
meaning a hollowed out commercial
cigar used to smoke marijuana. The
lexeme is an onomastic synecdoche of
the cigar brand "Phillies Blunt"
Masela wameingia kati kula blanti.
Marafiki wameenda nyumbani kuvuta bangi
> *kijiti*

blingbling, bringbring v *meremeta, ng'aa*
glitter, shine, be nice
Metonymic extension of English slang 'bling'
for 'jewellery'.
Pamba inablingbling.
Nguo nzuri inameremeta.

blingbling, bringbring n *mkufu mkubwa /*
mikufu mikubwa inayong'aa yenye thamani
kubwa sana glittering chain(s) and
necklace(s) of great value
Transfer from English slang 'bling' for
'jewellery'.
Washikaji wameng'arisha bringbring kali
kinoma.
Marafiki wamevaa mikufu mikubwa na ya
kung'aa mingi sana.

bloo
> *broo*

bloo v 1. *shangaa* 2. *penda* 1. be astonished
with wonder or admiration 2. like sb
Semantic extension of SE 'blow'. Also
attested for Sheng (Mbaabu & Nzuga
2003: 3).
1. *Watoto wa chuo kikuu wananibloo.*
1. Wasichana wa chuo kikuu
wananishangaza.
1. *Utafanya mambo mpaka utabloo.*
1. Utafanya mambo mpaka hutaamini.
2. *Nimembloo sana braza huyo hapa.*
2. Nimempenda sana huyo kaka.

bluu n_{9/10} 1. *noti ya shilingi 10000 ya zamani*
(no longer in use since the red notes were
issued in 2003) 2. *picha au mikanda ya video*
ya X 1. note of 10000 TSh. 2. blue internet-
sites; blue videos; X-rated videos
1. Metonymic extension of SE 'blue'. 2.
Ellipsis of SE phrase 'blue movie'.

2. *Tulikwenda internet, tulikuwa tunacheiki*
picha za bluu, bwana.

2. We went to an internet café and watched
blue pictures.
> 1. *buku teni* 2. *pilau*

boga n_{5/6} *mtu asiye na akili, mjinga,*
mpumbavu fool, stupid person
Metaphorical extension of SS *boga
'pumpkin'; especially used by teachers to
call unable pupils. Attested in older
Swahili slang as 'head' (Ohly 1987a: 24).
Old and common.
Wewe ni boga nini?
Wewe huna akili?
> *ziro*

boka n_{5/6} *bwege, mjinga* good-for-nothing,
simpleton, fool
< ? Derived from the character "Kaboka
Mchizi" in the cartoon "Songombingo ya
Kaboka Mchizi" by A. Kingo in the
newspaper "Kasheshe". This character
likes to get drunk and to steal.
Rafiki yangu usiwe boka.
Rafiki yangu usiwe mjinga.
> *mbwiga, mnyela, ndula, poyoyo, uboka*

bomba adj/n 1. *zuri* 2. *hali ya kulewa* 1.
beautiful, nice, handsome 2. drunkenness
Transfer from Italian "bomba" 'bomb', used
in colloquial expressions like "x é
bomba" 'x is very nice, super'. Italian
sailors could be the source. Or semantic
extension of SS *bomba 'syringe, big
pipe, pump'; probably derived from the
meaning 'hard blow' attested in older
Swahili slang (Ohly 1986a: 24).

1. *Demu yuko bomba.*

1. Msichana ni mzuri sana.

1. *Mademu bomba wameibuka.*

1. Wasichana wazuri wamekuja.

1. *Tangazo: Buzz ni bomba*

1. Commercial: Buzz (Mobile phone
company) is nice.

1. *Aisei, shosti leo umepigilia pamba,*
umetoka bomba.

1. Aisei, rafiki, leo umevaa nguo nzuri sana,
umetoka safi.

2. *Hapa nilipo nipo bomba kweli.*

2. Hapa nilipo nimelewa sana.

> 2. *bunduki, bwi, chicha*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

bombastiki n5/6 *msamiati mgumu* difficult, extraordinary vocabulary
Transfer from SE 'bombastic'. Very common in schools and colleges.

Mabombastiki ya mwalimu ni makali.

Misamiati ya mwalimu ni migumu sana.

bomu v 1. *omba vibaya* 2. *ongopea* 1. beg from someone, esp. money, cadge for, sponge 2. tell lies in order to get money
Metaphoric extension of SE 'bomb'.

1. *Walevi wa madawa ya kulevya hawaoni haya kumbomu kila mtu.*

1. *Walevi wa madawa ya kulevya hawaoni haya kumwomba kila mtu.*

1. *Yule amenibomu.*

1. That one has begged me.

1. *Nimeshambomu mama hela, twende zetu.*

1. Nimeshaomba hela kwa mama, kwa kumdanganya kuhusu matumizi, twende zetu.

> *piga mzinga, piga kirungu, jamaa wa virungu*

bomu n/adj 1. *kitu kibaya* 2. *feki, bandia* 1. bad thing 2. fake
Transfer from SE 'bomb', metaphorically used.

1. *Yule mwanamke kachukua bomu sana.*

1. Yule mwanamke si mzuri.

1. *Mfanyabiashara: "Mzigo wa safari hii bomu."*

1. Mfanyabiashara: "Bidhaa za safari hii ni mbaya sana."

2. *Hii mali ni nzima au bomu?*

2. Hii mali ni nzima au feki?

2. *Yule bomu tu yule.*

2. Yule hana ujuzi, hafai.

bonda v 1. *piga* 2. *maliza kitu* 1. beat, hit 2. finish

> ? Also in Kihore (2004: 9).

1. *Nitakubonda.*

1. Nitakupiga.

2. *Masela wamebonda jiwe lao.*

2. Marafiki wamemaliza shahada yao ya kwanza.

bondeni n.loc *Afrika kusini* South Africa

1. Semantic extension of SS *bondeni 'in the valley', motivated by orientation on maps, i.e. south = down. 2. Metaphorical extension of *bonde 'valley' as fertile area.

Leo nataka kuzamia meli kwenda bondeni.

Today I want to board a ship to South Africa as blind passenger.

Mshikaji mimi nikipata hela nitazama bondeni kwa Mzee Mbeki.

My friend, if I get money I will go to South Africa to live there illegally.

Dili likikubali nitazama bondeni.

If I get money from my business I will go to South Africa to live there illegally.

> *sauz*

bondo n5 *ugali porridge*

< ? Also attested in older Swahili slang (Gower 1958: 251, Ohly 1987a: 25).

Bondo la leo zuri utafikiri beche.

Ugali wa leo mzuri utafikiri wali.

> *dona, dongo, nafaka, nguna, sembe*

bonga v 1. *ongea* 2. *zungumza kwa lengo la mapenzi* 3. *ongea kitu cha uongo* 1. talk 2. talk with the intention of seducing sb 3. speak false words, cheat

< ? In older Swahili slang (Ohly 1987a: 25) attested with the meanings 'seduce; mix somebody up'. Also attested for Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 3).

1. *Bonga, basi.*

1. Sema, basi.

1. *Shosti njoo tubonge.*

1. Rafiki njoo tupige stori.

2. *Nimebonga naye.*

2. Nimezungumza naye kwa lengo la mapenzi.

bonga ung'eng'e v.phr 1. *ongea lugha ya*

Kiingereza 2. *ongea mambo yasiyoeleweka*

1. speak English 2. speak incomprehensively

1. Dysphemistic extension of older Swahili slang *bonga ung'eng'e 'talk nonsense'.

The singing and voice of the bird

*chiriku is called *ung'eng'e: Chiriku

anasema ung'eng'e 'the Chiriku bird is

speaking ung'eng'e'. It has different

melodies and can sing very fast. In LyM

*ung'eng'e means 'English'.

1. *Jamani, anabonga ung'eng'e vizuri sana.*

1. Friends, he can speak English very well.

> *bibisii, ingia external, tema ngeli, ung'eng'e*

bonge n5 1. *kitu kikubwa, kitu kizuri, kitu*

kinene 2. *mtu mnene* 1. big thing, nice thing

2. fat person

Semantic generalisation of SS *bonge 'lump, clod'; almost always used as a qualitative head noun in genitival constructions. In older Swahili slang (Ohly 1987a) attested as *bonge 'big thing' (25) and as *kibonge 'beauty; brutal person' (43).

1. *Lorand leo katinga bonge la mzula.*
 1. Lorand leo kavaa kofia kubwa..
 1. *Du babu lake, bonge la dili nikugee.*
 1. We rafiki, nikueleze siri kubwa.
 1. *Du acha, babu lake, bonge la bahati.*
 1. We acha, rafiki, bahati kubwa.
 1. *Du, huyu demu ana bonge la bambataa!*
 1. Du, huyu msichana ana matako makubwa!
 1. *Bonge la Coca Cola.*
 1. Chupa ya 0,5l ya Coca Cola.
 2. *Bonge la mama.*
 2. Mwanamke mnene.
 2. *Bonge yule amekuja.*
 2. Yule mtu mnene amekuja.
 2. *Yule ni bonge la jitu.*
 2. Yule ni mtu mkubwa na mnene kupita kiasi.

Bongo n.prop.loc *Dar es Salaam* Dar es Salaam

Hyperbolic metaphorical extension of augmentative derivative of SS *ubongo 'brain'. The term came up in the 80s, when it was forbidden to migrate to Dar es Salaam without permission. People who went there without permission were caught in the 'operesheni kuzuia uzururaji' (Operation 'prevent loitering'). Therefore it was very difficult to stay in Dar es Salaam. The term's use is now on the decline.

Ukikaa Bongo lazima uchemshe ubongo.
 If you live in Dar es Salaam, you have to use brains.
 > *Dizim*

Bongoland n.prop.loc *Tanzania* Tanzania
 Composite made of LyM "Bongo" 'Dar es Salaam' and transfer from SE 'land'. Not as common as "Bongo".

Ili uweze kuishi Bongoland, lazima uwe na miradi.
 Ili uweze kuishi Tanzania, lazima uwe na miradi.

bontaun v.phr *mtoto wa mjini, mtu wa mjii*

town-born child, person

Metonymic extension of SE 'born' plus 'town'. There is a range of orthographic varieties: bon-taun, bon-town, born-town. The expression also features prominently in a cartoon about two football teams "Bush Stars", a rural team, and "Born Town", an urban team, published in the magazine "Sani".

Unajua mi' ni bon-town.

Unajua mimi ni mtoto wa mjini.
 > *mbushi*

bravo adv 1. *nzuri* 2. *hongera* 1. well, good
 2. congratulations
 Transfer from Italian 'bravo'. Not common.
Hali? - Bravo!
Hali? - Nzuri!

braza n5/6 1. *kaka* 2. *rafiki* 1. brother 2. friend
 1. Transfer from SE 'brother'. 2. Semantic extension of SE 'brother'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 2).

Yule braza kanisaidia.

Yule kaka kanisaidia.
 > *broo*

brazameni n5/6 *rafiki* friend

Transfer from American slang *brotherman 'friend'. There is a connotation of 'being better off than a *msela'. The female counterpart is *sista du.

Mabrazameni wamekuja.

Marafiki wamekuja.

> *broo, sista du*

broo n5/6 *kaka, rafiki* friend, bloke, brother
 Truncation of SE 'brother' attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 25) as *bro.

Soo broo, wacha noma!

Hapana kaka, usilete balaa!

Mnachekei, washikaji, wakati nasevu mapaparazi wakanifotoa picha.

Mnaona, marafiki, wakati nilipotoroka, waandishi wa habari wakanipiga picha.

Yule broo kawamba bonge la kombati.

Yule kaka kavaa vest nzuri.

> *bloo, braza*

buku n9/10 *noti ya shilingi 1000 ya zamani*
 note of 1000 TSh. (since 2003 no longer in use)

Metonymic extension of SE 'book',

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

motivated either (a) by the design on the front side of the note which could be interpreted as showing a book, or (b) by the fact that these notes usually came in bundles resembling a book.

> *baba wa taifa, tenga*

buku teni n *shilingi 10000 10000 TSh.*

Metonymic extension of SE 'book' and 'ten': 'ten 1000 TSh. notes'.

> *wekundu wa Msimbazi*

bukua v *soma sana* study intensively

Metonymic extension of derivative based on SE 'book' or metonymic extension of SS *bukua 'discover, reveal, uncover, ferret out scandal'? Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 25). In KKS2.

Degera anabukua sana.

Degera studies very much.

> *chimba, keshu na vitabu, Joni Kisomo*

bulingibulingi

> *blingbling*

bunduki n10 1. *bia aina ya Lager* 2. *hali ya kulewa* 3. *nyonga kubwa* 1. Lager beer 2. drunkenness, state of being drunk 3. large hips

1. Metaphorical extension of SS *bunduki 'gun', based on the higher content of alcohol compared to other kinds of beer.
2. Metaphorical cum metonymic extension of SS *bunduki 'gun': "bunduki" is name for Lager beer, because it is said to be stronger than other kinds of beer. Also another etymology was offered: Just as a gun is controlled by its owner, a drunken man is driven by alcohol - he has no control over himself.

3. Metonymic extension of SS *bunduki 'gun', motivated by form of pistols worn in holster on hips in "cowboy-style".

2. *Jana nilimwona jamaa yuko bunduki.*

2. *Jana nilimwona jamaa aliyelewa sana.*

3. *Yule ana bunduki.*

3. *Yule ana nyonga kubwa.*

3. *Duh! Mary amefungasha mibunduki ya kufa mtu.*

3. *Duh! Mary ana nyonga kubwa sana.*

>2. *bomba, bwi, chicha, keroro, tungi, zimika*

>3. *bastola, pisto[l], silaha, mvinyo*

bunya v *kula kwa fujo* guzzle

< ? Probably derived from Sheng *bunyonga 'eat' (Mbaabu & Nzuga 2003: 22). Old and common

Oya, lete hiyo mihanjumati tuibunye.

Oya, lete hivyo vyakula vizuri tuvile.

bunyanga v *pata pesa bila kutarajia na*

kuzitumia ovyo get money without having expected it, and squander it

Metaphorical extension of *bunya 'guzzle'.

Wanafunzi walibunyanga kinoma.

Wanafunzi walipata pesa bila kutarajia na hawakutumia kwa busara.

bunyenye n *mtu mnene* fat person

< ?

Yule ni bunyenye.

Yule ni mnene.

bushi n *kijijini* rural area

Dysphemistic hyperbolic extension of SE 'bush'.

Alivyo utafikiri katoka bushi jana.

Alivyo utafikiri katoka kijijini jana.

Yule anaishi bushi.

Yule anaishi kijijini.

buti n5 *kondomu* condome

Euphemistic hyperbolic extension of SS *buti 'boot'

2. *Bwana, unapotaka kuchukua demu angalia, lazima uwe na buti.*

2. *Bwana, unapotaka kufanya mapenzi na msichana, lazima uwe na kondomu.*

2. *Nisaidie buti. (dukani)*

2. *Nisaidie kondomu. (dukani)*

> *ndomu, soksi*

butua v *piga mateke* kick, kick the ball wildly

Derivation from transfer from SE 'boot'.

Mchezaji yule anabutua tu mpira uwanjani.

Mchezaji yule anacheza na mpira ovyo, hachezi vizuri.

butuka v.stat 1. *jipokonya* 2. *ongea ovyo,*

ropoka 1. tear off sb 2. speak carelessly

Metonymic extension of derivative of LyM

*butua 'kick (the football) wildly'.

1. *Unachekei, bloo, basi, nikabutuka*

nikawasevu.

1. *Unaona, rafiki, basi, nikajipokonya*

nikawatoroka.

2. Pita anapenda kubutuka akiona watu.
2. Pita anapenda kuropoka akiona watu.
> *butua*
- buzi** n5/6 *mwanamume anayeliwa pesa na mwanamke kwa ajili ya mapenzi; mwanamume ambaye anamsaidia mwanamke matumizi kwa ajili ya kufanya mapenzi naye* man having a sexual relationship with a woman who aims at getting money out of him; temporary sexual partner of a woman, who is well-off and maintains her; (well-off) man who provides financial support for a woman in exchange for a sexual relationship.
Dysphemistic metaphorical extension of augmentative derived from SS *mbuzi 'goat'.
Mary amepata buzi.
Mary amepata mwanamume ambaye anampa pesa.
Mary anamchuna buzi.
Mary anapata pesa kutoka kwa mwanamume ambaye anatembea naye.
Hata ukinuna buzi tumelichuna. (Khanga writing)
Hata ukinuna, nimefanya mapenzi na mtu mwenye uwezo na nimeshapata cho chote toka kwake.
> *akademiki buzi, bingo*
- bwabwa** n5/6 *msenge* homosexual man
Euphemistic extension of SS *ubwabwa 'soft cooked rice'.
Masela eh! Huyo bwabwa anafanya nini hapa maskani?
Marafiki eh! Huyo msenge anafanya nini hapa nyumbani?
> *anti, chakula, choko, kaka poa, mshumaa*
- bwana** n5/6 *rafiki* friend
Semantic extension of SS *bwana 'master, Sir'. Used by men and women to address men and women alike. Very old and common
- bweche, beche** n5 *wali* cooked rice
< ? For the meaning 'gruel' attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 23).
Bondo la leo zuri utafikiri beche.
Ugali wa leo mzuri utafikiri wali.
Beche lile lilikuwa zuri.
Wali ule ulikuwa mzuri.

> *mavi ya panya, nyali, punje, pungu, ubeche, ubwabwa*

- bwena** adj *wingi wa kupita kiasi* exceedingly many, exceedingly much
< ?
Amenijazia maji kwenye glasi bwena.
Amenijazia maji kwenye glasi kupita kiasi.
Watu walikuwa bwena kweli.
Walikuwa wengi kupita kiasi.
- bwenzi** n *aina ya unyoaji wa nywele* style of haircut for men
Metonymic extension of SS *bwenzi 'quiff'.
Wengine wakatengeneza bwenzi.
Wengine walinyoa nywele kwa mtindo wa "bwenzi".
> *dungu, panki*
- bwi** id 1. *hali ya kulewa kupita kiasi* 2. *ujazo uliopita kiasi* 1. state of being excessively drunk 2. state of being more than full
1. Metaphorical semantic extension of 2.
1. *Jamaa kalewa bwi!*
1. That guy is excessively drunk.
2. *Kanijazie bwi!*
2. Fill (the vessel) for me more than full!
> *bunduki, chakari, chicha, keroro, tungi, zimika*
- bwimbwi** n9/10 *kokeni* cocaine
Metonymic extension of SS *bwimbwi 'ground pop-corn mixed with sugar'.
Pale kwa kina Juma wanauza bwimbwi.
Pale kwa kina Juma wanauza kokeni.
> *palma*
- byee** adv;adj *nzuri* cool, nice, good, fine
Probably transfer from French *bien 'good'; used in greetings as a reply to *hali vipi or *mambo.
Hali vipi? - Ni byee tu!
Hali vipi? - Nzuri tu!
> *baridi, poa, shwari*
- callbox**
> *kolboksi*
- chacha** v *kuishiwa pesa* be broke
Metaphorical extension of SS *chacha 'turn sour, go bad'.
Amechacha yule.
Amefilisika.
Wiki hii nimechacha.
Wiki hii nimeishiwa pesa.
> *arosto, waya*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

chachandu n9/10 1. *kichombezo cha chakula*
2. *shanga za kiunoni* 1. spicy appetiser 2.
waist lace made of beads
2. Metaphorical semantic extension of 1; 1.
and 2. very common
2. *Kama mwanamke hana chachandu si
mwanamke tena.*
2. *Kama mwanamke hana shanga za kiunoni
si mwanamke tena.*

chagizwa v.caus.pass *tiwa ari, sukumwa na
ari* be made eager
Semantic extension of SS *chagiza 'insist,
pester'
*Vijana walichagizwa na munkari wao wa
ngono.*
Vijana walisukumwa na hamu yao ya
kufanya mapenzi.

chai n9 *rushwa* bribe
Euphemistic metonymic extension of SS
*chai 'tea', also attested in older Swahili
slang (Ohly 1987a: 26). The metaphor of
'sipping chai' is used to signal the
warming-up phase of any procedure. In
this spirit, the bribe is conceptualised as
the necessary preliminary which sets
things in motion. Also attested in Sheng
(Mbaabu & Nzuga 2003: 4).

Pokea chai kidogo!

Kula rushwa!

Nipe chai, basi!

Nipe pesa nikanywe chai nikufanyie kazi
yako.

Unanipa kazi bila hata chai, bwana?

Unanipa kazi bila kutanguliza cho chote,
bwana?

> *chai ya rangi, soda, kitu kidogo*

chai ya rangi n.phr 1. *hafifu* 2. *rushwa ndogo*
1. broke, miserable 2. small bribe
Metonymic extension of SS *chai ya rangi
'black tea'.
1. *Mambo zao zinakuwa wasiwasi, chai ya
rangi.*
1. *Mambo zao zinakuwa wasiwasi, hafifu.*
2. *Jamani, aliniomba nimfanyie kazi yake,
nikamwambia nipe chai, chai yenyewe
ilikuwa ya rangi.*
2. *Jamani, aliniomba nimfanyie kazi yake,
nikamwambia anipe pesa kidogo
kwanza, lakini alichonipatia kilikuwa*

kidogo kuliko nilivyotegemea.
> *chai, soda*

chakula n7 *msenge, shoga* homosexual man
Euphemistic extension of SS *chakula 'food,
meal'. Also attested in older Swahili
slang (Ohly 1987: 26).

*Mwana, unamcheiki huyo bwege, nas'kia eti
ni chakula?*

Rafiki, unamwona huyo bwege, nasikia eti ni
msenge?

> *anti, bwabwa, choko, kaka poa, mshumaa*

chalala v *kutokuwa na pesa* be broke
< ?

Nimechalala kishenzi.

Nimeishiwa na pesa kabisa.

> *apeche alolo, arosto, majalala, waka*

chale n10 *hisia ya kitu fulani* sense, sentiment,
premonition
Semantic extension of SS *chale 'incision,
tattoo'?

Chale zikamcheza.

Amehisi kitu fulani / Ameshtuka.

> *machale, magutugutu*

chalii n5/6 *mvulana, kijana* boy, young man
Transfer from Sheng *chalii 'young man,
friend' (Mbaabu & Nzuga 2003: 4)?
> *mchalii*

chana v 1. *nenepa* 2. *fanya vizuri katika
mtihani* 1. grow fat 2. do well in exam
Metaphorical extension of SS *chana 'tear'.
1. *Siku hizi Declare kachana kishenzi.*
1. *Siku hizi Declare amenepa sana.*
2. *Ali alichana ile paper.*
2. *Ali alifaulu vizuri sana katika mtihani.*
2. *Alichana sana mtihani yake.*
2. *Alifanya vizuri katika mtihani yake.*

chana mistari v.phr *imba nyimbo za "rap"*
rap verses
Metaphorical extension of SS *chana 'tear'
plus *mistari 'lines'.
*Alishika maiki na kuanza kuchana mistari ya
traki yake.*
*Alishika maiki na kuanza kuimba wimbo
wake.*
> *achia mistari, dondosha mistari, shusha
mistari*

chana neti v.phr *kupa msichana mimba*
impregnate

- Metaphorical expression "tear the net", based on the image of a hard hitten ball tearing the net of a goal in a football match.
Jamaa kapiga bao kachana na neti.
 Jamaa kafanya mapenzi na msichana, kampa mimba.
- chang'aa** n9/10 *pombe ya kienyeji* locally brewed beer
 Metonymic extension of SS *ng'aa 'shine, gleam'. Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 26).
 > *mataputapu, mnazi, tungi, ulabu*
- changudoa** n5/6 *mwanamke anayejiuza kwa pesa; kahaba; malaya* female prostitute, commercial sex worker
 Probably dysphemistic metaphorical extension of SS *changu 'fish species' cherished as very good eating and SS *doa 'mark, blotch, stain', not confirmed by informants. This extension might partly be motivated by association with *changanya 'copulate' and *changua 'lay a woman' in older Swahili slang (Ohly 1987a: 26). In KKS 2.
Machangudoa wanakabiliwa na hatari ya ukimwi.
 Prostitutes are at risk of getting infected with AIDS.
- chanja** v *toza pesa; toza nauli katika daladala* extort money
 Hyperbolic extension of SS *chanja 'split'.
Babaake konda alichanja fasta!
 Rafiki, kondakta alitoza nauli upesi!
 > *chuna*
- chanja mbuga** v.phr *kimbia, pita pale pasipo na njia* run away, make off, slip away
 Metaphoric extension of SS *chanja 'incise' and *mbuga 'grassland': 'incise the grassland'.
Baada ya kuiba, mwizi amechanja mbuga.
 Baada ya kuiba mwizi amekimbia.
- chapaa** n9/10 *pesa* money
 Transfer from Kenyan Sheng.
Bwana, hili gazeti unauza chapaa ngapi?
 Bwana, hili gazeti unaliuza kwa shilingi ngapi?
Usiniletee matatizo, mimi nataka chapaa.
 Usiniletee matatizo, mimi nataka pesa.
- > *faranga, goto, mapene, mkwanja, mshiko, ngawila, uchache*
- chapa maji** v.phr *kunywa sana pombe* drink alcohol excessively
 Metaphorical and euphemistic extension of SS *chapa 'hit' plus *maji 'water'. Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 26). In KKS 2.
Yule amechapa maji.
 Yule amekunywa sana.
 > *piga maji*
- chapa nao** v.phr *fanya mapenzi* make love, have sex
 Pronominal form SS *nao referring to SS *uume 'penis', plus SS *chapa 'hit' Cf. older Swahili slang "chapa mimba" 'make pregnant' (Ohly 1987a: 26)
Punguza kumchapa nao kila siku.
 Punguza kufanya naye mapenzi kila siku.
 > *piga nao, piga bao*
- chapia** v.appl 1. *danganya* 2. *kosea katika matamshi, hasa ya maneno ya Kiingereza* 1. lie, cheat 2. mispronounce words, esp. in English
 Metaphorical extension of applicative derivation of SS *chapa 'hit'; probably ellipsis of the older Swahili slang phrase *chapa viboko 'cheat, dupe, take somebody in' attested in Ohly (1987a: 26).
Mara nyingi unachapia unapojaribu kuzungumza Kiingereza.
 Mara nyingi unakosea katika matamshi unapojaribu kuzungumza Kiingereza.
- chauchau** n *mbeya, mtu anayependa kusengya wenzake* gossip, sb who likes to spread rumours
 Onomastic synecdoche based on the name of Bi. Chau, a character in a TV programme who was a gossip par excellence.
Shoga tuondoke chauchau ameshafika.
 Shoga tuondoke mbeya ameshafika.
- chee** id *kwa bei rahisi* cheap
 < ? Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 27). In KKS 2.
Nilikwenda Kariakoo nimekuta nyanya chee.
 Nilikwenda Kariakoo nimekuta nyanya kwa bei rahisi.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Gari lenyewe bei chee.
Gari lenyewe bei rahisi.

chechetuka v.stat *kujipendekeza, nyenyekea*
ingratiates sb with sb, curry favour with sb
< ?

*Akijua una dili za mshiko tu anaanza
kuchechetuka.*

Akijua una mipango ya pesa tu anaanza
kujipendekeza.

cheki v *ona, hakikisha, tazama* see, make sure,
watch

Metonymic extension of SE 'check'. The less
adapted *check is also used in texts.

Njoo tucheki kioo.

Come and let's watch the video.

MaTZQ walikucheki.

Mapolisi wageni walikuona.

*Mnachekei, washikaji, wakati nasevu
mapaparazi wakanifotoa picha.*

Mnaona, marafiki, wakati nilipotiroka,
waandishi wa habari wakanipiga picha.

Mjage, basi, hapo geto kunichekishia!

Njoooni, basi, kuniangalia hapo chumbani!

Godi anatucheki.

Mungu anatuangalia.

Tomorrow nitakucheki kwenye runinga.

Kesho nitakuangalia kwenye video.

Sijui tutakucheki wapi tena.

Sijui tutakuona wapi tena.

> *chekishia*

chekibobu n *kijana anayejiweka, mtu
anayejirusharusha, kijana wa mjini, kijana
mhuni* male youth who is boasting, male
urban youth

Transfer from American slang *checkbob.

*Lakini wewe mwenyewe chekibobu
u'shamaliza.*

Lakini wewe mwenyewe ni kijana
anayejiweka, umeshajua mabaya yote.

Ali ana mambo ya kichekibobu.

Ali ana mambo ya kihuni (au ya ujana).

> *sista du*

chekishia v.caus.appl *angalia* watch, look at,
Derivation from LyM *cheki 'see'.

Leo kuna muvu poa sana tukalichekishie.

Leo kuna video nzuri sana tukaiangalie.

Mjage, basi, hapo geto kunichekishia!

Njoooni, basi, kuniangalia hapo chumbani!

Iko dei tutachekishiana mitaani.

Iko siku tutaonana katika pitapita zetu.
> *cheki*

chelea pina v.phr *safi* nice, well

Probably coined by rap artist II Proud in
1996 in his song "Moja kwa moja":
chelea pina - zali zalina noma sina.
Especially used in greetings. Now on
decline.

Mambo? - Chelea pina!

Mambo? - Safi tu!

chemka v.stat *kosea, tofanya kitu vizuri, fanya
vibaya* make a mistake, do sth badly

Metaphorical extension of SS *chemka 'boil'.

Umechemka usingemwambia.

Umekosea usingemwambia.

Ah! Timu yetu ilichemka kabisa!

Ah! Timu yetu haikuweza kufanya vizuri.

> *nyemka, tokota*

chemsha v.caus *toa jasho nyingi bila*

*mafanikio; kushindwa; kushindwa katika
kufanya kazi* do something in vain, invest
much effort without any result

Metaphorical extension of SS *chemsha
'boil', based on the image of cooking
beans or maize where boiling is the first
stage in its preparation. The image
implies that one gets stuck in the first
steps of a complex task, struggling hard,
but without being able to get past the
initial stages.

Degera amechemsha.

Degera ameshindwa.

chenza n5 *mwanamke asiye bikira* woman
who is not a virgin

Metaphorical extension of SS *chenza
'tangerine' Used in contrast to *chungwa
'orange' denoting a virgin. Concept: A
tangerine is easier to peel than an orange.
Introduced through a song by Suma Lee.

Hoya lile ni chenza.

Hoya, yule ni mwanamke asiye bikira.

> *chungwa*

chesa n9 *msichana bikira* virgin

Metaphorical extension based on the name of
the car model Toyota "Chaser" which has
high prestige. Used in contrast to *gofu
'girl who is not a virgin any more'. Rare.

> *gofu*

cheza bingo v.phr *bahatisha* try one's luck; participate in a game of chance
Metaphorical extension of SE 'bingo' (game of hazard, game of chance), which is also performed in Tanzanian TV; expression "play 'bingo'".
Vipi una dili gani? - Nacheza bingo.
What are you doing in order to get something? - I try my luck in some commerce.

cheza chesi v.phr *hadaa, danganya, tumia njia isiyo halali kwa ujanja* manouever, cheat
Metaphorical extension of SE 'chess'; expression "play chess". Not common
Nilicheza chesi polisi wakaniachia.
Nilidanganya polisi wakaniachia.

chee, chechee disc *nzuri* good, alright
< ? Standard reply to greetings such as *kidanka, or *danka. Probably development of the older Swahili slang forms *chee 'easy; free of charge' (Ohly 1987a: 27).
Yule ni msichana kama wa chee!
Yule ni msichana mzuri sana.

chicha n *hali ya kulewa kupita kiasi* drunkenness
Metonymic extension of SS *chicha 'lees, residuum after beer has been strained', motivated by the image of 'draining something to the lees', probably also related to the older Swahili slang *chicha 'native beer' attested in Ohly (1987a: 27).
Niko chicha.
Nimelewa sana.
> *bwi, bomba, bunduki, keroro, tungi*

chikichia v.appl 1. *elekea, ondoka* 2. *angalia kwa makini* 3. *ficha, fîcha sana, k.m. katika sehemu za siri* 4. *lala na msichana; danganya msichana (meaning provided by female informant)* 1. head for, go away 2. watch carefully 3. hide, hide very well, e.g. in private parts 4. sleep with a woman
Metonymic extension of derivative of SS *chikicha 'cut with a sawing motion, as with something blunt'.
Aliponidakisha mshiko tu nimechikichia.
Aliponipa pesa tu nikaondoka.
Mwanafunzi alichikichia kama mwalimu anamwona.

Mwanafunzi aliangalia kwa makini kama mwalimu anamwona.
Nimempa shilingi 200 aniletee machungwa.
Kaniletea ya shilingi mia na hamsini, hamsini kachikichia.
Nimempa shilingi 200 aniletee machungwa.
Kaniletea ya shilingi mia na hamsini, hamsini ameficha mfukoni.
Alichikichia mishiko yote.
Alificha pesa zote.
>

chikopa n *hali ya kupendeza kwa mavazi* smart look
< ? Introduced through a song by Fid Q (*Bongo Flewa*)
Suti uliyoivaa imekutoa chikopa.
Suti uliyoivaa imekupendeza.

chimba v *soma sana* study intensively
Metaphorical extension of SS *chimba 'dig'. Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 27).
Kuchimba kitu gani bwana, siyo bongo!
Kusoma kuna maana gani bwana, Dar es Salaam hakuna!
> *bukua, chimbo, Joni Kisomo, kesho na vitabu*

chimba biti v.phr *tishia kwa maneno* threaten verbally
Metaphorical extension from SS *chimba 'dig' plus LyM *biti which see
Usinichimbe biti.
Usinitishie.
Wandago walichimba biti la kutisha.
Mapolisi walitishia sana.
> *mikwara*

chimbo n5/6 1. *nyumbani* 2. *maficho* 3. *sehemu ya kubukua* 1. home 2. hiding place 3. retreat to study
Dysphemistic extension of SS *chimbo 'mine'
Twende chimbo!
Twende nyumbani!

chini adv *mambo ya ngono* sex
Metonymic extension of SS *chini 'beneath, below'.
Huyu jamaa anapenda chini sana.
Huyu jamaa anapenda mambo ya ngono sana.

chinja v 1. *mwanamke kutoza pesa kwa*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- mwanamume* 2. *mwanamke kufanya mapenzi kwa ajili ya kupata pesa* 1. women: extort money from men 2. women: make love in order to get money
Hyperbolic extension of SS *chinja 'slaughter'.
Mshikaji anamaindi kuchinja kinoma.
Yule rafiki anapenda sana kufanya mapenzi.
> *chuna, buzi*
- chizi** n 1. *mtu afanyaye mambo ya kihunihuni*
2. *rafiki* 1. cheater, hooligan 2. friend
Dysphemistic extension of SS *chizi 'stupid person, crazy person'. In older Swahili slang as 'white man, European' (Ohly 1987a: 28).
1. *Yule mtu si wa kufanya naye biashara, chizi kweli yule.*
1. *Yule mtu si wa kufanya naye biashara, mambo yake ya kihunihuni.*
2. *Chizi wangu vipi?*
2. *Rafiki yangu vipi?*
> *mento, kichizi, mchizi*
- choo** n7 *matatizo, ovyo, baya* trouble, something problematic, shit, bad
Dysphemistic metaphorical extension of SS *choo 'toilette'. Very popular in late 1990s.
Mambo yalikuwa choo.
Mambo yalikuwa mabaya.
> *kasheshe, kimeo, kizaazaa, msala, noma, sheshe, soo, zali*
- choo paspoti saizi** n.phr *choo chenye kuta fupi na ambacho hakina paa* outside toilet with low wall and no roof
Hyperbolic extension of SS 'toilet' and SE 'passport size'. In such a toilet the head and shoulders of a person can be seen from outside - like a passport photograph; expression 'toilet of passport size'.
Choo chetu cha paspoti saizi.
Choo chetu hakina kuta ndefu.
- chobi, chobingo** n9/10 *pembeni* corner
< ?
Oya mshikaji, njoo nikupe dili kiaina hapa chobi.
We rafiki yangu, njoo nikueleze siri kuhusu kitu fulani hapa pembeni.
- choko** n5/6 *msenge* homosexual man
Metaphoric extension of SS *choko 'oven'?
Or terminal clipping of LyM *chokolaa?
We choko nini?
Wewe ni shoga au nini?
> *anti, bwabwa, chakula, mshumaa, kaka poa*
- chokolaa, chokoraa** n5/6 *watoto wa mitaani ambao hawana sehemu pa kuishi* street children, homeless children
Metaphorical extension of transfer from French *chocolat 'chocolate'? Transfer from Kenyan Sheng *chokora.
Mtoto yule ni chokolaa.
Mtoto yule ni mtoto wa mitaani.
- choli** v *iba* steal
Transfer and semantic extension of Gujarati *choli 'thief'.
Babu kwa kucholi umezidi sana.
Rafiki kwa kuiba umezidi sana.
> *chomoa*
- choma** v *semea (kwa kuongeza uongo)* denounce, sell out (by exaggerating)
Metaphorical extension of SS *choma 'roast; pierce'.
Unaenda kuchoma kwa mshua.
Unaenda kusemea kwa baba.
- chombo** v *iba, dokoa* steal as a pick-pocket
< ? Seems to be variant of LyM *chomoa.
Nimetoka sokoni, nilipopita mtaa wa Kongo wakachombo ndizi kwenye kapu langu.
Nimetoka sokoni, nilipopita mtaa wa Kongo wakaiba ndizi kwenye kapu langu.
> *chomoa*
- chomekea** v 1. *tongoza* 2. *ingiza jambo mahali ambapo halikutarajiwa* 3. *ingiza gari mbele ya mwingine bila utaratibu mzuri*
1. seduce 2. chip in 3. overtake car in a hazardous way, because the space is very small
Semantic extension of SS *chomekea 'stick into'.
1. *Tulipokuwa tukiongea na yule demu kuhusu masomo nilichomekea swala la mapenzi, likajibu.*
1. *Tulipokuwa tukiongea na yule demu kuhusu masomo niliingiza swala la mapenzi, likafanikiwa.*
2. *Kwenye kikao nilichomekea ishuru ya likizo*

fupi.

2. Kwenye kikao niliingiza swali la likizo fupi katika agenda.
3. *Amenichomekea, afande.*
3. Ameniwekea gari mbele bila utaratibu, afande.

chomoa v.sep 1. *ondoka ghafla bila kupanga toka mwanzo* 2. *kataa, katalia ombi au shauri* 3. *iba* 4. *toa* 1. make off, go away abruptly 2. refuse to respond to an advice, or to a request 3. steal 4. give
Semantic extension of SS *chomoa 'pull out, unplug, extract, bring to light', related to the older Swahili slang *chomoa 'pinch, pick up sb's pocket, lend' (Ohly 1987a: 28).

1. *Alisimama katika foleni, akachomoa.*
 1. Alisimama katika foleni, akaondoka ghafla.
 1. *Dereva wa daladala alichomoa mchuma.*
 1. Dereva wa daladala aliondosha gari.
 2. *Alichomoa shauri.*
 2. Alikatalia shauri.
 2. *Nimempa dili kachomoa.*
 2. Nimempa kazi kaikataa.
 2. *Dereva wa daladala alichomoa kumlipa askari.*
 2. Dereva wa daladala alikataa kumpa askari pesa.
 3. *Kibaka alichomoa pochi ya Juma.*
 3. Mwizi aliiba pochi ya Juma.
 4. *Yule alichomoa pesa.*
 4. Yule alitoa pesa.
- > *timua*

chomoka v.stat *kimbia, toroka* run away, run away from

Stative derivation / backformation of SS *chomoza 'make a way out, come out'; also attested in the older Swahili slang phraseme *chomoka mbio 'run fast' (Ohly 1987a: 28), which is also still in use. In KKS 2.

Washikaji, chomokeni! Mamwela kibao wanakatiza maskani.

Jamani, kimbieni! Mapolisi wengi wanapita nyumbani.

Vicenti alimchomoka mama yake.

Vicenti alimtoroka mama yake.

Vick alichomoka mbio na kuipokea barua hiyo.

Vick alikimbia upesi na kuipokea barua hiyo

chomokea v *kumwendea msichana kwa nia ya kumtongoza* approach a girl in order to seduce her

Metaphorical extension of stative plus applicative derivation of SS *chomoa 'extract, take out'?

Wanadai eti kuna mchizi wetu anamchomokea demu wao.

Wanadai eti kuna rafiki yetu anamwendea msichana wao kwa nia ya kumtongoza.

chonde inj *tafadhali, naomba* please

Transfer from a local Bantu language, e.g. Yao, Makonde, Mwera. Also attested in older Swahili slang as *chondechonde 'please, please' (Ohly 1987a: 28)

chonga v 1. *ongea sana* 2. *toboa siri, eneza maneno (ya uongo)* 1. chatter, talk uselessly

2. give away secret, leak information
Metaphorical extension of SS *chonga 'carve'; probably ellipsis of the SS phraseme *chonga maneno 'invent a story'.

1. *Jamaa anachonga kweli.*

1. Jamaa anapenda kuongea sana.

1. *Unachonga sana siku hizi.*

1. Unaongea sana siku hizi.

2. *Yule amenichonga.*

2. Yule ametoboa siri yangu.

> *-pakaza*

chuchu saa sita n.phr *maziwa*

yaliyochongoka, maziwa yasiyoanguka female breast that points upwards, so that the nipples point also upwards like the hands of a clock in the 12 h position

Hyperbolic metonymic extension of SS

*chuchu 'nipple' and *saa sita '12

o'clock', based on the image of the

position of the hands of a clock at 12 h;

expression "nipple 12 o'clock".

Mtoto kaumbika, chuchu saa sita.

Msichana ameumbika, matiti yake yamechongoka.

> *matiti saa sita*

chuma n *bastola* pistol

Metonymic extension of SS *chuma 'iron'. In KKS 2 with remark "msemu". Also in KKS 1.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

*Dereva tekisi alivamiwa na majambazi.
Hakutaka kuwaachia gari, wakamtolea
chuma.*

Dereva tekisi alivamiwa na majambazi.
Hakutaka kuwaachia gari, wakamtolea
bastola.
> *mguu wa kuku*

chuma n *msichana mzuri, mtu au kitu chenye
maana* beautiful girl, girlfriend (or other
treasured objects)

Metonymic extension of SS 'iron', related to
the older Swahili slang item *chuma
'beauty' and the phraseme *mtoto chuma
'lovely girl' and *kama chuma 'fine,
O.K.' (Ohly 1987a: 28). Also attested in
Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 5).

Miye n'nacho chuma changu.
Miye n'naye msichana wangu.
Jamaani, yule ni chuma kweli.
Jamaani, yule ana maana kweli.
Yule msichana chuma kweli.
Yule msichana bomba kweli.

chuna v *toza pesa, pata kitu fulani kwa njia
ya kufanya mapenzi na mwanamume*
extort money, extort money from a man
in a sexual relationship

Metaphorical extension of SS *chuna 'flay'.
Common, ten years old.

*Wanachojua watoto wa mjini ni kuwachuna
wote wanaozubaa.*

Wanachojua watoto wa mjini ni kuwatoza
hela wote wanaozubaa.

Nimemchuna shilingi elfu tano.

Nimepata shilingi elfu tano kwa njia ya
kujiuza.

> *chinja, buzi*

chuna buzi v.phr *mwanamke kutoza pesa kwa
mwanamume ambaye anatembea naye* have
a sexual relationship with a man in order to
get money out of him

Metaphorical extension of SS *chuna 'flay'
and *buzi 'big goat'.

Mary anachuna buzi.

Mary ana mwanamume ambaye anampatia
pesa.

Hata ukinuna buzi tumelichuna. (Khangha
writing)

Hata ukinuna, nimefanya mapenzi na mtu
mwenye uwezo na nimeshapata cho

chote toka kwake.

> *buzi*

chungwa n5 *mwanamke bikira* virgin

Metaphorical extension of SS *chungwa
'orange'. Used in contrast to *chenza
'tangerine' denoting a woman who is not
a virgin any more. An orange can not be
peeled as easily as a tangerine.

Introduced through a song by Suma Lee.

Hoya lile ni chungwa.

Hoya, yule ni mwanamke bikira.

> *chenza*

chupi n9/10 *msichana, mwanamke* girl, young
woman

Dysphemistic synecdoche of SS *chupi
'underpant'. Attested in older Swahili
slang as 'mini skirt' (Ohly 1987a: 29)

Kulikuwa na chupi nyingi.

Kulikuwa na wasichana wengi.

chwee, chwee rega disc *hakuna* there is none

Probably development of the older Swahili
slang forms *chee 'easy; free of charge'
and *chewale 'cheap, free of charge'
(Ohly 1987a: 27) plus metaphorical
extension of SS *rega 'be careless; be
limp, be loose, be slack'.

Chwee [rega], babu lake, dongo limeyeyuka.

Hakuna, jamaa yangu, ugali umeisha.

chákari n *hali ya kulewa* drunkenness

Ellipsis of expression *amelewa chákari 'he
is extremely drunk'; SS *chakari 'more
than usually'. Probably originally
metaphorical extension of SS *chakari
'hangman'.

Yuko chákari.

Amelewa sana.

> *bunduki, bwi, chicha, bunduki, keroro, tungi,
zimika*

chélea pina disc *nzuri sana, safi sana,*

barábara very good

Semantic extension of SS *chelea 'be
apprehensive' plus unidentified second
element *pina? Standard reply to
greetings such as *kidanka, *hali vipi or
*mambo vipi. Sometimes heard as *bina.
Coined (?) and popularised through
Bongo Flewa song "Moja kwa Moja" by
II Proud on Album "Ndani ya Bongo" in

1996. The song has a line "Chelea pina zali zalina noma sina". On decline.
Tuliza boli, kichaa wangu, mambo chélea pina.
 Subiri mambo, rafiki yangu, mambo mazuri sana.
Natumaini mpo fiti, mambo chélea ya (?) pina.
 Natumaini mpo wazima, mambo mazuri sana.
Mambo chélea na nguvu pina.
 Mambo safi sana.
- dakika moja mbele** n.phr *mtu asiye na akili* stupid person
 Metaphoric expression: "one minute ahead".
 > *zezeta, zoba, ziro*
- dakisha** v.caus *pa give*
 Dysphemistic extension of SS *daka 'grab'.
Alinidakisha mshiko.
 Alinipa pesa.
Juzi nilimdakisha fuba.
 Juzi nilimpa pesa.
- dala** n 1. *sarafu ya shilingi 5* 2. *tano* 1. coin of 5 TSh. 2. five
 Metonymic extension of SE 'dollar', dating from the time, when one US-Dollar was worth 5 TSh (early 1980s).
 2. *Mchezaji wao namba dala aliwasaidia sana wasifungwe.*
 2. *Mchezaji wao namba tano aliwasaidia sana wasifungwe.*
 > *gobole, gwala; bee, taraa*
- dalika** v *ambukiza ugonjwa, hasa ukimwi* infect with a disease, especially AIDS
 <? .
Amemdalika.
 Amemwambukiza.
 > *dalikwa ngoma*
- dalikwa ngoma** v.phr *ambukizwa na ugonjwa, hasa ukimwi* get infected with a disease, especially AIDS
 <? Passive form of LyM *dalika 'infect' plus LyM *ngoma 'AIDS'.
Amedalikwa ngoma.
 Ameambukizwa ukimwi.
 > *dalika, ngoma*
- damdam, damu damu** n *hali ya kuwa rafiki wa karibu, lakini siyo mpenzi* relationship

- between close friend
 Semantic extension of SS *damu 'blood'.
Mimi na Juma ni damdam.
 Mimi na Juma tuna uhusiano wa karibu sana.
Wewe na mimi damu damu.
 Wewe na mimi tupo wa karibu sana.
- Dar kombaini** n *aina moja ya kitu au mtindo (wa kuvaa) unaoenea wakati fulani jijini Dar* any item or fashion (of clothing) which comes up in Dar es Salaam and lasts for some time
 Metonymic extension of SS *Dar 'Dar-es-Salaam' plus transfer from SE 'combine'.
 Expression: 'Dar es Salaam combine'.
Ile nguo ni nzuri lakini imekuwa Dar kombaini.
 Ile nguo ni nzuri lakini imevaliwa na watu wengi.
- data** v *hangaika, changanyikiwa* get puzzled, get nervous, be confused
 Metonymic semantic extension of SE 'data':
 having too much data causes confusion.
Madenti walisoma mpaka kudata.
 Wanafunzi walisoma mpaka kuchanganyikiwa.
 > *datisha*
- datisha** v.caus *hangaisha* puzzle, make nervous
 Causative derivation of LyM 'data'.
Kila unapopita masela unawadatisha.
 (Ngwair 2005: She Gotta Gwan)
 Kila unapopita wanaume unawahangaisha.
- debe** n5/6 1. *meli; gari* 2. *disco* 1. boat, ship; car 2. discotheque
 Dysphemistic extension of SS *debe 'tin, can'.
 1. *Leo nataka kuzamia debe kwenda bondeni.*
 1. *Leo nataka kuzamia meli kwenda Afrika Kusini.*
 1. *Fr. Celestino na Rolani wamekwea debe kwenda Gumbu.*
 1. *Fr. Celestino na Rolani wamepanda gari kwenda Gumbu.*
 2. *Tulijirusha debe mpaka liamba.*
 2. *Tulistarehe katika disko mpaka asubuhi.*
- debweza** v *kulegeza nguo (suruali) katika kiuno* loosen clothes at waist

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- < ?
> *kata kundu, kata kei, mlegezo, mdebwezo*
- dedi** v *kufa* die
Extension of transfer from SE 'dead'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 6).
Amededi.
Amekufa.
> *kata kamba*
- dege la jeshi** n.phr (n5) 1. *mtu asiyejjali* 2. *malaya, hasa yule anayeshukiwa kuwa ameathirika na ukimwi* 1. untidy person 2. prostitute, especially one who is suspected to have been infected by HIV
Hyperbolic metaphorical extension of augmentative of SS n.phr. *ndege ya jeshi 'bomber'.
2. *Mshikaji usifuatilie lile luzi, ni dege la jeshi, ni soo!*
2. Rafiki, usifuatilie yule msichana, ana hatari ya ukimwi, ni balaa!
- dei** n9 *siku* day
Transfer from SE 'day'.
Dr. Gwassa dei fulani kamotoa na mtutu.
Dr. Gwassa siku fulani kaondoka na pikipiki.
Ipo dei fulani mamwela walinijia kutaka niwagee ganja ili wanisobe rupango.
Ipo siku fulani polisi walinijia kutaka niwape bangi ili wanichukue gerezani.
Ipo dei nitakuja kukukill.
Ipo siku nitakuja kuuua.
Ms[h]irika, ipo dei tutawamba masuru ya jeans.
Rafiki, ipo siku tutavaa suruali za jinsi.
Iko dei tutachekishiana mitaani.
Iko siku tutaonana katika pitapita zetu.
- deile** adv *kila siku* daily
Transfer from SE 'daily'.
Deile mi' natimba skani.
Kila siku mimi naingia kijiweni.
- deiwaka** n5/6 *mtu mwenye ajira ya kubahatisha, mtu mwenye kazi isiyo na mkataba* labourer; worker without contract
Transfer from SE 'day worker'.
> *ushanta*
- demu** n5/6 *mwanamke ambaye hajaolewa, msichana mzuri* unmarried girl, lady, beautiful young woman
Semantic extension of SE 'dame', also reported for older Swahili slang as *dem (Ohly 1987a: 30) and for Sheng (Moga & Fee 1993, Mbaabu & Nzuga 2003: 6).
Yule demu yuko bomba.
Msichana yule ni mzuri sana.
Yule demu yuko pini.
Yule msichana ni mzuri sana.
Yule demu yuko magoli.
Yule msichana ni mzuri sana.
Mademu ni mapepe.
Wasichana ni wahuni.
Mademu bomba wameibuka.
Wasichana wazuri wamekuja.
Du, huyu demu ana bongela bambataa!
Du, huyu msichana ana matako makubwa!
> *kipopo, mlupo*
- denda** n5 *busu mdomoni* French kiss
Metonymic extension of SS *denda 'saliva'.
Nikamdaka Tom nikampa denda.
Nikamdaka Tom nikampa busu mdomoni.
Tulipeana denda jepesi.
Tulipeana busu jepesi mdomoni.
> *piga denda*
- denge** n9/10 *mtindo wa nywele wa kipolisi na kiaskari* haircut of police style: the hair is shaved around the ears
Metonymic extension of SS *denge 'goat pen built on poles, raised off the ground'.
Cognitive motivation: form. In KKS 1 and 2.
Mimi huwa napenda sana kunyoka denge.
Mimi huwa napenda sana mtindo wa nywele wa kipolisi.
> *bwenzi, pank[i]*
- dent[i]** n5/6 *mwanafunzi, mwanachuo, hasa msichana* student, mainly female
Initial clipping of SE 'student'.
Madent wa Kurio leo wametinga makatalogi.
Wanafunzi wa Kurio leo wamevaa nguo nzuri.
Denti yule amefanya fujo.
Mwanafunzi yule amefanya fujo.
- desa** n5/6 *karatasi au kitabu cha kutumia katika mihani kwa kuangalia majibu bila ruhusa* notes and books used for cheating in exams
< ? Popular in schools and colleges.
Wanafunzi walifaulu kwa madesa.

- Wanafunzi walifaulu kwa kuchungulia majibu kwenye karatasi.
> *kibuti*
- desa** v *danganya katika mtihani* cheat in exams
Semantic extension of SS *desa 'show off, put on airs'? Popular in schools and colleges.
Juma anapenda sana kudesa.
Juma anapenda sana kudanganya katika mtihani.
- dilei** v *chelewa* be late, be delayed
Semantic extension of transfer from SE 'delay'.
Alipodilei tu mzee mzima nikakunjuka.
Alipochelewa tu mzee mzima nikakimbia.
Amedilei.
Amechelewa.
- dili** n5/6 1. *siri, jambo* 2. *biashara, mpango, kazi* 1. secret, affair 2. business, project, work
Semantic extension of SE 'deal'.
1. *Oya mshikaji, njoo nikupe dili kiaina hapa chobi.*
1. We rafiki yangu, njoo nikueleze siri kuhusu kitu fulani hapa pembeni.
1. *Nipe dili!*
1. Nieleze siri!
1. *Sasa, washikaji, mnanitonya vipi kuhusu dili hili?*
1. Sasa, marafiki, mnanieleza vipi kuhusu jambo hili?
1. *Yupo mlami mmoja jina Lorand kanigea dili kuwa atanigea chesa.*
1. Yupo mzungu mmoja jina Lorand kanieleza siri kuwa atanipa gari.
2. *Nimempa dili kachomoa.*
2. Nimempa kazi kaikataa.
> *ishu, michongo*
- dingi** n *baba; mkuu wa sehemu; mtu muhimu mwenye pesa; mzee* father, daddy; leading man; important man with money; old man
< ? Since 1980s.
Habari za dingi?
How is your father?
Huyu ni dingi yangu.
Huyu ni baba yangu.
Huyu dingi mdosi kweli.
Huyu baba tajiri kweli.
- > *mdingi, mshua*
- Disiem** n *aina ya gari la abiria Toyota DCM* small bus "Toyota DCM"
Acronym.
- dizaini** n *mtindo, staili, muundo* design, style
Transfer from SE 'design'.
Nimependa sana dizaini ya kitanda kile pale.
Nimependa sana mtindo wa kitanda kile pale.
> *staili*
- dizaini dizaini** n. phr *mambo ya uongo, mambo ya utapeli* cheating, lying
Euphemistic extension of reduplication of LyM "dizaini".
Acha dizaini dizaini zako hapa.
Acha mambo ya utapeli yako hapa.
- Dizim** n.prop.loc *Dar es Salaam* Dar es Salaam
Derived from the acronym DSM for Dar es Salaam. Almost obsolete.
Kila mtu anatamani japo kufika tu Dizim.
Kila mtu anatamani japo kufika tu Dar es Salaam.
> *Bongo*
- dola** n *Shilingi 1000* 1000 TSh.
Transfer from SE 'dollar'. Used in connection with prepaid telephone cards. "Dola moja" denotes a voucher of 1000 shillings. By the time Vodafone introduced prepaid cards they gave the value in dollars, but they were paid in Tanzanian shillings.
Nipe vocha ya dola tano.
Nipe kadi ya simu ya shilingi elfu tano.
Nahitaji vocha ya nusu dola.
Nahitaji kadi ya simu ya shilingi mia tano.
- doma** n *sarafu ya shilingi 100* coin of 100 TSh.
< ? Not common.
> *alasisi, hais, jiti, nyanga, nyeta, pini*
- domo gundi** n.phr *mtu asiyependa au asiyeweza kuzungumza, mtu mzito wa kuzungumza* rhetorically slow and clumsy person
Dysphemistic metaphorical extension of SS *domo 'big lip' and *gundi 'glue'; expression "glue lip".
Yule jamaa domo lake gundi yule.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Yule ni mzito wa kuongea.

Yule ni domo gundi.

Yule ni mzito wa kuongea.

> *domo zito, domo zege, domo limejaa kokoto*

domo limejaa kokoto n.phr *tabia ya mtu asiyependa au asiyeweza kuzungumza, mtu mzito wa kuzungumza* rhetorical clumsyness and slowness

Dysphemistic extension of SS *domo 'big lip' and *jaa kokoto 'be full with gravel'; expression 'big lip full of gravel'.

Domo lake limejaa kokoto, hawezi kuongea.

Yule ni mzito sana wa kuongea.

> *domo gundi, domo zito, domo zege*

domo lina ujauzito idiom *kutokuwa na uwezo wa kuzungumza vizuri* be clumsy in speaking

Dysphemistic metaphorical extension of SS *domo 'big lip' and SS *ujauzito 'pregnancy': "big lip with pregnancy".

Domo lake lina ujauzito, hawezi kuongea.

Yule ni mzito wa kuzungumza, hawezi kuongea.

domo zege n.phr *mtu asiyependa au asiyeweza kuzungumza, mtu mzito wa kuzungumza* rhetorically slow and clumsy person

Dysphemistic metaphorical extension of SS *domo 'big lip' and *zege 'concrete'; expression "big lip of concrete".

Mdomo wake mzito sana, ni domo zege.

Yule ni mzito sana wa kuongea.

> *domo gundi, domo limejaa kokoto, domo lina ujauzito, domo zito*

domo zito n.phr *mtu asiyependa au asiyeweza kuzungumza, mtu mzito wa kuzungumza* rhetorically slow and clumsy person

Dysphemistic extension of SS *domo 'big lip' and *zito 'heavy'; expression 'heavy big lip'.

Yule hawezi kuongea, ni domo zito.

Yule hajui kuongea.

> *domo gundi, domo limejaa kokoto, domo zege*

dona n5 *ugali wa mahindi yasiyokobolewa* porridge made of maize flour from non-husked maize

Metonymic extension of SS *dona 'maize flour made from non-husked maize'.

According to Gower (1958: 251) the word was used in the 1950s with the meaning of 'maize flour'. It was derived from the name (MacDonald) of the owner of the first flour mill erected in Morogoro in Tanganyika.

Maisha ya jeli ni magumu, kila siku dona kwa maharage.

Maisha ya gerezani ni magumu, kila siku ugali kwa maharage.

> *bondo, dongo, nguna, sembe*

dondosha mistari v.phr *imba nyimbo za "rap"* rap verses

Metaphorical extension of SS *dondosha 'drop' plus *mistari 'lines'; expression "drop lines".

Akadondosha mistari ya traki zake.

Akaimba mistari ya wimbo wake.

> *achia mistari, chana mistari, shusha mistari*

dongo n5 *ugali porridge*

Dysphemistic extension of augmentative derivation of SS *udongo 'clay'.

Mshirika, leo n'na ubao kinoma, twenzetu kanigee dongo!

Rafiki, leo nina njaa sana, twende ukanipe ugali!

Chwefe] rega, babu lake, dongo limeyeyuka.

Hakuna, jamaa yangu, ugali umeisha.

Kama dongo hola, nigee basi hata ganja tu.

Kama ugali umeisha, nipe hata bangi tu.

> *bondo, dona, nguna, sembe*

du interj. *alama ya mshangao* ah, oh

< ? Very common, colloquial.

Du bloo, leo umevaa bongela saa.

Alaa, kaka, leo umevaa saa kubwa.

dungu n5 *kitu ambacho kwa juu si cha mraba, bali ni cha mviringo, k.m. basi aina ya*

Toyota Hiace anything which has a rounded top, e.g. bus model Toyota Hiace

Metaphorical extension of SS *dungu 'stage or platform, raised from the ground and often roofed over, for a watchman guarding crops on a plantation'.

Cognitive motivation: form.

Juma siku hizi anaendesha hais dungu.

Juma siku hizi anaendesha Toyota Hiace.

> *panki*

emolo

- > *emoro*
- emoro** n 1. *chupa ndogo ya Coca Cola* 2. *mtu mfupi* 1. 200 ml bottle of Coca-Cola 2. short person
Onomastic synecdoche based on Emoro, the name of a very small singer in the Congeese soukous band "Empire Bakuba". The founder Pépé Kallé was 2m10 tall. In their live shows both the giant Kallé and the dwarf Emoro danced to enchant the public (see: http://www.geocities.com/MotorCity/Speedway/4939/frames/art_bakuba.html).
Nimeenda bichi nikakutana na emoro.
Nimeenda bichi nikakutana na mtu mfupi sana.
> *sista P, pimbi*
- emsii** n5/6 *msanii wa Bongo Fleva* Master of ceremony (MC) in HipHop culture
Transfer from English.
Emsii huyo alishika maiki. (Sani 214:6-7)
MC huyo alishika mikrofoni.
- endesha** v.caus *harisha* have diarrhoea
Metaphorical extension of SS *endesha 'drive'.
Jana niliendesha sana wacha mchezo.
Jana niliharisha sana.
- fagilia** v *sifia kitu au mtu* praise sth or sb
Metaphorical extension of SS 'sweep at, sweep away'. Cognitive motivation: sweeping somebody is like cleaning him from all bad things, thus only good ones remain.
"Akihutubia, Rais Mkapa 'aliwafagilia' wagombea [...]." (Nipashe, 7.5.2005)
"Akihutubia, Rais Mkapa aliwasifia wagombea [...]."
"Jamaani tumfagilie sherehe yake" - "Wawaaa!"
"Jamaani tumsifie sherehe yake" - "Ndiyo!"
- famba** adj 1. *bovu (kitu)* 2. *bandia (pesa)* 1. sth rotten, bad 2. fake (money)
< ? New in 2005.
Hoya, mbona umenipa pamba famba ile.
Hoya, mbona umenipa nguo mbovu.
Ameniletea famba.
Ameniletea pesa bandia.
- faranga** n9/10 *pesa* money
Transfer from French 'franc'.
Oya nigee faranga.
Rafiki nipe pesa.
Katika mizunguko yangu nimepata faranga.
Katika mizunguko yangu nimepata pesa.
- fasta, fasta fasta** adv *upeshi, haraka, chapu chapu!* quickly, fast, quick quick!
Transfer from SE 'faster'.
Mbona uko fasta sana.
Mbona una haraka sana.
Nenda fasta fasta urudi.
Nenda haraka urudi.
Kwenye simu: Ongea fasta fasta, hela yenyewe ni ndogo.
Kwenye simu: Ongea haraka, hela yenyewe ni ndogo.
Fanya fasta mshikaji.
Fanya haraka rafiki.
> *shaa shaa, shuta shuta*
- fegi** n9/10 *sigara* cigarette
Transfer of SE 'fag', also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 33). Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 8).
Mshikaji, nigee fegi nipige pafu moja, nimekalukwa.
Rafiki, naomba sigara nivute kidogo, nimeishiwa.
Nipatie fegi mbili hapo.
Nipatie sigara mbili hapo.
> *mneli, munganya*
- feki** adj., n *ya bandia* fake
Transfer from SE 'fake'.
Hii mali ni nzima au feki?
Hii mali ni nzima au ya bandia?
- feruzi** n *ukimwi* AIDS
Onomastic synecdoche based on the name of the rapper Ferooz, who had a song about AIDS. Also, Feruzi is a Haya name, and AIDS started in Tanzania among the Haya in Kagera Region. Not common.
Ana feruzi.
Ana ukimwi.
> *ngoma, kanyaga miwaya, ngwengwe, umeme, shoti, virusi*
- fia** v.appl *penda mtu kupita kiasi* be very much in love
Hyperbolic ironic extension of SS *fia 'die

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

for', also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 33).

Nimekufia.

Nimekupenda kupita kiasi.

> *zimia*

fidodido n 1. *mtu mwembamba sana* 2. *mtindo wa nywele kwa wanaume: pembeni ya kichwa hakuna nywele, juu nywele zinakuwa nyingi* 1. very slim person 2. certain haircut preferred by males: sides of head are shaved, but on top there is hair left Metonymic extension of "Fido Dido", a character from a commercial of Pepsi Cola, which was used in Tanzania at the end of the 90s. Fido Dido, a gawky, cornball, very successful licensed character, was invented in 1985. He is very slim and has a triangular head with eight locks of scary, stand-up hair (see: <http://www.rmlicensing.com/ENG/Fido/fidodido.htm>).

1. *Wewe nini bwana, mtu mwenyewe fidodido tu.*

1. *Wewe nini bwana, mtu mwenyewe mwembamba sana tu.*

fiesta n *shati ya kiume yenye mikono mifupi* kind of T-Shirt for men

Onomastic synecdoche based on the name of the music festival "Fiesta". In the year of the first festival (ca. 2000) the T-Shirts appeared. Not common.

figa n *umbo mzuri wa mtu (mwanamke)* good figure (of woman)

Transfer of SE 'figure'.

Ah, msichana huyu ana figa nzuri sana. FL

Ah, msichana huyu ana umbo mzuri sana.

> *English figure, kimóbitel, kipótabo*

finya v *kula ugali* eat ugali

Metonymic dysphemistic extension of SS *finya 'pinch'.

Wacha tufinye nyali.

Wacha tule wali.

fisi n9/10 1. *sarafu ya shilingi 50.* 2. *mtu mwoga* 1. coin of 50 TSh. 2. coward Semantic extension of SS *fisi 'hyena', motivation unclear, since rhinos are imaged on the coin. Possibly rather derived from transfer of SE 'fifty';

attested as 'beer; booze' in older Swahili slang (Ohly 1987a: 33).

1. *Oya, nisusie fisi yangu!*

1. *Oya, nipe shilingi hamsini zangu!*

2. *Wewe fisi tu!*

2. *Wewe mwoga tu!*

fiti adj.inv *zima, zuri* fit

Transfer from SE 'fit'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 8).

Natumaini mpo fiti, mambo chelea ya pina.

Natumaini mpo wazima, mambo mazuri sana.

Mambo yapo fiti, mshirika?

Mambo yapo mazuri, rafiki?

Je, wewe uko fiti?

Je, wewe uko sawa?

> *fresh*

foma limau n.phr *simu ya mkononi kubwa* big-sized mobile phone

Onomastic synecdoche based on soap brand "Foma limau" which is a bar soap.

Cognitive motivation: form.

> *mshindi, mche wa sabuni*

foto n9/10 *picha, nakala* photo, photocopy

Transfer from SE 'photo'.

Washirika, tuishie, mapaparazi

watatuchukua foto.

Jamani, tuondoke, waandishi wa habari

watatupiga picha.

fotoa v *piga picha mtu au kitu* take a photo of sb or sth

Derivation based on SE 'photo'.

Mnacheki, washikaji, wakati nasevu

mapaparazi wakanifotoa picha.

Mnaona, marafiki, wakati nilipotoroka,

waandishi wa habari wakanipiga picha.

Kanifotoa mapicha kibao.

Akanipiga picha nyingi.

fresh[i] adj, adv *zima, zuri, safi, salama* fine, well, fresh

Transfer from SE 'fresh', attested in various forms of adaptation ranging from *fresh over *freshi to *fuleshi. Primarily used as reply to greetings such as *vipi, *mambo or *mitikasi.

Hali yake yuko fresh.

Hali yake yu mzima.

Mambo freshi gado!

Mambo yanaendelea vizuri sana!
Lorand kawamba gamba kiufuleshi.
 Lorand kavaa suruali maridadi.
 > *fuleshi*

fuba n5 *pesa* money
 < ? There could be a connection to *fupa
 'highly paid job' as attested in older
 Swahili slang (Ohly 1987a: 34).

Nilimdakisha fuba.
 Nilimpa pesa.
Majita wamenitaiti, wamelamba fuba lote.
 Wahuni wamenibana, wamechukua pesa
 zote.
Yule ana fuba kweli.
 Yule ana pesa kweli.
 > *mapene, mkwanja, mshiko, uchache*

fuga ndevu v.phr *kuwa na mpenzi wa kiume
 kwa mwanamume* live with a homosexual
 partner (men)
 *fuga as 'cohabit' attested in older Swahili
 slang (Ohly 1987a: 33)

fuleshi
 > *fresh[i]*

full kipupwe n.phr *hewa iliyopozwa sana,
 k.m. katika gari* air cooled by air condition,
 e.g. in a car
 Metaphorical extension of SS *kipupwe
 'rainy season'; expression "full rainy
 season". Obviously coined by *Bongo
 Flewa* artist Prof. Jay in his track "Zali la
 mentali" (the luck of the crazy one) in
 2001.

Gari iko full kipupwe.
 Katika gari kuna hewa baridi sana.
 > *kiyoyazi*

funga (ma)kamba v.phr *ongopa, sema
 uwongo, danganya* tell lies
 Metaphorical extension of SS *funga 'tie'
 plus SS *kamba 'rope'; expression "tie
 the rope". Referring to the image of sb
 being tied inside (kumfunga mtu ndani).

Jamaa kanifunga kamba.
 Yule amenidanganya tu.
Amenifungia kamba.
 Amenidanganya.
Anafunga kamba tu hapa.
 Anasema uongo tu hapa.
 Yule jamaa kwa makamba achana naye.

Yule mtu kwa uongo amezidi, humwezi.
 > *kamba, piga fiksi*

fungasha [nyuma] v *kuwa na matako
 makubwa* have large buttocks
 Semantic extension of SS *fungasha 'fasten
 sth behind sth else'. Mainly in the
 phraseologisms "fungasha nyuma" and
 "fungashia mzigo".

Yule amefungasha.
 Yule an matako makubwa.
Yule mama amefungashia mzigo.
 Yule mama ana matako makubwa.
Sasa alianza kufungasha nyuma.
 Sasa alianza kuwa na matako makubwa.
 > *jazia*

funika bovu v.phr *fanya vizuri kupita
 wengine, kitu kizuri kupita vingine* excel
 Hyperbolic metaphorical extension of SS
 *funika 'cover' and *bovu 'bad, rotten';
 expression "cover the bad thing".

Ile party ilikuwa funika bovu.
 Ile party ilikuwa nzuri hakuna mfano.
Kwenye disko tulifunika bovu.
 Kwenye disko tulistarehe kupita kiasi.
Jana ulifunika bovu babaake.
 Jana ulipendeza kupita kiasi, rafiki.

fweza n10 *fedha* money
 Derived from SS *fedha 'money'. Since
 1990. The augmentative *mafweza is
 more common.

Sina fweza.
 Sina fedha.
 > *mafweza*

fyeka mnazi v.phr *ua mtu* kill sb
 Euphemistic metaphoric extension of SS
 *fyeka 'weed' and *mnazi 'coconut tree';
 expression "weed/cut the coconut tree".

*Kiongozi wa majambazi kasema 'fyeka
 mnazi'.*
 Kiongozi wa majambazi kasema 'mwue'.

gado adj, adv *tayari; kamili, hodari, shupavu*
 ready; brave
 Semantic extension of SE 'guard' or based on
 SS *gadi 'prop, shore'?

Mambo fresh gado!
 Mambo poa tayari!
Nipo gado.
 Nipo kamili.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

gamba n5/6 1. *jinsi nzito* 2. *kitambulisho* 1. heavy jeans 2. identity card
Dysphemistic metaphorical extension of SS *gamba 'bark'.

1. *Lorand kawamba gamba kiufuleshi.*

1. Lorand kavaa jinsi nzito safi sana.

2. *Tumepewa magamba yetu jana.*

2. Tumepewa vitambulisho vyetu jana.

> *suru, ngozi*

gamu n5/6 *dawa ya kulevya, hasa aina ya mirungi* drugs

Transfer from Sheng (Kenya) *gamu (< SE 'gum'). It denotes "glue" in Kenya (Mbaabu & Nzuga 2003: 8), but in Tanzania it means *mirungi 'stimulant herb'.

Walilevywa sana na gamu.

Walilevywa sana na madawa ya kulevya.

Mshikaji nigee gamu yangu.

Rafiki nipe dawa yangu ya kulevya.

ganda v *simama sehemu moja kwa muda*

mrefu stand at a place for a long time

Metaphorical extension of SS *ganda

'coagulate, become hard; stick to'?

Attested as 'be garbled, be distorted' in older Swahili slang (Ohly 1987a: 35).

Ulikuwa ukiganda nyumbani.

Ulikuwa ukikaa sana nyumbani.

Kwa nini umemgandisha mwenzio hapa?

Kwa nini unamlazimisha mwenzio

kusimama hapa kwa muda mrefu?

Mbona jana ulinigandisha.

Mbona jana hukutokea pale sehemu

tulipokubaliana kukutana.

ganja n *bangi* Indian hemp, marijuana

Transfer from Jamaican Patois *ganja 'marijuana'.

Kama dongo hola, nigee basi hata ganja tu.

Kama ugali umeisha, nipe hata bangi tu.

Ipo dei fulani mamwela walinijia kutaka

niwagee ganja ili wanisobe rupango.

Ipo siku fulani polisi walinijia kutaka niwape

bangi ili wanichukue gerezani.

> *kijiti, msuba, ndumu, blant*

ganjia v.appl *patia, pa, gawia kitu, hasa pesa* pass, give, share sth (especially money)

Probably generalised derivation from Sheng

*ganji 'money or property with which to accomplish a given project; capital'

(Mbaabu & Nzuga 2003: 8).

Niganjie, basi.

Nipatie, basi.

Poa, tega antena nikuganjie dili!

Tulia, tega masikio nikueleze siri!

gashi n5/6 *msichana mzuri* girl, young, beautiful woman

< ? According to Gower (1958: 253) derived from Japanese 'geisha'. Also attested in older Swahili slang as 'desirable woman' (Gowert 1958: 253), and 'desirable woman; woman; homosexual man (queen)' (Ohly 1987a: 35).

Yule ni gashi wangu.

Yule ni msichana wangu.

> *pini*

gawa dozi v.phr *patia kipigo kikali, shinda* beat sb heavily, defeat

Metaphorical extension of SS *gawa 'divide, share' plus transfer from SE 'dose'; expression "share a dose". Very common.

Nikaona ananiletea longolongo ndo' nikaanza kumgawia dozi.

Nikaona kwamba analeta maneno ya uongo ndiyo nikaanza kumpa kipigo kikali.

Simba mwaka huu kazi yao kugawa dozi tu.

Simba mwaka huu kazi yao ni kushinda tu.

gea v *gawia, patia, toa, kupa* share, pass, give
Metonymic dysphemistic extension of SS *gea 'throw away, leave'.

Vipi mbona hamnigei stori, kuna soo au noma, washikaji?

Vipi mbona hamnipi habari, kuna tatizo au aibu, marafiki?

Ipo dei fulani mamwela walinijia kutaka niwagee ganja ili wanisobe rupango.

Ipo siku fulani polisi walinijia kutaka niwape bangi ili wanitie gerezani.

Du babu lake, bonge la dili nikugee.

We rafiki, nikueleze siri kubwa.

Yupo mlami mmoja kanigea dili kuwa atanigea cheser.

Yupo mzungu mmoja kanieleza siri kuwa atanipa gari.

Ali alinigea fisi jana.

Ali alinipa shilingi hamsini jana.

gei v *gawia, patia, toa, kupa* share, pass, give
Metonymic dysphemistic extension of SS

*gea 'throw away, leave'. Also attested in Sheng in the form *nigei 'give me' (Mbaabu & Nzuga 2003: 25). Seems to be restricted to the northern parts of Tanzania.

Mshikaji, nigei fegi nipige pafu moja, nimekalukwa.

Jamaa, naomba sigara nivute kidogo, nimeishiwa.

Mshirika, leo n'na ubao kinoma, twenzetu kanigee dongo!

Rafiki, leo n'na njaa sana, twende ukanipe ugali!

Kama dongo hola, nigei basi hata ganja tu.

Kama ugali umeisha, nipe hata bangi tu.

Oya bloo, nigei uchache kiaina.

Rafiki, unipe pesa kidogo.

gemu n9 mchezo game, match

Transfer from SE 'game'.

Gemu ya jana ni patulo.

Gemu ya jana imekuwa sare.

geto n chumba wanapolala vijana, chumba cha masela, maskani youths' (shared)

sleeping room; room, quarter

Dysphemistic extension of SE 'ghetto'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 9). Since end 1970s (Remes 1999: 13). Still very popular.

Du washikaji, hamwoni noma kuvinjari getoni!

La jamani, hamwoni aibu kuzunguka chumbani!

Mjage, basi, hapo geto kunichekishia!

Njoooni, basi, kuniangalia hapo chumbani!

Mie naenda geto.

Mie naenda maskani.

glasi n5/6 miwani glasses

Synecdochical extension of SE 'glass'.

Yule kapigilia glasi.

Yule amevaa miwani.

> *tivi, macho manne*

gobole n 1. kitu kikubwa (na cha zamani) 2. simu kubwa ya mkononi 3. sarafu ya shilingi tano ya zamani 1. something big (and outdated) 2. big mobile phone 3. coin of 5 TSh

Metonymic transfer of *gobori 'old muzzle-loading gun', based on its big size. In Kenyan Sheng as "kobole" with the

meaning of "coin of KSh. 5" (Mbaabu & Nzuga 2003: 15). The Kenyan 5-Shillings-coin is much bigger than the other coins, in Tanzania it is the second-biggest coin, but both are polygonal.

3. *Nimekwenda vijijini nikashangaa kukuta gobole bado linatumika.*

3. *Nimekwenda vijijini nikashangaa kukuta sarafu ya shilingi tano bado inatumika.*
> *dala, gwala*

godi n mungu god

Transfer from SE 'God'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 9).

Godi anatumchekei.

Mungu anatumchekei.

Godi akujalie safari poa.

Mungu akujalie safari nzuri.

gofu n9/10 gari ndogo ya polisi (VW Golf)

small police car (VW Golf)

Onomastic synecdoche based on the name of the car model "Golf".

Polisi na gofu yao walitembelea mitaa yetu.

Polisi na gari yao walitembelea mitaa yetu.

gofu n9 msichana asiye bikira girl who is not a virgin any more

Metaphorical extension based on the name of the car model Volkswagen "Golf" which has low prestige. Used in contrast to *chesa 'virgin'. Rare.

> *chesa*

gogo n garimoshi, treni passenger train

Dysphemistic extension of SS *gogo 'log, trunk (of tree)', or onomastic synecdoche of the name of the Central Tanzanian ethnic group? Not widely known.

Enzi zetu tulikuwa tunapanda gogo bure.

Enzi zetu tulikuwa tunapanda garimoshi bure.

goli n5 sehemu ya kazi work-place

Metaphorical extension of SS *goli 'goal'.

The same meaning is in older Swahili slang attested for *bao, which in Standard Swahili denotes also 'goal' (Ohly 1987a: 23).

Hili siyo goli langu, ni deiwaka tu.

Hapa siyo sehemu yangu ya kazi, nafanya kazi kwa muda tu.

Hapa ndipo golini kwangu.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Hapa ndipo sehemu yangu ya kazi.

golikipa n5/6 1. *mtu ambaye anapokea tu, mtu ambaye anasubiri vitu vya kuletewa* 2.

mama wa nyumbani 1. someone who is only receiving 2. housewife

Metaphorical extension of SE 'goalkeeper'.

1. *Unajidai hutaki kuwa golikipa.*

1. Unajidai hutaki kuwa mtu ambaye anapokea tu.

2. *Golikipa ni mgonjwa.*

2. Mke wangu, mama wa nyumbani, ni mgonjwa.

2. *Nisalimie golikipa.*

2. Nisalimie mke wako, mama wa nyumbani.

gonga ikulu v.phr *ongea pointi, pata kitu kizuri* talk sense, get something nice

Semantic extension of SS *gonga 'knock' and *ikulu 'state house': "knock at the state house". Not common.

Hapo amegonga ikulu.

Hapo ameongea pointi.

gonga ngozi v.phr *fanya mapenzi na*

msichana sleep with a girl, make love with a girl

Metaphorical expression "hit the skin"; SS *gonga 'hit, knock at' plus SS *ngozi 'skin, hide'.

Yule dada du! Nishamgonga ngozi!

Yule dada du! Nimeshalala naye kimapenzi.

> *kula ngozi, kaza, piga bao*

gonga pombe v.phr *kunywa pombe* drink alcohol

Semantic extension of SS *gonga 'hit' plus *pombe 'alcohol'.

Amegonga pombe.

Amekunywa pombe.

Amegonga mvinyo. (Prof. Jay)

Amekunywa pombe.

goto n5 *fedha* money

Derived from SS *gota 'knock, tap, strike'?

In Sheng attested for the meaning 'ten cent coin' (Mbaabu & Nzuga 2003: 9).

Oya, nisuusie goto langu.

Oya, nipe pesa zangu.

> *chapaa, mapene, mkwanja, mchuzi, mshiko, ngawila*

gozi n5/6 1. *kiatu cha ngozi halisi* 2. *mpira wa soka* 3. *noma, longolongo* 1. shoe made of

leather 2. football 3. trouble, lies

Hyperbolic metonymic extension based on an augmentative derivation of SS *ngozi 'skin, hide'.

> *bandapanda, buti, dula, lakuchumpa, ngozi, tumba*

gozigozi n 1. *hali ya kumzibia riziki mtu* 2.

poteza muda, zubaa 1. disrupt habit 2. lose time

< ? There seems to be no direct association with SS *ngozi 'skin', as informants rejected this notion.

1. *Ameniletea gozigozi.*

1. *Amenizibia riziki yangu.*

1. *Usiniwekee gozigozi.*

1. *Usinizibie riziki.*

2. *Acha gozigozi.*

2. *Acha kuzubaa.*

> *kiwingu, bania*

gubeli, gubeligubeli n5/6 *malaya* prostitute

< ? *guberi 'harlot' attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 36).

Shangingi gubeli limefika.

Malaya mnene mwenye umbo tata amefika.

> *mama huruma*

gwala n5 1. *sarafu ya shilingi 5* 1. coin of 5 TSh.

< ?

Nipe gwala langu la jana.

Nipe shilingi tano zangu za jana.

> *dala, gobole*

gwiji n5/6 *mtu maarufu, mchawi* expert, sorcerer

Metonymic extension of SS *gwiji 'expert'?

Huyu ni gwiji wa hapa.

Huyu ni mchawi wa hapa.

hais n9/10 *sarafu ya shilingi 100* coin of 100 TSh.

Onomastic synecdoche based on the name of the bus model Toyota "Hiace" for which a fare of 100 shillings used to be charged until recently.

> *jiti, nyeto, pini, alasiri*

haja kubwa n.phr *matako makubwa* big behind

Dysphemistic metonymic extension of SS *haja kubwa 'stool, excrements'.

Yule amefungashia haja kubwa.

Yule ana matako makubwa.
> *bambataa, kibinda, mkundu, ndómbolo, taarabu, tukunyema, shuzi, wowowo*

haluu inj *alama ya mshangao* expression of surprise
Derived from SE 'hallo'?
Haluu! Umependeza.
Aisee! Umependeza.

hola n *hamna, hali ya kukosa, hali ya kutofanikiwa* there isn't
Metonymic extension of the expression "hola", used by children in a game called "rede", where two players try to hit a third one with a ball. "Hola" means "you didn't hit me".
Kama dongo hola, nigee basi hata ganja tu. Kama ugali hamna, nipe hata bangi tu. Nimekwenda nikakuta hola.
Nimekwenda nikakuta hamna.

homligi n *mambo ya binafsi* private matters
Semantic extension of SE 'home league'.
Hoya, usiniingilie homligi yangu.
Hoya, usiniingilie katika mambo yangu ya binafsi.

hoya, oya excl *we!* hey!
< ? Used as a call for attention.
Hoya mshikaji, njoo nikupe dili kiaina hapa chobi.
We rafiki yangu, njoo nikueleze siri kuhusu kitu fulani hapa pembeni.
Hoya mshikaji, tuliza mapepe, usiwe na mzuka!
Rafiki, tuliza haraka, usiwe na wasiwasi!
Hoya pailoti, weka tuta!
We dereva, simamisha!

ibuka v 1. *kuja, chipukia, tokea* 2. *pata* 3. *fanikiwa* 1. come, appear 2. get 3. succeed
Semantic generalisation of SS *ibuka 'pop up, appear (of a problem), emerge, resurface'.
1. *Mademu bomba wameibuka.*
1. Wasichana wazuri wamekuja.
1. *Majambazi wameshaibuka huku.*
1. Majambazi wameshachipukia huku.
2. *Umeibukia maisha.*
2. Umefanikiwa katika maisha.
2. *Ameenda machimbo kaibuka.*
2. Ameenda machimbo kafanikiwa.

3. *Yule mtu baada ya kufilisika kaibuka tena.*
3. Yule mtu baada ya kufilisika karudia tena hali nzuri.

ile mbaya n.phr *sana, kupita kiasi, kabisa, mno* very much, exceedingly, too much
Dysphemistic semantic extension of SS *baya 'bad'.
John ananipenda ile mbaya.
John ananipenda kupita kiasi.
Tulikwenda kwenye pati, tukajichana ile mbaya.
Tulikwenda kwenye pati, tukala kupita kiasi.
> *kwa kwenda mbele*

ingia external v.phr *badili lugha (Kiingereza au Kilugha) ili watu wasiohusika wasielewe* swith to other language (English oder ethnic language) in order that bystanders cannot understand.
Onomastic synecdoche of the name of the English language radio programme "External Service" aired by Radio Tanzania; expression "enter external [service]".
Sasa wameingia external.
Sasa wameanza kusema Kiingereza.
Samahani, tunaingia external kidogo.
Samahani, tunabadili lugha kidogo.
Samahani, tuko external kidogo.
Samahani, tunasema lugha nyingine kidogo.

ingia laini v.phr *kubali* agree
Metaphorical extension of SS *ingia 'enter' plus transfer from SE 'line'; expression "enter the line".
Demu namchombeza lakini haingii laini.
Msichana namtongoza lakini hakubali.
Nilikwenda kuongea naye biashara fulani, ameshaingia laini, kesho mambo poa.
Nilikwenda kuongea naye biashara fulani, ameshakubali, kesho mambo safi.

ingia mitini v.phr *jificha, potelea mbali, kimbia* hide oneself, disappear, run away
Semantico-pragmatic extension of SS *ingia mitini 'enter the wood'.
Leo Degera kaingia mitini.
Leo Degera kajificha.
Mwenzetu kaingia mitini.
Mwenzetu katoroka na pesa.

inglish figa n.phr *msichana mwembamba,*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- msichana mzuri, umbo dogo wa mtu* slim lady, beautiful lady
Transfer from SE 'English figure'.
Yule ni english figa.
Yule ni msichana mwembamba.
Duh! Yule sholi ana english figa.
Duh! Yule msichana ni mwembamba.
Aisee! Jack ni english figa!
Aisee! Jack ni mwembamba.
> *figa, kimóbitel, kipótabo*
- inspekta** n *mchunguzi, mdadisi, mpelelezi, mtu mwenye tabia ya kujitia, mbeya, mkorofi* nosy and inquisitive person
Metonymic extension of SE 'inspector'.
Inspekta sema basi unataka nini?
Hey, inspector, what do you want?
Unajifanya inspekta hapa.
Unataka kujua mambo yasiyokuhusu.
- ishia** v.appl *ondoka* make off, run away
Metonymic extension of derivation of SS *isha 'finish, come to an end'.
Washirika, tuishie, mapaparazi watatuchukua foto.
Jamani, tuondoke, waandishi wa habari watatupiga picha.
Kapten John Degera kaishia na nzogolo ughaibuni.
Kapten John Degera kaondoka na treni nchi za mbali.
Du brother, unaishia majuu la!
We rafiki, unaondoka kwenda ulaya!
Ishia mbali huko!
Toka hapa!
> *timua, toa kiwingu, chomoa, anza, yeya, timka, kipa, jikata, jisanzua*
- ishu** n3/4 *mambo ya faraghani* secret or private matters, affairs. In older Swahili slang attested with the meaning 'food' (Ohly 1987: 38).
Transfer of SE 'issue'.
Njoo tuongee ishu kidogo.
Njoo tuongee faragha kidogo.
> *dili, mchongo*
- jamaa wa virungu** n.phr *mtu anayeomba vibaya* someone who is sponging, scrounging
Semantic extension of SS *jamaa 'guy' plus *virungu 'clubs'; expression "guy with clubs".
Yule jamaa wa virungu hafai.
- That scrounger doesn't fit.
> *piga kirungu, piga mzinga*
- jambazi** n5 *mwanamke asiye na mapenzi ya dhati, anayefanya mapenzi kwa ajili ya kujikimu* woman who has no true love, who goes with men in order to get a living
Metaphorical extension of SS *jambazi 'rogue'.
Mji huu una wanawake majambazi wengi sana.
Mji huu una wanawake wengi sana wasiye na mapenzi ya dhati.
> *shankupe, shuga memmi*
- janta** n5/6 *mhuni, mtu ambaye hana mke; hata mwanamke mhuni* wild youth, bachelor (only exceptionally used for women).
Probably transfer from SE 'giant' or Sheng *janta 'secret project' (Mbaabu & Nzuga 2003: 11).
Vipi janta wangu?
Vipi rafiki yangu?
Yule ni janta wangu.
Yule ni rafiki yangu.
> *mjita, msela*
- jazia haja kubwa** v.phr *kuwa na matako makubwa* have a big behind
Derivation of SS *jaza 'fill' plus *haja kubwa 'excretion', dysphemistic expression for "buttocks".
Yule amejazia haja kubwa.
Yule ana matako makubwa.
> *jazia sehemu za nyuma, mavi, shuzi*
- jazia kifua** v.phr *kuwa na maziwa makubwa* have big breasts
Semantic extension of SS *jaza 'fill'.
Yule mama amejazia kifua.
Yule mama ana maziwa makubwa.
> *fungasha*
- jazia sehemu za nyuma** v.phr *kuwa na matako makubwa* have large buttocks
Semantic extension of SS *jaza 'fill'.
Yule mama amejazia sehemu za nyuma.
Yule mama ana matako makubwa.
> *fungasha, jazia haja kubwa*
- jeitano** n *Jumatano Wednesday*
English pronunciation of abbreviation J for SS *juma, used for the days of the week beginning with "Juma": Jumamosi (J1),

Jumapili (J2), Jumatatu (J3), Jumanne (J4), Jumatano (J5) plus Swahili number. *Jeitano nilichelewa shuleni.* Jumatano nilichelewa shuleni.

jero n *noti ya shilingi 500* note of 500 TSh. Semantic extension of a truncated version of the name of the car model Mitsubishi "Pajero", motivated by the simultaneous appearance and prestige of both items. A note of this value was first issued in 1997.

Bwana nataka unipe vocha ya jero.
Bwana nataka unipe kadi ya simu ya shilingi mia tano.

jeruhi n5/6 *abiria alipaye sehemu ya nauli tu, k.v. wanafunzi* passenger who does not pay full
Derived from verb *jeruhi 'wound', meaning "wounded person". Metaphor used by daladala personnel to denote passengers who pay a reduced fare. The image comprises "wounded people" (who pay a reduced fare, e.g. students) and "corpses" (LyM **maiti*; who pay nothing, e.g. soldiers)

Tumebeba majeruhi wengi.
Tumebeba abiria wengi wanaolipa sehemu ya nauli tu.
> *kiroba, maiti*

jii Id *kimya* silence
(Transfer of) ideophone in some Bantu languages, e.g. Mwera, Yao, Makonde, representing silence. Perhaps since long in use by Swahili speakers in spoken language?

Mbona hatuonani bwana, tangu kipindi kile [...] ndio *jii!*
Mbona hatuonani bwana, tangu kipindi kile [...] ndio kimya!

jiachia v.phr 1. *ondoka eneo la tukio, kimbia* 2. *pumzika* 1. go away, run away, leave a place 2. make a pause, rest
Metaphorical extension of reflexive form of applicative derivation of SS *acha 'leave'.

1. *Amejiachia.*
1. Amekimbia.
1. *Jiachie bwana.*
1. Toka hapa, bwana.

1. *Baada ya kutoafikiana niliamua kujiachia kuepusha ugomvi.*

1. Baada ya kutoafikiana niliamua kuondoka kuepusha ugomvi.
2. *Nikimaliza mtihani nitajiachia.*
2. Nikimaliza mtihani nitapumzika.
> *anza, chomoa, ishia, jikata, jisanzua, kipa, kula bunda, lala mbele, piga bunda, tambaa, timka, timua, toa kiwingu, yeya*

jibu v *kuwa zuri, tokuwa na matatizo* be o.k. Metaphorical extension of SS *jibu 'answer'. *Kuna mambo nasubiria, yakijibu itakuwa freshi.*

Kuna mambo nasubiria, yakiwa mazuri itakuwa safi.
> *jibu, jipa, kaa freshi*

jichana v.phr *kula vizuri sana, kufaidi kwa chakula (na vitu vingine)* eat very good food, enjoy food (and other things like drinks)
Hyperbolic extension of reflexive form of SS *chana 'slit'.

Tumeenda hotelini tumejichana chipsi na soda.
Tumeenda hotelini tumekula chipsi na soda.
> *sunda*

jichanganya v.phr 1. *fanya kosa* 2. *hama, potea* 2. make a mistake 2. move, change address
Semantic extension of reflexive form of SS *changanya 'mix'. Attested in older Swahili slang as *changanya 'go away, move away; bolt' (Ohly 1987a: 26).

1. *Ah, nilijichanganya, bwana.*
1. Ah, nilifanya kosa, bwana.
2. *Nimejichanganya mjini.*
2. Nimehama na kupotea mjini.

jichenga v.phr *ingia* enter
Metonymic extension of reflexive form of SS *chenga 'evade'
Amejichenga kitaani.
Ameingia nyumbani.

jichimbia v.phr *hamia sehemu kwa kutumia njia za panya zisizo halali, na bila kutaka kurudi* disappear; leave the town or, illegally, emigrate to another country without planning to come back
Metaphorical extension of reflexive form of applicative derivation of SS *chimba

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

'dig'.

Bora nijichimbie huko Bongo.

Bora nizame huko Dar es Salaam.

> *zama*

jicho la mamba n5 *saa yenye rangi ya shaba*
watch of copper colour

Metaphorical extension of paraphrase of SS
*jicho 'eye' plus SS *mamba 'crocodile';
expression "crocodile's eye".

Du bloo, leo umewamba bonge la jicho la mamba.

Du, kaka, leo umevaa saa kubwa rangi ya mamba (shaba).

> *kidonda*

jicho la tatu n.phr 1. *mtazamo wa hekima au busara* 2. *bangi* 1. wise consideraton 2.

Indian hemp, marijuana

Metaphorical extension of SS *jicho 'eye' and SS *-a tatu 'third'; expression "third eye".

1. *Mambo yale lazima uyaangalie kwa jicho la tatu.*

1. Mambo yale lazima uyaangilie kwa hekima na busara.

> *ganja, kijiti, majani, ndumu, nyasi*

jicho nyanya n.phr *hali ya kulewa sana*
drunkenness

Metonymic extension of SS *jicho 'eye' and *nyanya 'tomato', motivated by the redness of one's eyes when drunk.

Yupo jicho nyanya.

Amelewa sana.

> *bwi, bomba, bunduki, keroro, tungi*

jidunga v.phr 1. *tumia madawa ya kulevya kwa kujichoma sindano* 2. *starehe, furahia, kunywa au kula (kitu fulani)* 1. use drugs by injection 2. enjoy something

Double metonymic extension of reflexive form of SS *dungu 'pierce, bore'.

1. *Washikaji kujidunga ni noma mnapoteza bure!*

1. Marafiki, kutumia madawa ya kulevya kwa kujichoma sindano ni vibaya, mnakufa bure!

2. *Anajidunga kunywa pombe.*

2. Anafurahia kunywa pombe.

jiegesha v.phr *kaa, tulia, pumzika* sit, rest
Generalisation of reflexive form of SS

*egesha 'park'.

Oya, naenda kujiegesha kijiweni.

Oya, naenda kukaa kijiweni.

Juma anajiegesha kule.

Juma anapumzika kule.

> *bana*

jigamba v.phr *jisifia, jiona bora kuliko wengine* boast

< ?

Juma anajigamba sana na vito vyake vya thamani.

Juma anajisifia sana na vito vyake vya thamani.

jikata v.phr *ondoka* go away, make off

Metonymic extension of reflexive form of SS *kata 'cut', referring to the separation from a group by going away. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 13).

Ah, mimi najikata bwana.

Ah, mimi naondoka bwana.

Jikate, bwana!

Toka hapa, bwana!

> *anza, chomoa, ishia, jisanzua, kipa, timka, timua, toa kiwingu, yesa, yeya*

jikoki v.phr *jiandaa, vaa vizuri, jiweka sawa*
prepare, dress os well

Probably metaphorical extension of reflexive form of SS *koki 'cock a gun'. Known from taarab lyrics.

Machizi wamejikoki freshi!

Marafiki wamejiandaa vizuri (hasa kwa kuvaa nguo nzuri).

> *jipeki*

jikweza v.phr *jipa sifa nyingi pasi na uwezo*
boast without reason

Metaphorical extension of reflexive form of causative derivation of SS *kwea 'climb'

Acha kujikweza, wewe ni mchovu tu.

Acha kujipa sifa wewe huna kitu.

> *jipaisha*

jimama, lijimama n5/6 *mwanamke mwenye mwili mkubwa na mrefu, bonge la mama,*

mwanamke mnene na anayependeza;

pengine anahusishwa na tabia ya kufanya

mapenzi na watoto wadogo big lady; sugar

mammy

Augmentative derivation of SS *mama.

- Babu jimama lile limeathirika.*
Rafiki yule mwanamke mnene labda
ameathirika na ukimwi.
> *tinginya, nyambizi*
- jinsi** n *suruali ya jeans* jeans
Transfer from SE 'jeans'.
Mshirika, ipo dei tutawamba masuru ya jeans.
Rafiki, ipo siku tutavaa suruali za jinsi.
> *mpayuko*
- jipa** v.phr *pendeza, tokuwa na matatizo* be o.k.
Metaphorical extension of reflexive form of
SS *kupa 'give'.
Kama mambo yanajipa, tuyese zetu.
Kama mambo ni mazuri, twende zetu.
Mambo yakijipa, kesho tutaenda kwenye muziki.
Mambo yakiwa mazuri, tutakwenda kwenye muziki.
> *jibu, kaa freshi, tiki*
- jipaisha** v.phr *jipa sifa nyingi pasi na uwezo*
boast without reason
Metaphorical extension of reflexive form of
causative derivation "paisha" (LyM) of
SS *paa 'fly'
Acha kujipaisha, wewe ni mchovu tu.
Acha kujipa sifa wewe huna kitu.
> *jikweza*
- jipeki** v.phr *jiandaa, vaa vizuri, jiweka sawa*
prepare, dress os well
Transfer from SE 'pack'.
Machizi wamejipeki freshi!
Marafiki wamejiandaa vizuri (hasa kwa kuvaa nguo nzuri).
- jirusha** v.phr *furahi, furahia, kwenda dansi, kunywa pombe, fanya mapenzi* enjoy in different contexts, party
Hyperbolic extension of reflexive form of SS *rusha 'make fly, make rush, throw'.
Anajirusha kwenye ukumbi wa sherehe.
Anafurahia mambo kwenye ukumbi wa sherehe.
- jisanzua** v.phr *ondoka* go away, make off
Metonymic extension of reflexive form of
SS *sanzua 'take sth away without permission of the owner'.
Baada ya maongezi marefu nikajisanzua.
Baada ya maongezi marefu nikaondoka.

- Jisanzue, bwana!*
Toka hapa, bwana!
> *anza, chomoa, ishia, jikata, kipa, timka, timua, toa kiwingu, yeya*
- jishaua** v.phr *jidai; jisifiasifia hata bila kuulizwa, jipelekapeleka mbele ya watu, jiona bora kuliko wengine pasi na uwezo wa mambo* claim falsely to be well off, boast
Dysphemistic extension of reflexive form of
SS *shaua 'make a useless show, be silly'? In older Swahili slang *shaua 'show off, display' (Ohly 1987a: 75).
Juma anapenda kujishaua.
Juma anapenda kujidai.
> *jishebedua, jishongondoa*
- jishebedua** v.phr *jipendekeza sana, jidai, jisikia, jipitishapitisha mbele za watu* flatter, ingratiate os
< ?
Acha kujishebedua mbele za wanaume.
Acha kujipitishapitisha mbele za wanaume.
> *jishaua, jishongondoa*
- jishongondoa** v.phr *jipitisha katika nafasi ambayo mtu hana uwezo nayo, jidai, jipitishapitisha mbele za watu* flatter, ingratiate os
< ?
Acha kujishongondoa.
Acha kujipitishapitisha mbele za watu.
> *jishaua, jishebedua*
- jiti** n5 *sarafu ya shilingi 100* coin of 100 TSh
Hyperbolic extension of SS *jiti 'big tree', motivation unclear.
Acha utani mbele ya jiti langu.
Acha uzushi, nipe mia yangu.
> *hais, nyeto, pini, alasiri*
- jiwe** n5 1. *pesa* 2. *msichana* 3. *shahada ya kwanza* 1. money 2. girl 3. first degree
Metaphorical extension of SS *jiwe 'stone'.
Also attested in older Swahili slang as 'girl who yields to nobody in strong language' (Ohly 1987a: 40).
1. *Mshikaji ana jiwe baya.*
1. Rafiki ana pesa nyingi.
2. *Jiwe langu umeliona?*
2. Msichana wangu umemwona?
3. *Masela wamebonda jiwe lao.*
3. Marafiki wamemaliza shahada yao ya kwanza.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

> *chuma, kifaa*

joblesi kona, joblesi n.phr *kijiweni* place where jobless youths meet
Transfer from SE 'jobless' and 'corner'; expression "corner of the jobless".

Leo nitakuwepo joblesi kona pale.

Leo nitakuwepo kijiweni pale.

> *kijiweni*

Joni Kisomo n.phr *mtu ambaye anasoma sana, hata kwa kukesha* someone who studies intensely, even during the night
Onomastic synecdoche based on a nickname composed of transfer from SE 'John' plus diminutive of SS *somo 'subject, lesson'.

Yule si ni Joni Kisomo? Hana muda wa kustarehe.

Yule si anasoma sana? Hana muda wa kustarehe.

juu ya mawe n.phr *kuwa bila kazi* be without job

Metaphorical expression 'on the stones', based on the image of a car which is broken down and jacked up on stones.

Niko juu ya mawe karibu mwezi sasa.

Niko bila kazi karibu mwezi sasa.

Kukaa juu ya mawe kwa maisha ya sasa hivi ni shida.

Kuwa bila kazi kwa maisha ya sasa hivi ni shida.

juu ya mstari n.phr *safi, nzuri* fine, o.k.

Metonymic extension of expression used for headlines in (news)papers, meaning "main point". Used as reply in greetings.

Mambo vipi? - Juu ya mstari!

Mambo vipi? - Safi!

jumba bovu n.phr *matatizo kwa ajili ya kitu ambacho mtu mwenyewe hajafanya* trouble on cause of being accused for sth one has not done

Metaphorical extension of augmentative SS *jumba 'big house' plus *bovu 'dilapidated'; expression "big dilapidated house".

Baada ya mtoto kupotea jumba bovu liliniangukia.

Baada ya mtoto kupotea nilipata matatizo makubwa sana.

Washikaji kuweni makini jumba bovu

linaweza kuwaangukia.

Marafiki kuweni makini, mnaweza kusingiziwa makosa ambayo hamjafanya.

> *shobo*

kaa freshi v.phr *kuwa zuri, tokuwa na matatizo* be o.k.

Metonymic extension of SS *kaa 'sit' plus transfer from SE 'fresh'.

Kama mambo yanakaa freshi, tutakwenda muziki.

Kama mambo yatakuwa mazuri, tutakwenda kwenye muziki.

> *jibu, jipa, tiki*

kabwela n 1. *mtu mjanja mtafutaji* 2. *mtu asiye na kitu, mtu mwenye hali ya chini, asiye na uwezo* 3. *mtu asiye na mke* 1. sly and deceitful person 2. poor person, powerless person 3. man without wife
Semantic extension of SS *kabwela 'poor person; fraud, hypocrite, deceiver; arbitrary and unfair use of force'? There are partly contradictory glosses for this item. Morino & Nakazima (1993: 739) have "mtu wa kawaida asiye na pato kubwa" which seems to fit best here, confirmed by older Swahili slang *kina kabwela 'people of low income group' (Ohly 1987a: 45). However, Rechenbach 1968, mentions two deviant meanings: (1) (unfair, arbitrary) use of force / power, (2) a person who conceals his true motives / acts on false pretenses (who claims to need something which he really does not need, etc.), hypocrite, deceiver, fraud. Ohly (1987a: 41) finally gives 'insecticide' as a older Swahili slang meaning.

Hassani ni kabwela usisadiki yote asemayo.

Hassani ni mjanja usisadiki yote asemayo.

Kabwela kama mimi nitaweza wapi, bwana?

A poor guy like me, how could I afford?

kachala n *rafiki* friend

< ? Attested in older Swahili slang with the meanings 'old and worn' and 'ugly girl' (Ohly 1987a: 41).

Bora kachala wangu umekuja unitoe na jiti.

Ni vema, rafiki, umekuja, unipe shilingi mia.

kachaso n9/10 *pombe kali sana haramu,*

- gongo* illicit hard liquor
< ?
Ulikuwa chicha sana jana, lazima utakuwa ulichanganya na kachaso!
Ulilewa sana jana, lazima utakuwa ulichanganya na gongo.
- kaka poa** n.phr *msenge, shoga* homosexual man
Euphemistic extension of SS *kaka 'brother' and *poa 'cool, relaxed'; expression 'cool brother'.
Peter ni kaka poa.
Peter ni msenge.
> *anti, bwabwa, chakula, choko, mshumaa*
- kalikiti** n *dawa ya kutilia nywele mawimbi*
curl kit
Transfer from SE 'curl kit'.
Asha ameweka kalikiti nywele zake.
Asha ameweka dawa ya mawimbi nywele zake.
- kalukwa** v 1. *ishwa pesa* 2. *kuwa na shida ya akili* 1. run out of money
< ? Derivation from colloquial Swahili *kauka 'be broke'. Intervocalic *l suggests influence from another Bantu language.
Mshikaji, nigeefegi nipige pafu moja, nimekalukwa.
Jamaa, naomba sigara nivute kidogo, nimeishiwa pesa.
Yule amekalukwa.
Yule ni chizi.
> *pigika, rosti, uawa, mabaga*
- kama hana akili nzuri** v.phr *safi kabisa, vizuri sana* very well
Dysphemistic hyperbolic extension of SS *hana akili nzuri 'he / she has no brains'.
Ameimba kama hana akili nzuri.
Ameimba vizuri sana.
> *kishenzi, kinoma*
- kama kawa** n.phr *kama kawaida* as always
Terminal clipping of SS *kawaida in "kama kawaida".
Nitakuona kesho kama kawa.
Nitakuona kesho kama kawaida.
- kama Kenya** n.phr *safi, nzuri* fine, o.k.
Metonymic extension of SS *Kenya, based on the comparatively high living

- standards there. Used as reply in greetings.
Mambo vipi? - Kama Kenya!
Mambo vipi? - Safi!
- kamba** n *uongo* lie
Ellipsis of LyM expression "funga (ma)kamba" 'tell lies'.
Acha kamba wewe.
Acha uongo wewe.
> *funga (ma)kamba, piga fikisi*
- kamua** v 1. *pata faida* 2. *fanya mambo kwa bidii ili kupata faida* 3. *furahia* 1. get profit
2. work hard to get profit 3. enjoy
Metaphorical extension of SS *kamua 'squeeze out, make sb bankrupt'
1. Leo tumekamua.
1. Leo tumepata faida.
2. Usilale babu! Kamua tu.
2. Usizubae, rafiki! Fanya bidii ili upate faida.
- kandamiza** v.caus 1. *kula* 2. *fanya mapenzi mwanamume kwa mwanamke* 3. *pata pesa, pata faida* 4. *soma* 1. eat 2. make love (man to woman) 3. get money, get profit 4. read, study
Hyperbolic metaphorical extension of SS *kandamiza 'press heavy on sth, suppress'.
1. Twende kukandamiza msosi.
1. Twende kula chakula.
1. Hoya, tunakwenda zetu mgahawani kukandamiza.
1. Hoya, tunakwenda kula chakula mgahawani.
2. Wapi bwana? - Naenda kukandamiza demu.
2. Wapi bwana? - Naenda kufanya mapenzi na demu.
3. Kondakta: Ah, leo nimekandamiza sana.
3. Kondakta: Ah, leo nimepata sana faida.
4. Naenda kukandamiza buku.
4. Naenda kusoma kitabu.
- kanyaga miwaya** v.phr *pata ukimwi* get infected with HIV
Metaphorical extension of SS *kanyaga 'step on' and augmentative plus plural from SS *waya 'wire' expression "tread on wires".
Amekanyaga miwaya.
He/She has been infected with HIV.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

kapelo n9/10 *polisi* police

< ?

Kapelo zitatia timu.

Polisi watakuja kwa kundi.

> *njago, mwela*

karaghabao, kalaghabao, kalaga baho n

hasara loss

< ?

Sijapata lo lote, karaghabao.

Sijapata lo lote, hasara tu.

Kama wewe huamini kalaga baho.

Kama wewe huamini, hasara yako.

karai n5 *division "C" katika matokeo ya*

mitihani division "C" in school results

Metonymic extension of SS *karai 'metal basin' based on form: the silhouette of a basin (in upright position) resembles the shape of a "C".

karume n9/10 *sarafu ya shilingi 200* coin of TSh. 200

Onomastic synecdoche based on Karume, the name of the first president of Zanzibar whose portrait is on the coin.

Bei gani? - Karume.

Bei gani? - Shilingi mia mbili.

> *mbala*

kasheshe n *vurugu, vurumai, tukio baya,*

matatizo, patashika furore, mayhem

Euphemistic extension of SS *sheshe

'beautiful' by use of pejorative prefix

*ka- (class 13)? In KKS 2.

Pale kuna kasheshe gani?

Pale kuna vurugu gani?

Noma bwana, umwache, usimfanyie

kasheshe.

Si vizuri, bwana, umwache, usimfanyie

vurugu.

Jamaa ameleta kasheshe.

Jamaa ameleta vurugu.

> *zohali, sheshe, noma, soo*

kashikashi n9 *fujo kubwa, pilikapilika kubwa*

great chaos

< ? Probably derived from LyM *kasheshe

'mayhem' or from SS *kashfa 'scandal,

libel'.

Kashikashi kubwa iliwapata majirani.

Fujo kubwa iliwapata majirani.

Nilimletea kashikashi mpaka akanilipa

changu.

Nilimletea fujo kubwa sana mpaka akanilipa changu.

kataa v *acha mtu, kana mtu* leave sb

Metonymic extension of SS *kataa 'refuse, reject'. New in 2005.

Nilipomwona amelewa chakari nilimkataa.

Nilipomwona amelewa sana nilimwacha.

kata gogo v.phr *kwenda haja kubwa, toa choo*

kavu defecate, shit

Hyperbolic extension of SS *kata 'cut' plus

SS *gogo 'log'; expression "cut a log".

Acha, nikakate gogo sasa.

Acha, nikaende haja kubwa.

kata kamba v.phr *kufa* die

Semantic extension of SS *kata 'cut' plus SS

*kamba 'rope', also attested in older

Swahili slang (Ohly 1987a: 42);

expression "cut the rope".

Asha amekata kamba.

Asha amekufa.

> *poteza, vuta kamba*

kata kei / kata k. v.phr *suruali inayokaa*

kiunoni loosely fitting trousers, low cut trousers

Euphemistic abbreviation of LyM "kata kundu" 'cut the big anus'

Yule amevaa kata kei.

Yule amevaa suruali ya mlegezo.

Keni anapenda kuvaa kata kei.

> *kata kundu, mlegezo*

kata kilauri v.phr *kunywa pombe* drink beer

Metonymic extension of SS *kata 'cut' plus

derivation of SS *bilauri 'drinking-glass,

tumbler', similar phraseme attested in

older Swahili slang *kata matindi 'drink

liquor' (Ohly 1987a: 42). Not common.

Leo tumekata kilauri.

Leo tumekunywa pombe.

> *ulabu*

kata kundu v.phr *suruali inayokaa kiunoni*

loosely fitting trousers, low cut trousers

Dysphemistic metonymic extension of SS

*kata 'cut' plus augmentative *kundu of

SS *mkundu 'anus'; expression "cut the

big anus".

> *mlegezo, kata kei*

kata shingo v.phr 1. *tazama kitu au mtu, hasa msichana, kwa kugeuza shingo, shangaa* 2. *acha kutazama (kitu/mtu fulani) kwa kugeuza shingo* 1. stare at sth or sb who is moving, esp. a woman by turning the neck 2. stop staring at sb

Hyperbolic extension of SS *kata 'cut' plus SS *shingo 'neck'; expression "cut the neck".

1. *Amekata shingo.*

1. *Ameangalia kwa kugeuza shingo.*

2. *Kata shingo, bwana.*

2. *Acha kutazama kwa kugeuka.*

> *shingo feni, macho bal[u]bu*

kata stimu v.phr *katisha tamaa* disappoint, frustrate

Metaphorical extension of SS *kata 'cut' plus SE 'steam'; expression 'cut the steam'.

Umenikata stimu.

Umenikatisha tamaa.

katalogi n5/6 1. *nguo au viatu vizuri na vya kisasa, vyenye thamani kubwa; fasheni* 2. *katalogi, tovuti* 1. nice modern cloth of quality and fashion 2. catalogue, website

Euphemistic extension of SE 'catalogue'; clothing catalogues are in use to see what is in fashion.

1. *Madent wa Kurio leo wanatinga makatalogi.*

1. *Wanafunzi wa Kurio leo wamevaa matishati mazuri.*

2. *Katalogi ya chuo ni babu kubwa!*

2. *Tovuti ya chuo ni safi kabisa!*

kauka v 1. *kaa kimya, nyamaza* 2. *isha kwa hela* 1. keep quiet 2. run out of money

Stative derivation of LyM *kausha 'be quiet'.

1. *Baada ya baba kurudi watoto walikauka.*

1. *Baada ya baba kurudi watoto walinyamaza.*

1. *Evaristo alikauka kama vile hamfahamu kabisa.*

1. *Evaristi alikaa kimya kama vile hamfahamu kabisa.*

2. *Mwanangu nimekaukiwa na mbumba.*

2. *Rafiki nimeishiwa na pesa.*

> 1. *kausha, uchuna, kula*

kausha v *puuza, jifanya kutosikia, nyamaza, tulia* be silly, play the ignorant fool, be quiet
Metaphorical extension of SS *kausha 'cause

to dry up'?

Kausha, bwana.

Usiseme, bwana.

Kausha, baba anakuja.

Nyamaza, baba anakuja.

Mama akikuuliza kitu, kausha tu, usiseme.

Mama akikuuliza kitu, nyamaza tu, usiseme.

Nilipomwuliza kuhusu jambo lile

alinikaushia.

Nilipomwuliza kuhusu jambo lile hakutaka

kusema.

> *uchuna, kauka, kula jiwe, mikausho*

kavu n/adj *hamna mpango, ovyo* no deal, chaotic

Metaphorical extension of SS *kavu 'dry'.

Reply to greetings such as *mambo vipi?

Mambo vipi? - Ah, kavu, bwana.

Mambo vipi? - Ah, hamna mpango, bwana.

Mambo yangu kavu kavu.

Mambo yangu ovyo.

kawoshi, kaoshi n *fulana bila mikono* sleeveless T-shirt

Transfer from SE 'carwash', based on the habit of men to wear sleeveless T-shirts when washing cars in order to avoid the clothes getting wet.

Nataka kwenda Kariakoo kununua kawoshi ya kuvaa jioni.

Nataka kwenda Kariakoo kununua fulana isiyo na mikono ya kuvaa jioni.

> *sing'lendi*

kaya n *bangi* Indian hemp, marijuana

Transfer from Jamaican Patois *kaya 'marijuana'.

Yule anavuta kaya.

Yule anavuta bangi.

> *blanti, ganja, jicho la tatu, kijiti, majani, mneli, ndumu, nyasi*

kaza v.caus 1. *bana* 2. *fanya juhudi* 2. *tomba, fanya mapenzi* 1. press 2. make an effort 3.

copulate, make love, have sex

Semantic extension of SS *kaza 'tighten'.

1. *Acha kunikazia.*

1. *Acha kunibania.*

2. *Timu pinza ilikaza sana.*

2. *Timu pinza ilicheza vizuri sana kwa kubana.*

3. *Jana nimetoka kumkaza Janet.*

3. *Jana nimetoka kufanya mapenzi na Janet.*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

3. *Ulimkazia demu wake.*
 3. Ulifanya mapenzi na demu wake.
 3. *Walikuwa wanakazana.*
 3. Walikuwa wanafanya mapenzi.
 > *bana, piga bao, piga nao, tia*
- kedekede** adj *maridadi, ya aina nyingi, kwa wingi* diverse, many
 < ?
Choo, bafu, simu, TV na vitu vingine kedekede.
 Choo, bafu, simu, TV na vitu vingine maridadi.
Walipika chakula kedekede.
 Walipika chakula nyingi.
- keroro** n 1. *pombe* 2. *hali ya kulewa sana* drunkenness
 Onomastic synecdoche, based on Keroro (from Gikuyu kirooro), the name of an alcoholic drink in Kenya.
 1. *Jana tulipiga keroro ya kufa mtu.*
 1. Jana tulikunywa pombe kupita kiasi.
 2. *Yuko keroro.*
 2. Amelewa sana.
 2. *Tulikuwa keroro kinoma.*
 2. Tulilewa kupita kiasi
- kerubi** n *kofi kubwa na la nguvu* hard slap on the face
 According to one informant transfer from Arab.
Alimpiga kerubi.
 Alimpiga kofi kubwa.
- kesha na vitabu** v *soma sana* study intensively
 Hyperbolic extension of SS *kesha 'stay awake all night' and *vitabu 'books'; expression; 'wake with books'.
Juma anakesha na vitabu.
 Juma anakesha kwa kusoma.
 > *bukua, chimba, Joni Kisomo*
- kiaina** adv 1. *kwa aina fulani* 2. *kwa siri, kisiri*
 1. certain, special 2. secretly
 Regular adverbial derivation from SS *aina 'kind', but probably used in a deviant way to talk in a veiled manner about a secret referent in the presence of others without giving away the secret.
 1. *Oya bloo, nigeo uchache kiaina.*
 1. Rafiki, unipe pesa kiasi fulani.

2. *Oya mshikaji, njoo nikupe dili kiaina hapa chobi.*
 2. We rafiki yangu, njoo nikueleze kitu fulani kwa siri hapa pembeni.
 2. *Nipe kiainaaina.*
 2. Nipe kisirisiri.
 > *aina aina*

kibao adv/adj *kwa wingi, -ingi* in abundance
 Metaphorical extension of class 7 derivation of *bao 'board'? Very common since long, but not attested in KKS2 with this meaning. Attested in older Swahili slang as 'beauty; fine record' (Ohly 1987a: 43).
Washikaji, chomokeni! Mamwela kibao wanakatiza maskani.
 Jamani, kimbieni! Mapolisi wengi wanapita nyumbani.
Kanifotoa mapicha kibao.
 Akanipiga picha nyingi.
 > *bwena*

kibendi n7 *mimba* pregnancy
 Metaphorical extension of SS *bendi ya shule 'schoolband': The big drum is held in front of the belly. Attested in older Swahili slang as *bendi ya wiki 'pregnant woman' (Ohly 1987a: 24).
Demu huyu ana kibendi.
 Msichana huyu ana mimba.

Kiberiti, kibiriti n7 *gari ndogo, simu ndogo* small car (e.g. Landrover with short chassis, Suzuki 404), small mobile phone
 Dysphemistic metaphorical extension of SS *kiberiti 'match-box'.
Kuna kiberiti kimoja ambacho kimepita.
 Kuna gari ndogo ambayo imepita.
 > *kipanya*

kibinda, kibinda nkoi n7 *tako kubwa* fat buttock
 Metonymic extension of refrain of a song from Kofi Olumide (DR Congo): kibinda kibinda kibinda - he, kibinda nkoy. The dance style to that song requires movements which emphasize the buttocks.
Huyu demu ana bongela la kibinda.
 Huyu msichana ana matako makubwa.
 > *bambataa, mkundu, ndombolo, shuzi, taarabu, tukunyema, wowowo*

kibongo n7 *lugha ya mitaani ya kisasa, lugha ya vijana* recent forms of colloquial and youth language

Derived from "Bongo", the nickname of Dar es Salaam, which is perceived as centre of linguistic creation.

Ah, sasa ameingia kibongo.

Ah, sasa ameanza kusema kibongo.

> *Bongo*

kibosile n7 *bosi, mtu mwenye pesa nyingi* boss, rich person

Probably derived from SE 'boss'.

Kibosile wetu amerudi.

Bosi wetu amerudi.

> *mdosi, mnene, pedeshee*

kibuti n7/8 *karatasi au kitabu cha kutumia katika mtihani kwa kuangalizia majibu bila ruhusa* notes and books used for cheating in exams

< ? Popular in schools and colleges.

Wanafunzi walifaulu kwa vibuti.

Wanafunzi walifaulu kwa kuchungulia majibu kwenye karatasi.

> *desa*

kichaa wangu n7/8 *address: rafiki yangu, hasa kati ya wanaume* address: my friend, esp. from man to man

Dysphemistic extension of SS *kichaa 'lunacy; crazy person'; expression 'my crazy one'.

Tuliza boli, kichaa wangu, mambo chelea pina.

Subiri, rafiki yangu, mambo mazuri sana.

> *mshikaji, mshirika, msela, mazee, mwana, mchizi*

kicheche n7 1. *mwanamume ambaye anafuata sana wanawake* 2. *msichana ambaye anajirahisisha* 1. womaniser 2. girl or woman who consents easily to a sexual proposal

Dysphemistic metaphorical transfer of name of a small carnivorous mammal which devours chicken. It is very cunning and manages to get into the chicken coop. Cf. *macheche attested in older Swahili slang for 'restless person; hooligan' (Ohly 1987a: 51).

1. *Yule bwana ni kicheche hatari.*

1. Yule bwana anafuata sana wanawake.

kicheni pati n.phr 1. *sherehe katika arusi wanaposhiriki wanawake tu* 2. *mkusanyiko wa wanawake wengi* 3. *gari aina ya Suzuki Vitara, au Suzuki RAV4 (magari ambayo mara nyingi huendeshwa na wanawake)* 4. *simu ya mkononi ndogo aina ya "Panasonic"*

1. a ceremony within the wedding celebrations where only women are admitted

2. a place where there are many women 3. car model "Suzuki Vitara", or Mitsubishi RVR (which are often driven by women) 4. small mobile phone "Panasonic"

Semantic extension of SE 'kitchen party', which forms part of the wedding ceremonies. At the kitchen party only women have access. Used to denote things mainly used by women, or events where a lot of women are present.

3. *Anna anaendesha kicheni pati siku hizi.*

3. *Anna anaendesha Suzuki RAV4 siku hizi.*

> 3. *mama koku*

kichizi adv *sana, mno* very much, exceedingly
Derivation from SS *chizi 'stupid person, crazy person'

Juma anaumwa kichizi.

Juma anaumwa sana.

kidampa n7 *kibarua, mpambe, mtumishi wa hali ya chini* day labourer, sb doing badly paid jobs

Derivation from SS *dampo 'dumping ground'.

Yule ni kidampa tu.

Yule mtu ni kibarua tu.

kidanka, danka disc *hali (yako)?* how is it?
< ? Used as a greeting. The reply is *chee.

Kidanka - chee.

Mambo vipi? - Safi.

kideo n7/8 *sinema, video, runinga* cinema, video, TV set

Morphological appropriation of SE 'video', and metonymic extension.

Yule mtu kavaa nguo kama kideo.

Yule mtu kavaa nguo ovyo ovyo.

Yule mlevi anacheza kideo.

Yule mtu anacheza kama katika video.

Unataka nije hapa kila siku kutafuta pesa zangu, unanifanya mimi kideo?

Unataka nije hapa kila siku kutafuta pesa zangu, unanifanya mimi kitu cha

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- kutazama?
> *piga deo*
- kidonda** n7 *saa* watch
Metaphorical extension of SS *kidonda 'wound'.
Oya, una kidonda kikali.
Oya, una saa safi sana.
> *jicho la mamba*
- kidosho** n7/8 *msichana mrembo* beautiful girl, young woman
< ? Attested in older Swahili slang (Reynolds 1962: 204).
Vidosho wa siku hizi bei mbaya.
Wasichana wa siku hizi ni ghali kuwapata.
> *mdosho*
- kidudu** n7/8 1. *kitu ambacho ni kidogo, kizuri ama kibaya* 2. *nguo ya kisasa* 1. little thing, nice or bad 2. fashion cloth
Semantic extension of diminutive derivation of SS *mdudu 'insect', motivation unclear.
Atakununulia vidudu chungu nzima.
Atakununulia vitu chungu nzima.
Kakununulia vidudu chungu nzima.
Kakununulia nguo nzuri za kisasa chungu nzima.
- kidudu mtu** n.phr *mtu mbaya, mtu anayetisha*
bad person, someone who is threatening
Semantic extension of diminutive of SS *mdudu 'insect plus SS *mtu 'person'.
- kiepe** n7/8 *kiazi* potato
< ?
Jana nimenunua viepe.
Jana nimenunua viazi.
> *viepe yai*
- kifaa** n7/8 *msichana mzuri kwa umbo na tabia*
beautiful and well-mannered girl
Metaphorical extension of SS *kifaa 'utensil'.
Mimi nina kifaa vile vile.
Mimi nina msichana vile vile.
> *chuma*
- kifaru** n7 *noti ya shilingi 5000 iliyotolewa 2003* note of 5000 TSh. issued in 2003
Metonymic extension of SS *kifaru 'rhinoceros', based on the picture of rhinos printed on the note. Not common.
- kifriza** n7 *kitambi* pot-belly
- < ? Probably metonymic extension of SE 'freezer', based on form.
Johani mambo yake sasa hivi ni mazuri, ameota kifriza.
Johani mambo yake sasa hivi ni mazuri, ameota kitambi.
- kigagula**
> *gagula*
- kigiza** n7 *kizuizi* obstacle
Metaphorical extension of SS *giza 'darkness'.
Ondoka unaniletea kigiza.
Ondoka unanisumbua.
> *kiwingu, bania, usiku*
- kihiyu** n7/8 *mtu anayejisikia, kumbe hamna kitu, mtu aliyegushi vyeti vya shule*, a person who is supposed to be an expert, but actually is not truly qualified; a person who has forged educational certificates
Onomastic synecdoche of the name of a minister, Kihiyu, who used forged certificates of higher education.
Vihiyu Bongoland wako kila mahali.
Walaghai Tanzania wako kila mahali.
Wewe huna kitu ni kihiyu tu.
Wewe huna kitu, umegushi tu vyeti vya shule.
- kijasti** n7 *nguo ndogo ya wanawake inayobana* short and tight dress for women
Abbreviation of 'just because' which is an ellipsis of 'just because to attract men'.
Demu ametilia kijasti cha nguvu.
Msichana amevaa kijasti cha gharama.
Alikula kijasti bomba.
Alivaa nguo ndogo na ya kubana nzuri sana.
- kijiti** n7 1. *msokoto wa bangi* 2. *daraja la kwanza katika shule ya sekondari* 1. joint (marijuana) 2. division one in results of examination at O- and A-level
Metonymic extension of SS *kijiti 'small stick', based on form.
2. *Ametundika kijiti.*
2. *Ametundika "division one"*.
> 1. *blant[i], ganja, mneli* 2. *vijiti viwili*
- kijiwe** n7/8 *mahali pa kukutania vijana / majobless* place where jobless youths meet
Metonymic extension of diminutive of SS *jiwe 'stone'. Stones are used to sit on.

- Or metaphoric extension of SS *jiwe 'stone', based on the property of being stationary and immovable.
Pale pana kijiwe changu .
 Pale pana mahali pangu pa kukutana na marafiki.
 > *joblesi kona, kijiweni, vijana wa vijiwani*
- kijiweni** n.loc *mahali pa kukutania vijana / majobless* corner or place where jobless youths meet
 Metonymic extension of locative of diminutive of SS *jiwe 'stone'. Stones are used to sit on, in other cases the youths sit on logs.
Vijana wanakutana kijiweni na kupiga stori.
Vijana wanakutana kijiweni na kuongea.
Oya, naenda kuegesha kijiweni.
Oya, naenda kukaa kijiweni.
 > *joblesi kona, kijiwe, vijana wa vijiwani*
- kikristu** n7 *Kiingereza* English language
 Metonymic extension of SS *kikristu 'Christian ways, Christian language'.
 Now in decline. Sometimes heard as *kikristo.
 > *kimombo, kizungu, ung'eng'e, BBC, tema ngeli*
- kikáladi** n7 *chotara ambaye wazazi wake ni wa rangi tofauti, hasa msichana* coloured person, esp. girl
 Derivation of transfer from SE 'coloured'.
Jana nimemkamatia mtoto wa kikáladi.
Jana nimempata msichana chotara.
 > *bambadi*
- kilaji** n7 *pombe*, alcoholic beverage, drink
 Metonymic extension of SS *kilaji 'food'.
Oya mshikaji, twenzetu kivulini tukapate kilaji.
 Rafiki yangu, twende pamoja bar tukapate vinywaji.
- kilauri** n7 *pombe* beer, alcoholic drink
 Metonymic extension of derivation of SS *bilauri 'drinking-glass, tumbler'.
Leo tumekata kilauri.
 Leo tumekunywa pombe.
 > *ulabu*
- kili** v *ua* kill
 Transfer from SE 'kill'.
Ipo dei nitakuja kukukili.
 Ipo siku nitakuja kukuua.
- kilo** n *shilingi 100000, laki moja* 100000 shillings
 Metaphorical extension of SE 'kilo', motivated by association of heavy weight with high value, probably also influenced by similarity to the metathesized form of SS *laki '100000'.
Kilo moja.
Laki moja.
Kilo mbili.
Laki mbili.
- kilongalonga** n7/8 *simu ya mkononi* mobile phone
 Metonymic extension of nominalisation of LyM *longa 'chat'.
Nahitaji kununua kilongalonga aina ya Nokia.
Nahitaji kununua simu ya mkononi aina ya Nokia.
 < *longa, foma limao, kiberiti*
- kiluzi** n7/8 *msichana ambaye ni rahisi kupata, msichana anayejirahisisha* girl who agrees easily to a proposal
 Diminutive of LyM "luzi".
Jioni itabidi nikipitie kiluzi changu.
Jioni itabidi nimpitie msichana wangu.
 > *luzi*
- kimeo** n7/8? 1. *kitu kibovu kibovu, kitu ambacho kimechokachoka* 2. *malaya* 1. sth broken, old, outworn 2. prostitute
 < ?. Common.
Simu yako ni kimeo.
Simu yako ni kitu kibovu.
Simu yako siku hizi kimeo.
Simu yako siku hizi ina matatizo.
 > *soo, msala, kizaazaa*
- kimini** n7/8 *sketi fupi sana* mini skirt
 Transfer from SE 'mini'.
Mary amevaa kimini.
 Mary amevaa sketi fupi sana.
- kimwana** n7/8 *msichana mzuri, binti mzuri* pretty girl
 Diminutive of SS *mwana 'child'
- kimóbitel** n7/8 1. *msichana mwembamba, msichana mzuri* 2. *umbo mdogo wa mtu* 1. slim lady, beautiful girl 2. small figure
 Metaphorical extension derived from the name of the mobile phone corporation

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

"Mobitel". Not pejorative.

1. *Yule ni kimóbitel.*

1. Yule ni msichana mwembamba.

> *figa, kipótabo, English figure*

kinaa n *tatizo, balaa* problem

Metaphorical extension of SS *kinaa 'satiety'.

Ee bwana, usituletee kinaa hapa.

Ee bwana, usituletee balaa hapa.

Hoya tusileteane kinaa hapa.

Hoya, tusileteane matatizo hapa.

> *shobo, noma*

kinabo n7/8 *mshamba* layman, country

bumpkin

< ?

Kinabo analeta soo!

Mshamba analeta aibu!

> *mporipori, wa kuja*

kinari n7 *kiberiti* match

Diminutive of SS *nari 'fire'. Not common.

king'asti n7 1. *msichana mrembo na*

mwembamba 2. *mchumba* 1. beautiful, slim girl 2. girlfriend, fiancée

Onomastic synecdoche based on the name of a girl in a song of Mr. Nice called King'asti; the chorus sings: King'asti I need u, I love u.

Huyu ni king'asti wangu.

Huyu ni mchumba wangu.

kinoma adv *sana, vizuri sana, kwa kupita*

kiasi very much, terribly

Adverbial derivation of LyM *noma 'trouble'.

Mshirika, leo n'na ubao kinoma, twenzetu kanigee dongo!

Rafiki, leo n'na njaa sana, twende ukanipe ugali!

Woch la nguvu kinoma.

Saa yenye nguvu kubwa.

Tulikumaindi kinoma.

Tulikuzoea sana.

Nina njaa kinoma.

Nina njaa vibaya sana.

> *kishenzi, kwa kwenda mbele, ya kufa mtu*

< *noma*

kinywaji n7/8 *pombe* alcoholic beverage

Euphemistic generalisation of SS *kinywaji 'drink'.

Twende tukapate kinywaji.

Twende tukapate pombe.

> *maji, tungi*

kioo n7 *video* video

Metonymic extension of SS *kioo 'mirror'; older Swahili slang has a different meaning 'a beauty' (Ohly 1987a: 45).

Njoo tucheki kioo.

Come and let's watch the video.

Wanaangalia kioo.

Wanaangalia filamu.

kipa v 1. *elekea* 2. *ondoka, toka* 1. move towards 2. make off

< ?

1. *Nakipa skonga.*

1. Naelekea shuleni.

2. *Kipa, bwana!*

2. Toka hapa, bwana!

> *anza, chomoa, ishia, jisanzua, jikata, timka, timua, toa kiwingu, yeya*

kipanya n7 *gari ndogo* small car

Dysphemistic metaphorical extension of diminutive of SS *panya 'mouse, rat'.

Nimepanda gari kipanya.

Nimepanda gari dogo.

Umekuja na gari gani? - "Kipanya Suzuki."

"Umekuja na gari gani?" - "Na Suzuki ndogo."

> *kiberiti*

kipepe n7 *mshamba* layman, country-bumpkin

Onomastic synecdoche of "Komredi Kipepe", a character in a popular cartoon who is a hunter.

Acha kuwa kipepe.

Acha kuwa mshamba.

> *kinabo, mporipori*

kipepsi n7 *kiwiko* elbow

Onomastic synecdoche of brand name

"Pepsi", based on similarity of form of elbow and bottle-neck.

kipimbi n7

> *pimbi*

kipodozi n7/8 *poda ya kujipodoa* cosmetics, make-up

Derived from SE 'powder' plus suffix -zi.

Uso wake ulikuwa wa mviringo usiohitaji kukolezwa kwa vipodozi vya aina yoyote.

Uso wake ulikuwa wa mviringo usiohitaji
kukolezwa kwa poda ya aina yoyote.

kipopo n7/8 *msichana ambaye hajaolewa*
unmarried girl, lady

Metaphorical extension of SS *popo 'bat',
probably related to older Swahili slang
*limpopo 'a beauty' (Ohly 1987a: 50).
Etymology provided by a female
informant: the unmarried girl has not yet
settled; just like a bat, she always
changes her ways and friends. Not
common.

> *demu, desa*

kipótabo n7/8 *msichana mwembamba,*
msichana mzuri, umbo mdogo wa mtu lady,
beautiful lady

Metaphorical extension of SE 'portable'.
Yule ni kipótabo.

Yule ni *msichana mwembamba.*

> *English figure, figa, kimóbitel*

kiroba n7/8 1. *mfuko wa unga, sukari,*
konyagi, maji 2. *abiria wasiolipa nauli* 3.
mtu asiye na umbo mzuri 1. packet of flour,
sugar, "Konyagi", or water 2. passenger who
gets a free lift 3. person being in bad shape
Truncation and semantic narrowing of

derivation of SS *robota 'packet, parcel'.

Further metaphoric transfer to derive
second meaning is motivated by the
parallel that luggage is not usually
charged for a fare. Common and old.

1. *Nipatie maji ya kiroba.*

1. Nipatie maji katika mfuko wa plastiki.

2. *Gari imejaa viroba tu.*

2. Gari limejaa abiria wasiolipa nauli tu.

> *totopaki, sanamu ya michelini, jeruhi, maiti*

kirukanjia n7/8 *msichana asiyetulia, malaya,*
mtu anayejitembeza prostitute, sb who has
not yet settled down

Metaphorical extension of SS *kirukanjia
'nightjar; restless person'.

Mwanamke yule ni mzuri lakini kirukanjia.

Mwanamke yule ni mzuri lakini hajatulia.

kishalishali adv

> *shali*

kishenzi adv *sana, vizuri sana* very much,
terribly

Adverbial derivation of LyM *mshenzi

'primitive person'.

Tulikula blanti kishenzi.

Tulivuta bangi kupita kiasi.

> *kichizi, kinoma, kwa kwenda mbele, ya kufa*
mtu

kishtobe n7 1. *rafiki wa kike, mpenzi* 2.
mwanamke mwenye matako, kuku mwenye
matako 1. girlfriend 2. woman with big
behind, chicken with big behind

According to Blommaert (2003: 18) this
term is derived from the name of a big
Greek cargo vessel. Now in decline.

1. *Yule ni kishtobe wangu.*

1. Yule ni mpenzi wangu.

2. *Ah, kuku huyu ana kishtobe.*

2. Ah, kuku huyu ana matako makubwa.

kishua adj *enye uhakika, zuri, safi* sure, nice
Derivation of transfer from SE 'sure'. Also
attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga
2003: 14).

Mambo yake ya kishua.

Mambo yake yana uhakika.

> *mshua*

kisu n *fedha, pesa; hasa fedha za noti* money,
paper money

Semantic extension of SS *kisu 'knife',
motivation unclear. In older Swahili
slang attested with the meaning 'sharp
tongue, strong terms' (Ohly 1987a: 46).

Sina kisu.

Sina pesa.

Kiswenglish n7 *lugha ya mitaani ambayo*
inatulia maneno mengi ya Kiingereza style
of non-standard language with many English
elements

Code mixing of SS *Kiswahili 'Swahili' plus
SE English'. Coinage to denote a code
which is basically Swahili with
incorporation of English elements.

Hii sasa ni Kiswenglish.

kitambi n7 *division "D" katika matokeo ya*
mitihani division "D" in school results

Metonymic extension of SS *kitambi 'belly'
based on form: the silhouette of a person
with big belly resembles the shape of
"D".

kitaani n.loc *nyumbani, maskani* at home
Metonymic extension and diminutive of SS

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

*mtaani 'on the street', 'in the living quarter'

Najitia kitaani.

Naingia nyumbani.

kitimoto n.phr 1. *nyama ya nguruwe (ya kuchoma)* 2. *kiti cha kumkalisha mtu kwa mahojiano makali* 3. *kikao* 1. (grilled) porc meat 2. a seat where one is questioned, "hot seat" 3. meeting

Metonymic extension of compound of SS

*kiti 'chair' and *moto 'heat, fire', meaning "hot seat". The metonymy is based on a television debate programme "kiti moto" on the independent channel DTV, where people like politicians were questioned. They had to sit on the "hot seat". Cognitive motivation: one explanation says that one time in the TV programme the topic was the sale of porc meat in butcheries. A second one maintains that some Muslims do not stick very seriously to the prohibition of porc meat. So when they eat it they feel like sitting on a "hot seat". Common.

1. *Siku hiyo kila mtu alipika kitimoto.*

1. Siku hiyo kila mtu alipika nyama ya nguruwe.

1. *Sili kitimoto.*

1. Sili nyama ya nguruwe.

2. *Aliwekwa kitimoto.*

2. Alihojiwa kikali.

3. *Tuko kwenye kitimoto.*

3. Tuko kwenye kikao.

> *mkuu wa meza*

kitobo n7 *msichana au mwanamke anayependa kufanya mapenzi na wanaume tofauti* girl or woman who likes to have various lovers.

Metonymic extension of SS *kitobo 'small hole'. Pejorative.

Asha ni kitobo.

Asha anapenda kufanya mapenzi na wanaume wengi.

kitombi n7 *mtu anayependa kufanya mapenzi na wanawake tofauti* man who has various lovers

Derived from SS *tomba 'copulate'.

Yule ni kitombi tu.

Yule anafanya mapenzi na wanawake wengi

tu.

kitopu n7/8 *blauzi ndogo ya kike isiyofika kiunoni.* short and small top
Transfer from SE 'top'.
Mary amevaa kitopu.
Mary amevaa blauzi ndogo isiyofika kiunoni.

kitu kidogo n.phr *rushwa, hongo* bribe
Euphemistic extension of SS *kitu kidogo 'something little'. Imported into LyM from Kenya. Old and common.

Kitu kidogo kinasababisha huduma duni za jamii.

Bribes cause an abject state of society.

Lete kitu kidogo.

Naomba hela kwanza.

Toa kitu kidogo!

Naomba hela.

TKK.

Kifupisho cha "toa kitu kidogo".

> *chai*

kivulini n *baa bar*

Metonymic extension of SS *kivulini 'in the shadow'; in older Swahili slang attested as *kivuli 'sun-umbrella, parasol' (Ohly 1987a: 46).

Oya mshikaji, twenzetu kivulini tukapate kilaji.

Rafiki yangu, twende pamoja bar tukapate vinywaji.

kiwanja n7 1. *eneo la starehe (baa, night club)* 2. *ulaya, nchi ya nje* 1. place to relax 2. foreign country (not common)

Metonymic extension of SS *kiwanja 'place of ground'.

1. *Twende zetu viwanja.*

1. Twende zetu kustarehe.

> *debe, kwanja*

kiwingu n7/8 *kizuizi* obstacle

Metaphoric extension of SS *kiwingu 'small cloud'.

Mbona unaniwekea kiwingu.

Mbona unaniwekea kizuizi.

Ondoka unaniletea kiwingu.

Ondoka unanisumbua.

Ondoa kiwingu chako.

Ondoka hapa.

Toa kiwingu.

- Fanya shughuli zako!
> *bania, gozigozi, kigiza, mchongoma*
- kiyoyozi** n7/8 *mashine inayopoza hewa* air condition
< ?. In KKS 2.
Tuna vipasha joto katika majira ya baridi na kutumia kiyoyozi katika majira ya joto.
We have heaters in the cold season and use air condition in the hot season.
> *full kipupwe*
- kizaazaa** n7 *kasheshe inayomfikia mtu mwenyewe, balaa, hali ya kutokuwa na utulivu* trouble, grief, calamity, misfortune
Semantic extension of derivation from SS *zaa 'give birth?'; in older Swahili slang attested as 'confusion' (Ohly 1987a: 46). In KKS 1 and 2.
Jamaa kaniletea kizaazaa.
Jamaa kaniletea vurugu.
Kizaazaa gani kimenikuta.
Bala gani imenikuta.
Kizaazaa kimeingia.
Bala imeingia.
> *soo, kimeo, msala*
- kizungu** n7 *Kiingereza* English language
Metonymic extension of SS *kizungu 'European ways, European language'.
Old and common.
Wanazungumza kizungu.
Wanazungumza Kiingereza.
> *kimombo, kikristu, ung'eng'e, BBC*
- klintoni** v 1. *baka* 2. *piga* 1. rape 2. beat up
Onomastic synecdoche of the name of Bill Clinton, former president of the USA, representing an icon of power.
Angalia asikuklintoni.
Angalia asikubake.
Nitakuklintoni.
Nitakupiga.
> *timori, kosovo, pasua mangumi ya jela*
- kolboksi** n *mwanamke aliyeolewa na anatembea nje ya ndoa* married woman who has lovers
Metonymic extension of SE 'callbox'.
Asha ni kolboksi.
Asha antembea na wanaume nje ya ndoa yake.
> *kirukanjia*

- kombati** n *nguo yenye michoro mingi, suruali yenye mifuko ya nje* cloth with camouflage design, cargo trousers
Metonymic extension from SE 'combat', motivated by the camouflage design. The word also appears as *kombati in written form. Before *batiki became more prestigious, these clothes were also called *mawingu.
Yule broo kawamba bongela kombati.
Yule kaka kavaa vest nzuri.
- konda** n5/6 *kondakta* conductor
Terminal clipping of SS *kondakta 'conductor'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 15).
Konda naomba unirusishie chenji yangu.
Kondakta naomba unirusishie chenji yangu.
- konda** v *jali* take sth serious
Metonymic extension of SS *konda 'become emaciated'.
Usikonde.
Usijali.
Ninakukonda wewe.
Nina wasiwasi na wewe.
- kong'oli** v 1. *gonga, piga, angalia* 2. *fanya tendo la ndoa* 1. click, beat, look at 2. have sexual intercourse
< ?
1. *Usinichezee nitakukong'oli.*
1. Usinichezee nitakupiga.
1. *Kong'oli hapa.*
1. Click here.
2. *Usimaindi kukong'oli mademu.*
2. Usipende kufanya mapenzi na wasichana.
- kong'ota** v *piga sana, piga kwa fimbo* beat up, beat severely, beat with a stick
Metonymic extension of SS *kong'ota 'beat sth in order to flatten it'. Also in Kihore (2004: 9). In Sheng as *ng'ota (Mbaabu & Nzuga 2003: 24).
Polisi amenikong'ota kinoma.
Polisi alinipiga vibaya sana.
- koromea** v *karipia, fokea* scold
Dysphemistic metonymic extension of SS *koroma 'snore'.
Bosi ananikoromea sana.
Bosi ananifokea sana

kosovo v.phr *piga* beat up

Onomastic synecdoche of the geographical term Kosovo which became emblematic as an area of conflict, combat and war in 1999/2000 during the Kosovo crisis.

Nitakukosovo.

Nitakupiga.

> *klintoni, timori*

kosovo n9/10 *ugomvi, kupambana* trouble, quarrel, fight

Onomastic synecdoche of the geographical term Kosovo which became emblematic as an area of conflict, combat and war in 1999/2000 during the Kosovo crisis.

Nitakuanzishia kosovo.

Nitakuanzishia ugomvi.

Kule kulikuwa na kosovo.

Kule kulikuwa na ugomvi.

Mtu atakuja kuleta kosovo nyumbani kwako.

Mtu atakuja kuleta ugomvi nyumbani kwako.

> *klintoni, timori*

kota n10 *sehemu ya nyumba wanapokaa watumishi* quarters of civil servants or personnel of a certain company

Transfer from SE 'quarter'.

Alielekea kota za serikali.

Alielekea nyumba za watumishi wa serikali.

Anaishi katika kota za shirika.

kula blanti v.phr *vuta bangi* smoke marijuana

Semantic extension of SS *kula 'eat' plus transfer from E 'blunt', which see; expression "eat marijuana".

Masela wameingia kati kula blanti.

Marafiki wameenda nyumbani kuvuta bangi.

> *kula nyasi*

kula bunda v.phr *ondoka, kimbia* go away, run away

Metaphorical extension of SS *kula 'eat' plus SS *bunda 'a heap of things'; expression "eat the heap".

Amekula bunda.

Amekimbia.

Kula bunda, bwana.

Toka hapa, bwana.

> *anza, chomoa, ishia, jiachia, jikata, jisanzua, kipa, lala mbele, piga bunda, tambaa, timka, timua, toa kiwingu, yeya*

kula chabo v.phr *chungulia vitu visivyomhusu mtu, chungulia dirishani, peleleza mtu,*

kuwaangalia watu kwa kificho peep, spy

Semantic extension of SS *kula 'eat'; origin of *chabo unclear.

Kula chabo!

Angalia!

Juma anapenda kula chabo madirishani kwa mwenzie.

Juma anapenda kuchungulia madirishani kwa mwenzie.

> *piga deo, piga tochi, kula chasi*

kula chasi v.phr *chungulia vitu visivyomhusu mtu, chungulia dirishani, peleleza mtu,*

kuwaangalia watu kwa kificho peep, spy

Semantic extension of SS *kula 'eat'; origin of *chasi unclear.

Amekula chasi.

Amewaangalia watu kwa kificho.

Acha kula chasi!

Acha kuangalia watu kwa kificho!

> *piga chasi, piga deo, piga tochi, kula chabo*

kula jiwe v.phr *puuza kwa kujikaza sana, jifanya kutosikia, nyamaza, tulia* force os to keep quiet, play the ignorant fool

Metaphorical extension of SS *kula 'eat' and *jiwe 'stone'; expression 'eat a stone'. The emotions which have to be suppressed are compared to a stone.

Amekula jiwe.

Amejikaza kunyamaza.

> *kauka, kausha, uchuna*

kula kona v.phr *kimbia, ondoka* run away, go away

Metaphorical extension of SS *kula 'eat' plus SE 'corner'; expression "eat the corner".

Amekula kona.

Amekimbia.

Kula kona, bwana.

Toka hapa, bwana.

> *anza, chomoa, ishia, jikata, jisanzua, kipa, lala mbele, timka, timua, toa kiwingu, yeya*

kula kwa macho v.phr *ishia kuona tu bila kula chakula chenyewe, angalia kitu bila uwezo wa kukipata* see nice food without being allowed to eat, see sth without being able to obtain it

Metaphorical extension of SS *kula 'eat' plus

SS *macho 'eyes', probably inspired by a

calque? Expression "eat with the eyes".
Common, colloquial.

Utakula kwa macho.

Utaona kitu bila kuweza kukipata.

kula mande n.phr *fanya ngono wanaume wengi na mwanamke mmoja kwa wakati mmoja, fanya ngono ya kuchangia* group sex, group rape: a number of men with one woman

< ? In older Swahili slang *tia mande 'sleep with a woman' (Ohly 1987a: 76).

Zaituni aliliwa mande.

Zaituni alifanyiwa ngono na wanaume wengi kwa wakati mmoja.

> *mtungo*

kula ngozi v.phr *fanya mapenzi na msichana* sleep with a girl, make love with a girl
Metaphorical expression "eat the skin"; SS *kula 'eat' plus SS *ngozi 'skin, hide'
Mcheke mshikaji, anakula ngozi.
Mwone rafiki yule, anafanya mapenzi na msichana.

> *gonga ngozi*

kula nguo v.phr *vaa nguo* wear clothes
Metaphorical extension of SS *kula 'eat' plus SS *nguo 'clothes'; expression "eat clothes".

Juma alikula nguo kinoma.

Juma alivaa nguo safi sana.

> *pigilia nguo*

kula nyasi v.phr *vuta bangi* smoke marijuana
Metaphorical extension of SS *kula 'eat' and *nyasi 'grass'; expression "eat grass".

Tulikula nyasi mpaka basi.

Tulivuta bangi mpaka tumetosheka.

kula pamba v.phr *vaa nguo nzuri* be nicely dressed
Metaphorical extension of SS *kula 'eat' and *pamba 'cotton'; expression "eat cotton".

Declare amekula pamba kali / ya nguvu / kwa kwenda mbele.

Declare amevaa nguo nzuri sana.

kula shaba v.phr 1. *pigwa risasi* 2. *kutosema*
1. get shot 2. not tell sth
Metaphorical extension of SS *kula 'eat' and *shaba 'copper'; expression "eat copper".

1. *Amekula shaba.*

1. Amepigwa risasi.

2. *Kula shaba, bwana.*

2. Usiseme, bwana.

kula suruali v.phr *vaa suruali* wear trousers
Semantic extension of SS *kula 'eat' plus SS *suruali 'trousers'; expression 'eat trousers'.

Masela walikula suruali za mdebwezo.

Marafiki walivaa suruali za mlegezo.

kula ugali / wali kwa saiti mira v.phr *kula ugali/wali kwa nyama au samaki bila mchuzi* eat ugali with meat or fish without sauce
Metaphorical extension of SE 'side mirror', based on the similarity in form between a side mirror of a car and a person holding a piece of meat or fish in his left hand; expression "eat ugali in the side-mirror manner".

Nakula ugali kwa saiti mira.

Nakula ugali na nyama/samaki bila mchuzi.

> *lumangia*

kula uroda v.phr *fanya mapenzi* make love, have sex
Semantic extension of SS *kula 'eat' plus SS *uroda 'sexual intercourse' which might have been derived from a word for rocking or swinging, since according to one informant a child who has played a game of rocking or swinging might say: "nimekula uroda".

Wasichana wa siku hizi wanafanya uroda waziwazi.

Wasichana wa siku hizi wanafanya mapenzi waziwazi.

Twenzetu tukale uroda.

Twende zetu tufanye mapenzi.

> *uroda*

kula vichwa v.phr 1. *pata abiria au wateja katika sehemu kama: daladala, saloni, piga picha za passport* 2. *nyoa nywele* 1. get customers in: bus, hair saloon, passport photo studio 2. shave hair
Metaphorical extension of SS *kula 'eat' plus a synecdochical extension of SS *vichwa 'heads'; expression "eat heads". In business it is heads of customers what counts. Thus a daladala driver might say to the conductor *kula vichwa as a request to collect the fare.

1. *Suka alikula vichwa stendi.*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

1. Dereva alichukua abiria kwenye kituo.
 2. *Juzi nilimdakisha mkwanja akaniletee mashine za kulia vichwa.*
 2. Juzi nilimpa pesa akaniletee mashine za kunyolea nywele
Probably transfer from local language *mlume 'man' plus SS *ndago 'kind of weed which resists weeding'
Washikaji wa TMK ni walume ndago.
Watu wa TMK (group of Bongo Fleva artists) ni wanaume shupavu sana.
- mlupo** n^{3/4} *mwanamke ambaye ni rahisi kumpata, malaya* woman easily laid, floozy
< ?
Jana klabu kulikuwa na milupo mingi sana.
Jana klabu kulikuwa na wasichana wengi sana wanaopatikana kirahisi.

mnazi n3 *pombe ya kienyeji aina ya tembo*
locally brewed palm wine
Metonymic extension of SS *mnazi 'coconut
palm'.
> *chang'aa, mataputapu, tungi, ulabu*

mneli n3 *bangi; sigara; msokoto* joint of
marijuana; self-rolled cigarette
Metonymic extension of transfer from SE
'nail', based on form.
Zungusha mneli huo.
Zungusha sigara/bangi, tushirikiane kuvuta.
> *blant[i], ganja, kijiti, majani, ndumu, nyasi*

mnene n1/2 *bosi, mtu mwenye hela* boss,
person having money
Metonymic extension of derivation of SS
*nene 'fat, stout', related to older Swahili
slang *nenepa 'be comforted, be relieved'
(Ohly 1987a: 62).
> *mdosi, kibosile, pedeshee*

mnoknok n1/2 *mbeya* gossip
Derivation of LyM *mnoko
Achana na wanoknok, nia yao ni kuvuruga.
Usiwasikilize wambeya, nia yao ni
kutugombanisha..
> *mkuda, mnoko*

mnoko n1/2 1. *mwadilifu, mnaifiki* 2. *mbeya* 1.
someone 'too' strict 2. gossip
Derivation of SS *noa 'sharpen, whet';
related to *nokoa 'the second man in
authority over a plantation?'
*Amekuwa mwalimu wa nidhamu kutokana na
kuwa mnoko.*
*Amekuwa mwalimu wa nidhamu kutokana
na kuwa mwadilifu.*
Yule ni mnoko kama nini.
*Yule ni mkorofi kama nini. Anachonganisha
habari.*
> *mkuda, mnoknok*

mnuso n3 *chakula cha bure (k.v. kwenye
mazishi, matanga, arusi)* free meal
Metonymic extension of SS *nusa 'smell'.

mnyama n1 *kitu kizuri* something nice
Metaphorical extension of SS *mnyama
'animal'.
Hoya, washikaji, mshapata mnyama?
Hoya, marafiki, mmeshapata vitu vizuri?

mnyamwezi n1/2 *mmarekani mwenye asili ya*

kiafrika Afro-American
Metonymic extension of SS *mnyamwezi
'Nyamwezi'. Both, the Nyamwezi as well
as Afro-Americans are perceived as
being strong and big and as having
money.

Mcheki mnyamwezi yule.
*Mwone Mmarekani mwenye asili ya kiafrika
yule.*

mnyela n1 *mjinga, bwege* henpecked man,
fool
< ?
Rafiki yangu usiwe mnyela.
Rafiki yangu usiwe mjinga.
Wewe ni mnyela tu kwetu.
Wewe ni bwege tu kwetu.
> *boka, mbwiga, mgoroko, ndula, poyoyo*

motoa v *ondoka kwa gari au ndege* depart
with motor-vehicle
Probably metonymic extension of SE 'motor'.
Rare.
Dr. Gwassa day fulani kamotoa na mtutu.
Dr. Gwassa siku fulani kaondoka na pikipiki.
*Walami baada ya kupoa hapa Kurio
watomotoa na pipa.*
*Wazungu baada ya kukaa hapa Kurio
wataondoka na ndege.*

mpayuko n3 *suruali kutoka ulaya*
inayopayuka bleached jeans
Metonymic extension of *payuka 'bleach,
fade'.
> *jinsi*

mporipori n *mshamba* layman, country
bumpkin
Metonymic extension based on SS *pori
'bush'.
> *kinabo, mbushi, mlugaluga, wa kuja, yeboyeyo*

mpunga n3 *wali* cooked rice
Synecdoche from SS *mpunga 'rice plant,
non-husked rice'.
Leo tumekula mpunga.
Leo tumekula wali.
> *beche, ubwabwa*

mrama adv *vibaya* badly
Metaphorical extension of SS *mrama
'askew, off-course (of vessel)'. Old and
common.
Ukiona mambo yanaenda mrama mpelekee

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- barua hii kaka yangu.*
Ukiona mambo yanaanza kuwa mabaya
mpelekee barua hii kaka yangu.
- msaada, misaada** n3/4 *ukimwi* AIDS
Translation of acronym SE 'AIDS' in SS
*msaada. This term seems to be used by
academics only.
Ampata msaada.
Ampata ukimwi.
> *feruzi, mdudu, miwaya, ngoma, ngwengwe,*
nyola
- msagaji** n1/2 *mwanamke ambaye anafanya*
mapenzi na mwanamke mwenzake lesbian
Semantic extension of SS *saga 'grind'? Also
in KKS 2.
- msala** n3/4 *matatizo* trouble, something
problematic, shit
Dysphemistic metaphorical extension of SS
*msala 'toilette'.
Msala kishenzi kwao kama akigundulika.
Matatizo kupita kiasi kwao kama
akigundulika.
> *kasheshe, kimeo, kizaazaa, noma, sheshe, soo,*
zali
- msanii** n1/2 1. *mtu ambaye anaishi kwa*
mipango midogo midogo 2. *tapeli* 3.
mwimbaji wa Bongo Fleva 1. person living
on small deals 2. swindler
Euphemistic metonymic extension of SS
*msanii 'artist'.
2. *Juma ni msanii.*
2. Juma ni tapeli.
3. *Mimi msanii kioo cha jamii.*
3. Mimi ni mwimbaji wa *Bongo Fleva*, kioo
cha jamii.
- msela** n1/2/6 *mhuni, mtu ambaye hana mke;*
hata kwa mwanamke mhuni wild youth,
bachelor, also exceptionally used for women
Metonymic extension of SE 'sailor'; or
metonymic extension of SS *msela
'bachelor'? Raab (2004b: 10) states that
the word originates in English 'sailor':
"In the elders' Swahili a "msela" is a
bachelor, but in street slang a "msela" is
more like a teenager who's still got a
wild youthful energy." This suggests the
following semantic development: 'sailor'
> 'bachelor' > 'wild and untamed youth'.

- The last meaning is also reflected in
older Swahili slang *sela 'hooligan'
(Ohly 1987a: 72). The plural varies
between wasela (2) and masela (6). Used
as address between male youths.
Vipi msela wangu?
Vipi rafiki yangu?
- msenge** n1/2 *shoga, mwanamume ambaye*
anafanya mapenzi na wanaume wenzake
homosexual man (who receives penetration)
< ? Attested in older Swahili slang as *senge
'(1) lazy fellow; (2) nancy, queen,
somebody sodomised' (Ohly 1987a: 72).
In KKS 2.
Mwizi yule ni msenge, badala ya kuiba gari
anaiba embe.
Mwizi yule ni mzembe, badala ya kuiba gari
anaiba embe.
- mshakunaku** n1/2 *mbea* gossip
< ?
Yule ni mshakunaku kweli.
Yule ni mbea kweli.
- mshika pembe** n.phr *mwanamume asiye na*
uhusiano wa kimapenzi na msichana lakini
anasema kuwa ana uhusiano naye sb who
pretends to have a girlfriend
Metaphorical extension of SS *shika pembe
'hold horns'.
Daudi ni mshika pembe.
Daudi anumia wakati na mademu wasio wa
kwake.
< *shika pembe, nawa*
- mshikaji** n1 1. *rafiki (mwanamume na hata*
mwanamke) 2. *mpenzi* 1. close friend,
homeboy, female friend 2. girlfriend
Semantic extension of derivation of SS
*shika 'hold'.
Oya mshikaji, njoo nikupe dili kiaina hapa
chobi.
We rafiki yangu, njoo nikueleze siri kuhusu
kitu fulani hapa pembeni.
Oya mshikaji, tuliza mapepe, usiwe na
mzuka!
Rafiki, tuliza haraka, usiwe na wasiwasi!
mambo vipi, washikaji?
Habari gani, marafiki?
Mnacheke, washikaji, wakati nasevu
mapaparazi wakanifotoa picha.
Mnaona, marafiki, wakati nilipotoroka,

waandishi wa habari wakanipiga picha.
Sasa, washikaji, mnanitonya vipi kuhusu dili hili?
 Sasa, marafiki, mnanieleza vipi kuhusu jambo hili?
Oya mshikaji, twenzetu kivulini tukapate kilaji.
 Rafiki yangu, twende pamoja bar tukapate vinywaji.
 > *mshirika, kichaa, masela*

mshikaki n3 1. *fanya kitu kwa pamoja* 2. *fanya mapenzi na mwanamke mmoja kwa wanaume wengi wakati mmoja* 1. doing sth together 2. group sex, group rape
 Metonymic (1) or dysphemistic metaphorical extension (2) of SS *mshikaki 'piece of meat roasted on a skewer'.
 1. *Tulikula mshikaki jana.*
 1. *Tulikula chakula kwa pamoja jana.*
 > *mtungo*

mshiko n *fedha, pesa* money
 Metonymic extension based on SS *shika 'hold, grab'.
Nina mshiko mwingi.
Nina pesa nyingi.
 > *mapene, mkwanja, uchache*

mshindi n3/4 *simu kubwa ya mkononi* big-sized cell phone
 Onomastic synecdoche of brand name *mshindi 'winner' for a bar soap.
Eh! Nora ana bongwe la mshindi!
Eh! Nora ana simu ya mkononi kubwa sana!
 > *foma limau, mche wa sabuni*

mshirika n1/2 *rafiki wa karibu, jamaa* close friend
 Metonymic extension of *mshirika 'partner, participator' or SS *shirika 'partnership'.
Washirika, tuishie, mapaparazi watatuchukua foto.
Jamani, tuondoke, waandishi wa habari watatupiga picha.
Mshirika, leo na ubao kinoma, twenzetu kanigei dongo!
Rafiki, leo na njaa sana, twende ukanipe ugali!
Ms[h]irika, ipo dei tutawamba masuru ya jeans.
Rafiki, ipo siku tutavaa suruali za jinsi.
 > *mshikaji, kichaa, masela, mazeli*

mshua n *baba; rafiki* father, friend
 Derivation of transfer from SE 'sure'.
We unaenda kuchoma kwa mshua.
Wewe unakwenda kusema kwa baba.
Dingi wangu ni mshua.
Baba yangu ni mwelewa.
 > *dingi*

mshumaa n3/4 *msenge, shoga* gay man, homosexual man
 Semantic extension of SS *mshumaa 'candle'.
Yule ni mshumaa.
Yule ni shoga.
 > *anti, bwabwa, chakula, choko, kaka poa*

msonge n3/4 *daraja la "A" katika mtihani wa shule* division "A" in school exams
 Metonymic semantic extension of SS *msonge 'circular house', cognitive motivation based on its shape which resembles a triangle.
Rose amefanya vizuri kwenye mtihani, amepata msonge.
Rose amefanya vizuri kwenye mtihani, amepata daraja la A.

msosi n *chakula* food
 Synecdochic extension based on SE 'sauce'.
 Very common.

msuba n *bangi* Indian hemp, marijuana; opium
 < ?
 > *ganja, kaya, kijiti, majani, mjani, ndumu, nyasi*

mtambo n3 1. *taahira, zezeta, mtu aliyezubaa* 2. *msichana asiye na aibu yo yote, anayefanya kila kitu bila aibu* 1. mad person, lunatic 2. shameless girl
 Semantic extension of SS *mtambo 'big engine, mashine, mechanism, motor'; attested in older Swahili slang with the meaning 'woman, girl' (Ohly 1987a: 58), cf. also *mitambo for 'vagina' (Ohly 1987a: 56).
 1. *Wewe ni mtambo nini?*
 1. *Wewe ni taahira nini?*
 2. *Yule ni mtambo.*
 2. *Yule msichana hana aibu yo yote.*
 > *some-time-yes-some-time-no*

mtanashati n *mtu mwenye hali nzuri ya maisha, mtu mtimilifu* well-off person

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Metonymic extension of SS 'well-dressed person'.

mtandao n 1. *interneti, mobitel, kitu cha mawasiliano, simu ya mkononi* 2. ukimwi 1. network, internet, mobile phone net, mobile phone 2. AIDS

Metaphoric extension based on *tandaa 'be spread out over a large area (i.e. a plain)'.

1. *Dr. Günther alipiga mtandao kwa Padre Celestino.*

1. Dr. Günther telephoned Padre Celestine by mobile phone.

1. *Shadafa ana mtandao.*

1. Shadafa ana simu ya mkononi.

1. *Naona shosti, siku hizi una mtandao.*

1. Naona rafiki, siku hizi una simu ya mkononi.

2. *Mtandao unamaliza watu.*

2. Ukimwi unaua watu.

mtasha

> *mtishi*

mtashi

> *mtishi*

mtemba n 1. *ndege ya jeshi* 2. *meli kubwa ambazo mabaharia walitumia kuzamia na kwenda nazo Ulaya* 1. airforce plane 2. big ship which was used by sailors to reach Europe illegally

Metonymic extension of SS *mtemba 'pipe (for tobacco); funnel'.

2. *Washikaji walikula mtemba na kuishia zao ughaibuni.*

2. Marafiki walipanda meli na kuzamia Ulaya.

> *debe, pipa*

mtemba temka (TMK) n.phr *bangi* Indian hemp, marijuana

Onomastic synecdoche based on the name of the *Bongo Fleva* musician Mtemba from the group TMK, who is said to smoke marijuana heavily.

> *ganja, jicho la tatu, kaya, kijiti, majani, mneli, ndumu, nyasi*

mti n3/4 *mboo* erect penis

Metaphoric extension of SS *mti 'tree', also attested in older Swahili slang with meaning 'big penis' (Ohly 1987a: 58)

Akaenda kumpiga mti msichana.

Akaenda kufanya mapenzi na msichana.

mtibwa n 1. *sukari* 2. *zuri, tamu* 1. sugar 2. sth good, sweet, fine

Onomastic synecdoche based on the name of a sugar cane variety which owes its name to "Mtibwa Sugar Estate", a plantation and factory near Morogoro where this variety was produced. Mtibwa Sugar Estate was handed over to Tanzania Sugar Industries (TSI) in August, 1998 (after TSI had bought the company). Prior to this, the Government of the United Republic of Tanzania owned it. Cognitive motivation for 2.: sweetness.

1. *Nipatie mtibwa.*

1. Nipatie sukari.

2. *Mambo yako mtibwa.*

2. Mambo yako mazuri.

> *supa, mambo ya isidingo*

mtindi n3 *maziwa makubwa* big breasts

Dysphemistic metonymic extension of SS *mtindi 'sourmilk'.

Amemshika mtindi.

Amemshika maziwa.

Ah, yule mwanamke ni mzuri lakini ana bongela mtindi.

Ah, yule mwanamke ni mzuri lakini ana maziwa makubwa.

> *balungi, tikitimaji, nido, nyonyo*

mtishi n1/2 1. *mzungu* 2. *mtu mwenye tabia za kizungu* 1. European 2. person behaving as a European

Initial truncation of transfer from SE 'British' plus class-1-prefix m-; there are also the variants *mtashi and *mtasha which seem to be derived by internal vowel change.

Mtishi amefika.

Mzungu amefika.

Mambo yake ya kitishi.

Mambo yake ya kizungu.

mtoto shoo n.phr *mtu mwenye umbo wa kuvutia, mrembo* good-looking person, attractive person

Metonymic extension of transfer from SE 'show', attested in older Swahili slang with the meaning 'desirable woman, pretty girl' (Ohly 1987a: 58).

Watoto shoo, mama yake angeliwaita.

- Watoto wenye umbo wa kuvutia, mama yake angeliwaita.
- mtoto wa geti kali, mtoto wa geti** n.phr
msichana ambaye kwao analindwa sana, msichana anayefungiwa ndani girl that is being guarded strictly by her parents, girl whose parents are very strict
Metonymic extension of SS *kali 'fierce' plus transfer from SE 'gate', popularised by the song "Mtoto wa Geti kali" of the *Bongo Flewa* group Gangwe Mobb; expression 'child of the fierce gate'.
- mtoto wa mama** n.phr *mtu mvivu na ambaye si mhuni* lazy person who is not a hooligan
Dysphemistic expression 'mother's child'.
Yule ni mtoto wa mama.
Yule ni mvivu.
Acha utoto wa mama.
Acha uvivu.
- mtoto wa watu** n.phr *msenge, shoga*
homosexual man
Euphemistic expression 'child of people'.
Juma ni mtoto wa watu.
Juma ni msenge.
> *anti, baba askofu, choko*
- mtu wangu** n.phr *rafiki yangu* my friend
Synecdochical extension of SS *mtu wangu 'my man'.
> *babu, mshikaji, mwana*
- mtungo** n3 1. *fanya kitu kwa pamoja* 2. *fanya mapenzi na mwanamke mmoja kwa wanaume wengi wakati mmoja* 1. do sth together 2. group sex, group rape
Metonymic extension of SS *tunga 'string'.
1. *Tulikula mtungo jana.*
2. *Tulikula chakula kwa pamoja jana.*
> *mshikaki*
- mtutu** n *pikipiki* motorbike
Metonymic extension of SS *mtutu 'barrel of rifle'.
Dr. Gwassa day fulani kamotoa na mtutu.
Dr. Gwassa siku fulani kaondoka na pikipiki.
- mukide** adj *mzuri, afadhali* good, better
< ?
Oya, sumu ya leo ni mukide.
Oya, uji wa leo ni mzuri.
> *shega, poa*

- mustachi** n *ndevu za mdomo* moustache
Transfer from SE 'moustache'.
> *oo*
- muvi** n5 *video* video
Metonymic extension of SE 'movie', also attested in varieties *muvi and *muven.
Attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 23).
Leo kuna muvi poa sana tukalichekeshie.
Leo kuna video nzuri sana tukaiangalie.
- muziki mnene** n.phr 1. *redio kubwa sana, alama ya uwezo wa mtu* 2. *ugomvi* 1. big radio, as sign of wealth 2. quarrel, fight
Metaphoric extension of SS *muziki 'music' and *nene 'fat, stout', attested in older Swahili slang as *muziki 'punishment' (Ohly 1987a: 59); expression "thick music".
1. *Yule ana muziki mnene.*
1. Yule an redio kubwa sana.
2. *Mwogope yule jamaa, muziki wake ni mnene.*
2. Mwogope yule jamaa, ana hatari, si rahisi kumchezea.
- mvinyo** n3 *nyonga kubwa* large hips
Metaphorical extension of SS *mvinyo 'wine', based on the form of a "Mateus rosé" wine-bottle.
Yule ana mvinyo.
Yule ana nyonga kubwa.
> *bastola, bunduki, pisto[l], silaha*
- mvinyo** n3 *pombe ya aina yo yote* alcoholic drink, beer
Synecdochical extension of SS *mvinyo 'wine'. Popularised through a song by Prof. Jay which has: "Amekuta mpenzi wake akigonga mvinyo".
Mpenzi wake amegonga mvinyo.
Mpenzi wake amekunywa pombe.
> *chang'aa, tungi, ulabu*
- mwaga macho** v.phr *angalia sana* stare
Metaphorical extension of SS *mwaga 'pour out' and *macho 'eyes'; expression 'pour out eyes'.
- mwaga mtu kinyesi** v.phr *mwaga mtu shutuma, paka shutuma mbaya* put blame on sb, slander, calumny
Metaphorical extension of SS *mwaga 'pour

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- out' plus *kinyesi 'faeces'; expression
"pour out faeces on sb".
Jana mlitaka kummwaga mtu kinyesi.
Jana mlitaka kumpaka mtu shutuma mbaya.
- mwaga nyeti** v.phr *toa habari za muhimu, simulia* diffuse sensitive news
Metaphorical extension of SS *mwaga 'pour'
plus SS* nyeti 'concerning sensitive, delicate matters'.
Mwanangu nimwagie nyeti.
Rafiki niambie habari za muhimu.
- mwaga sera** v.phr *eleza kwa ufasaha* explain clearly
Metonymic extension of SK *mwaga 'pour out' plus *sera 'policy'
Nilimwaga sera wakakubali.
Nilieleza jambo wakakubali.
- mwake** adj? *safi, zuri* nice
< ?
Maria mambo yake mwake kabisa.
Maria mambo yake safi kabisa.
Vipi, nguo safi? - Mwake tu.
Vipi, nguo ni safi? - Safi tu.
- mwana** n1 *rafiki yangu* my friend
Synecdochical extension of SS *mwana 'child'. Since 2000.
Tuliza boli, mwana, mambo chelea pina.
Subiri, rafiki yangu, mambo mazuri sana.
Hoya mwana, unamcheiki huyo bwege?
Hoya mwana, unamwona huyo bwege?
> *mshikaji, mshirika, msela, mazee, mzee, kachala, kichaa wangu*
- mwanangu** n.phr *rafiki* friend
Synecdochical extension of SS *mwanangu 'my child'.
Unasemaje mwanagu?
Unasemaje rafiki yangu?
- mwanaapolo** n1/2 *mzamiaji chini ya mgodi* person who works unofficially in a mine as helper. He is going deep into the mine.
Metaphorical expression based on US space programme "Apollo"; expression "astronaut in the Apollo programme". In older Swahili slang *Apolo is attested with the meaning 'menstruation'; *niko Apolo 'I have my monthlies' (Ohly 1987a: 21).
Mwanaapolo amefia shimoni.
- The unofficial worker died in the mine.
- mwela** n5/6 *polisi, askari, afande* police
< ?
Washikaji, chomokeni! Mamwela kibao wanakatiza maskani.
Jamani, kimbieni! Mapolisi wengi wanapita nyumbani.
Ipo dei fulani mamwela walinijia kutaka niwagee ganja ili wanisobe rupangoo.
Ipo siku fulani polisi walinijia kutaka niwape bangi ili wanichukue gerezani.
> *kapelo, ndata, ndula, njagu*
- mwembe** n3 *nywele nyingi au afro* thick hair or Afro-look
Metaphorical extension of SS *mwembe 'mango tree', based on the shape of mango trees with many branches and twigs.
Mwembe wako unavuta kinoma!
Nywele zako nyingi zinapendeza sana.
- mwepesi** n1/2 *mtu mchangamfu, mwenye kusikia raha* cheerful person
Metonymic extension of SS *epesi 'light, quick'.
Yaani babu sasa ni mwepesi.
Yaani rafiki sasa wewe una raha.
- mzamiaji** n1/2 *mtu ambaye amefika mahali au katika tukio bila mwaliko au kibali* sb who comes to a place or event without invitation
Metaphorical extension of SS *mzamiaji 'diver by profession, e.g. of those who dive for coins in harbours when passenger ships are in'.
Yule amevalikwa hapa? - Hapana, ni mzamiaji.
Yule amevalikwa hapa? - Hapana, amefika bila mwaliko.
> *zama, zamia*
- mzee** n1 *rafiki* friend
Synecdoche of SS *mzee 'old man, elder'.
Used as address.
Kisha mzee najipulizia marashi. (In song Mikasi by Ngwair, 2004).
Kisha rafiki najipulizia marashi.
> *mshikaji, msela, mwana*
- mzee ruksa** n.phr *rais Ali Hassan Mwinyi* nickname of President Ali Hassan Mwinyi

Dysphemistic antonomastic extension of derivation of SS *ruhusa 'permission', based on president Mwinyi's politics of liberalisation.

mzee wa busara n.phr *mchawi* sorcerer, witch
Euphemistic extension of SS *mzee 'old person' and *busara 'wisdom'.
> *gagula*

mzee wa mikogo n.phr *mtu mwenye maringo* proud, boasting man
Semantic extension of SS *mkogo 'showing off, doing tricks, display'.
Yule ni mzee wa mikogo.
Yule ana maringo.
Mzee wa mikogo Juma amepita.
Juma anayependa sifa amepita.

mzuka n 1. *wasiwasi* 2. *hamu* 3. *ari* 1. worry
2. desire 3. moral
Metonymic extension of SS *mzuka 'sudden apparition, pop-up, spirit, ghost'.
Oya mshikaji, tuliza mapepe, usiwe na mzuka!
Rafiki, tuliza haraka, usiwe na wasiwasi!
Nina mzuka kwenda kwenye muziki.
Nina hamu kwenda kwenye muziki.

mzula n3 *kofia* cap
Derived from older Swahili slang form meaning 'fez' (Ohly 1987a: 60).
Lorand leo katinga bongwe la mzula.
Lorand leo kavaa kofia kubwa.

mzungu wa reli n.phr 1. *mshamba, mgeni, mpumbavu* 2. *mkubwa wa wapiga debe daladala* 1. country-bumpkin, stranger, fool
2. leader of the daladala cryers
1. is the older meaning, also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 60). It denoted people who came from up country or far away to Dar es Salaam (by train). There is also a saying: "mbumbubum - mzungu wa reli." 2. is connected to the daladala sub-culture and denotes the young men, often said to be drug users, who earn a little money by calling passengers to a daladala. They get a small share by the daladala personnel.
Wale wazungu wa reli wanapiga debe.

mzungu wa unga n1/2 *muzaji mkubwa wa*

madawa ya kulevya (big) drug dealer
Expression based on metonymic extension of SS *mzungu 'European, white man' which in LyM has the connotation "mtu mwenye hali ya juu" 'person who is well-off' plus metonymic extension of SS *unga 'flour' meaning 'drugs in form of white powder'; also used in gender 5/6 as *zungu la unga.

Wanaokamatwa mara nyingi ni watumiaji wadogo na si wazungu wa unga.
Wanaokamatwa mara nyingi ni watumiaji wadogo na si wauza madawa ya kulevya.

nafaka n *ugali* porridge
Synecdochical extension of SS *nafaka 'cereals'.
Nafaka ya leo noma sana.
Ugali wa leo mbaya sana.
> *dona, dongo, nafaka, nguna, sembe*

namba kumi n.phr *umbo la mwanamke mnene kuanzia juu hadi chini* shape of a fat woman with flat forms
Metaphorical extension of SS *namba kumi 'number ten' based on form of the number 10. Attested in older Swahili slang with the meaning 'intelligence officer' (Ohly 1987a: 61).
Mwanamke mwenyewe ni wa namba kumi.
Mwanamke mwenyewe ana umbo kama namba kumi.

namba nane n.phr *umbo la msichana anayevutia, mwanamke mwenye kiuno chembamba* shape of a beautiful girl with wasp waist
Metaphorical extension of SS *namba nane 'number eight' based on form of the number 8.
Mimi napenda wasichana wenye umbo la namba nane.
Mimi napenda wasichana wenye kiuno chembamba.
Grace ana umbo la nane.
Grace ana kiuno chembamba.
Hoya cheki namba nane ile.
Mwangelie msichana mwenye umbo la kuvutia.

namba sita n.phr *umbo la mtu ambao kwa chini ni mnene na kwa juu ni mwembamba* shape of body with fat lower part and slim

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- upper part
Metaphorical extension of SS *namba sita 'number six' based on form of the number 6.
- namba tisa** n.phr *umbo la mtu ambao kwa chini ni mwembamba na kwa juu ni mnene*
shape of body with slim lower part and fat upper part
Metaphorical extension of SS *namba tisa 'number nine' based on form of the number 9.
- nanii** (n/v) *neni lisilo na maana na liwezalo kutumika badala ya neno lolote lile, agh. wakati wa kutafuta neno halisi* what'sit, thingummy, doo-dah
Probably derived from SS *nani 'who', used as a dummy for any noun or verb.
Colloquial, old, and common.
- narenare** adv *taratibu; kwa uzembe* slowly < ?
Acha kufanya narenare.
Acha kufanya [mambo] taratibu.
Alitembea narenare.
Alitembea taratibu.
> *ado ado*
- nari** n9 *moto kwa ajili ya kuwasha sigara* fire to light a cigarette
Metonymic extension of SS *nari 'fire'. In Sheng attested as *nare 'match stick' (Mbaabu & Nzuga 2003: 23).
Naomba nari niwashe sigara.
Naomba moto niwashe sigara.
> *kinari*
- nata** v *ringa kwa kudharau* boast by looking down on sth or sb
Dysphemistic metaphorical extension of SS *nata 'stick'.
Mary ananata sana.
Mary anaringa sana.
- nawa** v *kutofaulu* fail
Elliptical metonymic extension of SS *nawa 'wash hands', based on the cultural script of washing hands as a prelude to eating. Since eating metaphorically refers to sexual intercourse, *nawa in this context refers to petting and fondling. In older Swahili slang with opposite meaning *amenawa 'he is clever, he is progressing' (Ohly 1987a: 79).
Utanawa.
Hutafaulu.
Nimenawa mtihani.
Sikufaulu mtihani.
Jamaa kanawa mikono.
Jamaa hakufaulu.
Misheni yangu imenawa.
Mpango wangu haukufaulu (Sikufanikiwa).
Unanawa, lakini hutakula! NHT
You might touch me, but you will not sleep with me! (spoken by a girl to her lover).
- naye** adv *safi* nice, well
Semantic extension of SS *naye 'with him/her'.
Mtihani vipi? - Naye!
Mtihani vipi? - Safi!
- ndata** n5/6 *askari (wa polisi)* policeman < ?
Mandata wamembamba.
Mapolisi wamemkamata.
> *mwela, ndula, njagu*
- ndina** adv *ndani, nyumbani* in, inside, at home
Metathesis of SS *ndani 'inside'.
Kesho mimi mwenyewe ndina.
Kesho mimi mwenyewe nitakuwepo nyumbani.
- ndinga** n9/10 *gari kubwa, lori* big car, lorry < ? Also attested in Sheng as 'car' (Mbaabu & Nzuga 2003: 23).
Oya kamata ndinga hiyo.
Oya panda lori hiyo.
- ndita** n9 *hasira* < ?
Probably ellipsis of SS *kunjia ndita 'frown'.
Juma ana ndita kila wakati.
Juma anakasirika kila wakati.
- ndomu** n9/10 *kondom* condom
Initial truncation of SE 'condome'.
> *buti, pilaa, soksi*
- ndonga** n9/10 1. *kichwa kikubwa* 2. *kiatu kikubwa* 1. big head 2. big shoe
Metaphorical extension of SS *ndonga 'stick with a round knot on one side'.
- nduki** n9/10 *nyonga kubwa* large hips
Initial clipping of LyM "bunduki" 'large hips'.
Yule ana nduki.

- Yule ana hips kubwa.
> *bastola, bunduk, pisto[l], silaha, mvinyo*
- ndula** n9/10/6 *polisi* police
Metonymic extension of LyM *ndula 'boots'.
Ndula wanakuja kila saa.
Mapolisi wanakuja kila saa.
> *mwela, ndata, njagu*
- ndula** n *kiatu kikubwa na ya bei ghali kinachopendwa na vijana, hata na wasichana* boots, big and expensive shoes, liked by young people, even girls
< ? Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 23).
Lorand leo katinga bongwe la ndula.
Lorand leo kavaa kiatu kikubwa.
> *bandapanda, buti, gozi, lakuchumpa, tumba*
- ndula** n *bwege, mjinga, mzembe* simpleton, fool, careless person
Metonymic extension of LyM *ndula 'police', motivated by the low level of education of police in former times.
Rafiki yangu usiwe ndula.
Rafiki yangu usiwe mjinga.
Yule ni ndula sana. Alinilengeshi!
Yule ni mzembe sana, alisababisha nikamatwe na polisi.
> *boka, mbwiga, poyoyo*
- ndumilakuwili** n *kigeugeu* fickle, unstable, wayward person
< ? Onomastic synecdoche of character in cartoon whose name is Ndumilakuwili.
Wewe ni ndumilakuwili tu.
Wewe ni kigeugeu tu.
- ndumu** n9/10 *bangi* Indian hemp, marijuana; opium
< ?
> *kijiti, ganja, mjani, msuba*
- ndómbolo** n *matako makubwa* fat buttocks
Metonymy based on a highly eroticised dance style originating in Zaire called "N'Dombolo", in which buttock-movements are prominent.
> *bambataa, haja kubwa, kibinda, mkundu, shuzi, taarabu, tukunyema, wowowo*
- nenepa kisimba** v.phr *nenepa kwa juu* have a big chest
Metaphorical extension of SS *nenepa 'grow fat' and *simba 'lion', based on the form of the lion's body with a broad front.
Mary amenenepa kisimba.
Mary amenenepa kifuni.
- nesanesa** v *yumbayumba* have good suspension (car), wave to and fro
Hyperbolic extension of reduplication of SS *nesa 'bend, beat'?
Gari lilikuwa linanesanesa kinoma.
Gari lilikuwa linayumbayumba sana.
> *yesa*
- neti** n *jela, gereza* prison
Metonymic extension of SE 'net', motivated by the fences of screen wire surrounding prisons.
> *sero / selo, shimoni, lupango*
- ngama** n *chakula kizuri, ugali* nice food, ugali
< ? Obsolete.
> *msosi*
- ngano** n9 *bia, hasa "Safari Lager"* beer, esp. "Safari Lager"
Synecdochical extension of SS *ngano 'wheat'.
> *maji ya dhahabu, tungi, ulabu*
- ngarangara** n9/10 *kitu kibovu; gari au basi bovu bovu* bad, broken thing; worn car or bus
< ?
Achana na ngarangara hizo.
Achana na vitu vibovu hivyo.
- ng'arisha** v.caus *pendezesha, pendeza* cause to please, please, look good
Metaphorical extension of derivation of SS *ng'ara 'shine, gleam'.
Yaani umeng'arisha babu.
Yaani umependeza.
- ngawila** n10 *fedha, pesa* money
< ?
Nipe ngawila zangu.
Nipe pesa zangu.
> *mapene, mkwanja, uchache*
- ngenga** n9/10 *shaka* doubt
< ?
Haina ngenga.
Haina shaka.
- ngeta** n9/10 *kabari* wedge
< ?
Alipigwa ngeta na masela jana.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Alipigwa kabari na vijana jana.

ngeukia v *umia* be hurt

< ?

Amengeukia!

Ameumia!

ngoma n9 1. *ukimwi* 2. *bunduki* 3. *msichana*

1. AIDS 2. gun 3. girl

Metaphorical extension of SS *ngoma 'drum, dance', attested for older Swahili slang with the meanings 'vagina' and 'generative power' (*hana ngoma 'he is impotent'; (Ohly 1987a: 62), in *piga ngoma 'copulate' (Ohly 1987a: 67), and in *hamna ngoma 'be without a girl (woman)' (Ohly 1987: 37).

1. *Alikufa kwa ngoma.*

1. Alikufa kwa ukimwi.

1. *Anaumwa na ngoma.*

1. Anaumwa na ukimwi.

1. *Umepima ngoma?*

1. Umepima ukimwi?

3. *Ngoma yangu yule.*

3. Msichana wangu yule.

> *feruzi, mdudu, minyenyele, miwaya, msaada, ngwengwe, umeme*

ng'ombe n9 *mtu mwenye pesa anayekabwa na wahuni* person who has money and is getting pinned down by hooligans

Dysphemistic metaphorical extension of SS *ng'ombe 'cow, cattle', based on the concept of a cow being milked.

Wana, jana tulikamua ng'ombe.

Marafiki, jana tulimtoza pesa mtu mwenye pesa.

ng'ota v *piga, hasa kwa fimbo* beat, especially with a stick

< ?

> *lamba njiti*

ngozi n9/10 1. *msichana, mwanamke* 2. *jinsi*

3. *kiatu* 1. girl, woman 2. jeans 3. shoe

Metonymic extension of SS *ngozi 'skin'.

Motivation for 1. Sexual act, where skin

meets skin 2. Jeans are like a second skin

3. Shoes are made of skin.

1. *Ile ilikuwa ngozi ya Mudi.*

1. Yule alikuwa mpenzi wa Mudi.

1. *Umeiona ngozi ya kutosha babu!*

1. Umemwona msichana mzuri, rafiki?

2. *Umevaa ngozi mpya?*

2. Umevaa jinsi mpya?

3. *Kaweka ngozi. IM*

3. Kavaa viatu.

> 1. *sholi, shori* 2. *gamba, suru* 3. *bandapanda, buti, dula, gozi, lakuchumpa, tumba*

ngudongudo n10 *pesa* money

< ?

Oya mshikaji nigeo ngudongudo!

We, rafiki, nipe pesa!

nguna n9/10 *ugali* porridge

< ?

Leo kuna nguna na mandondo.

Leo kuna ugali kwa maharage.

> *bondo, dona, dongo, sembe*

ngurumbili n9/10 *mtu, binadamu* human being

< ?

Huwezi kumdhibiti ngurumbili.

Huwezi kumdhibiti mtu.

ngwengwe n9 *ukimwi* AIDS

Derived from SS *ngwea 'become thin, emaciated'?

Ah, mwenzetu amepatikana na ngwengwe.

Ah, Mwenzetu amepatikana na ukimwi.

Baba yule ana ngwengwe.

Baba yule ana ukimwi.

> *feruzi, ngoma, mdudu, minyenyele, miwaya, umeme*

ngángari n *kitu au mtu imara* tough, strong, brave person, state of being fit

Coinage of party CUF during election campaign in 2000; motivation unclear.

Popularised by *Bongo Flewa* song "Ngangari" (Gangwe Mobb 2000).

Mimi niko ngángari kinoma hapa, njoo tu.

Mimi niko hodari sana hapa, njoo tu.

Baada ya wao kuwa ngangari, manjagu wakawa ngunguri.

Baada ya wao kuwa watu wenye msimamo, mapolisi wakawa wakali.

> *ngúnguri*

ngúnguri n *kitu au mtu imara* tough person; strong, brave person

Coinage of Police leader during election campaign in 2000, in response to CUF:

Katika uchaguzi uliopita CUF walisema: wakitaka kutudhulumu, sisi ni ngángari.

- Inspekta jenerali wa polisi akajibu:
"Kama mko ngángari, basi sisi tuko ngúnguri." Motivation unclear.
Baada ya wao kuwa ngangari, manjagu wakawa ngunguri.
Baada ya wao kuwa watu wenye msimamo, manjagu wakawa wakali.
> *ngángari*
- nido** n5/6 *matiti makubwa* big breasts
Onomastic synecdoche based on the name of the milk powder "Nido".
Asha ana nido.
Asha ana matiti makubwa.
Manido yake yamezidi.
Matiti yake ni makubwa kupita kiasi.
> *mtindi, tikitimaji, balungi*
- nipa** n9 *pombe kali haramu, gongo* locally and illegally distilled liquor
> ? Attested in older Swahili slang with the meaning 'kind of local beer' (Ohly 1987a: 62). Old.
Anakunywa sana nipa.
Anakunywa sana gongo.
> *machozi ya simba, maji makali, supu ya mawe*
- njago, njagu** n5/6 *polisi, askari* police officer
< ? In the presence of policemen the kinyume variety *gonja would be chosen to veil the meaning in a more effective way. Also in Kihore (2004: 9).
Huyu njagu anasemaje?
Huyu polisi anasemaje?
Kinachotukera ni mtindo wa yule njago kukamata watu ovyo.
Kinachotukera ni mtindo wa yule askari kukamata watu ovyo.
Manjago watakuja.
Mapolisi watakuja.
> *kapelo, mwela, ndata, ndula*
- njemba njemba** n.phr *mtu mwenye mwili mkubwa na mwenye nguvu, baunsa, miraba minne* big strong man, bouncer
Onomastic synecdoche of Zambian football player Njemba Njemba.
Zikatuibukia njemba njemba flani.
Tukakutana na watu fulani wenye miili mikubwa.
> *baunsa*
- njia za panya** n.phr *njia zisizo halali* unofficial route, unofficial procedure
Metaphorical extension of SS *njia 'way' and *panya 'rat'; expression 'ways of rats'.
AMepata pasipoti kwa njia za panya.
Amepata pasipoti kwa njia zisizo halali.
- njiapanda ya Ulaya** n.phr *barabara kubwa ya kuelekea uwanja wa ndege Dar es Salaam* the main road from town to the airport of Dar es Salaam
Antonomastic extension of SS *njiapanda 'crossroads' and *ulaya 'Europe'.
- njiti** n9/10 *fimbo* stick
Derivation of *jiti 'big stick'.
Akanilamba njiti sita.
Akanipiga fimbo sita.
- njoroge** n10 *fedha za chuma* silver money, coins
< ? There might be an etymological link to SS *njugu 'groundnuts' via another Bantu language. Njoroge is also a frequent name in Kenya.
Huyu maza ana njoroge za maandazi.
Huyu mama ana pesa za maandazi.
- noa** v *kosa* fail, miss
Metonymic extension of transfer from SE 'no'? Semantic extension of SS *noa 'sharpen'? In KKS 2.
Utanoa.
Utakosa.
- nokolaizi** v/n *kueleza jambo hata siri, kusemea kwa mkubwa, sengenya, singizia* tell secrets, calumniate, slander, snitch on sb
Derivation of LyM *mnoko 'one who gives secrets away', extended by a verbalising suffix *-laize ~ *laizi shaped after the English model, e.g. verba-lise. Rare.
Huyu bloo ni kichomi tena mnokolaize sevuni.
This bloke is a pest and a telltale, so avoid him!
Jamaa ameninokolaizi kwa bosu wangu.
Jamaa amenisemea kwa mkubwa wangu.
> *chonga, pakaza*
- noma** n9/10 *aibu, soni; balaa, kasheshe, matatizo, hatari* bad; shame; trouble
Semantic extension of SS *noma 'working chit (as proof that one was working)' or reduction, fusion and semantic extension

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

of SE 'no, man!', or transfer from Se 'normal'? According to Bertoncini (cited after Böhme 2004: 49) originating in the name of a currency used as payment in a plantation in colonial times to bind workers to that plantation. It is frequently used as a single word utterance for the purpose of saying 'leave it!, stop it!'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 25).

Du washikaji, hamwoni noma kuvinjari getoni!

La jamani, hamwoni aibu kuzunguka chumbani!

Soo bloo, wacha noma!

Hapana kaka, usilete balaa!

Ampata bongwe la noma.

Ampata matatizo makubwa sana.

> *skendo, kasheshe*

ntimanyongo n *roho mbaya* unkindness
Metonymic extension of *ntima 'heart' (from a Bantu language other than Swahili) plus SS *nyongo 'bile'.

> *roho ya korosho, roho ya kwanini*

nundu n5 *matako makubwa* big behind
Dysphemistic metaphorical extension of SS *nundu 'hump'.

Cheki nundu lile.

Angalia matako makubwa yale.

> *shuzi*

nunga embe n.phr *mwanamke ambaye hapati mume, mwanamke asiyeolewa* woman who doesn't get a husband

Metaphoric extension of SS *embe 'mango', based on the image of a mango fruit which has fallen from a tree and starts rotting as a worthless thing. Coined and popularized by *Bongo Flewa* lyrics: "Wanawake wazuri wazuri wameolewa, wamebaki manunga embe wanahangaika." The first part of the phraseme might be related to older Swahili slang *nunge 'nil, nothing' (Ohly 1987a: 63).

nunga nanasi n.phr *mvulana asiyepata mke* man who doesn't get a wife

Metaphoric extension of SS *nanasi 'pineapple'. First part of phraseme might be related to older Swahili slang *nunge

'nil, nothing' (Ohly 1987a: 63).

*Manunga nanasi is a reply to *manunga embe in *Bongo Flewa* music. The line is: Wanaume wazuri wazuri wameoa, wamebaki manunga nanasi wanahangaika.

nusu kilo n.phr *shilingi 50000* 50000 shillings
Semantic extension of SS *nusu 'half' and SE 'kilo'.

> *kilo*

nusu peponi nusu kuzimu n.phr *hali wanayojisikia watu wanaotumia madawa ya kulevya* drug intoxication
Metaphorical expression "half in heaven, half with the ancestral spirits".

Niko nusu peponi nusu kuzimu.

Niko nimelewa madawa.

nyali n10 *wali* cooked rice
Plural of SS *wali 'cooked rice'. Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 63).

Wacha tufinye nyali.

Wacha tule wali.

> *mavi ya panya, pungu, punje, ubeche, ubwabwa*

nyambizi n9 1. *mwanamke aliyejaaliwa maungo ya nyuma* 2. *mtu mnene na ameambukizwa na ukimwi* 1. lady with big buttocks 2. fat person, attractive and dangerous, because she or he might be infected by AIDS

Dysphemistic metaphorical extension of SS *nyambizi 'submarine'. Since 2001.

Jana nilikutana na nyambizi mmoja kituo cha basi.

Jana katika kituo cha basi nilikutana na mwanamke mnene ambaye labda ameambukizwa na ukimwi.

Nyambizi yule ana bongwe la figa.

Mwanamke mnene yule ana umbo mzuri kupita kiasi.

Jana nilikuona na bongwe la nyambizi.

Jana nilikuona na mwanamke mnene sana.

> *dege la jeshi, gubeli, jimama, shangingi, tinginya*

nyanga n9/10 *shilingi 100* 100 shillings
< ? Older Swahili slang has *nyang'ule 'money' (Ohly 1987a: 63).

> *jiti, nyeto, pini, hais, alasiri, fisi*

nyanya puza n.phr *suruali inayoishia chini ya magoti na iliyo pana* wide trousers ending below the knees; pant skirt
< ? Metaphorical extension of SS *nyanya 'tomato' seems to be involved.
> *pensi nyanya*

nyanyapaa v *tenga, nyanyasa, epuka mtu kwa dharau (hasa mwenye ukimwi)* avoid, stigmatise sb (especially AIDS patients)
Metaphoric extension of SS *nyanya 'cause to be prominent, protrude, put out, raise up' and SS *paa 'roof of hut' or blend with SS *nyapa 'stalk after, creep after' or SS *nyanyasa 'treat disrespectfully'?
Neologism by BAKITA. In KKS 2.

nyasi n9/10 *bangi* weed, grass
Calque of English slang *grass: SS *nyasi 'grass'.
Juma ameshakula nyasi yake.
Juma ameshavuta bangi yake.
> *blant*

nyea debe v.phr *wekwa jela* be in prison
Metonymic extension of SS *kunya 'shit' and *debe 'tin'; expression 'shit in the tin'.
Mshikaji amenyea debe saa hizi.
Mwenzetu yuko jela sasa.
> *swekwa lupango*

nyemka v *kosea* err
< ?
> *chemka, tokota*

nyento n9/10 *sarafu ya shilingi 100* coin of 100 TSh.
?. Especially used by daladala personnel.
Nipige nyento.
Nipe shilingi 100.
> *alasiri, bati, doma, hais, jiti, nyanga, pini*

nyenyere, nyenyele n10 *virusi za ukimwi* HIV-Viruses
Metaphorical extension of SS *nyenyere 'tiny black ant'
Angalia usije ukavamie nyenyere.
Angalia usije ukapate (virusi vya) ukimwi.
> *mdudu, minyenyele, miwaya, msaada, ngoma, nyenyere, umeme*

nyoka n9 1. *msaidizi wa kazi katika mgodi* 2. *mtu anayefanya kazi ya kibarua na katika sehemu ya kazi hiyo yeye ni mgeni na wa*

cheo cha chini kabisa 1. unofficial worker who helps in mines 2. labourer who is new in a certain unofficial work-place
Metaphorical dysphemistic extension of SS *nyoka 'snake'. The term started to be used in mines, where those people dig in the deepest parts. From there the concept was transferred to any work, but especially daladala buses.
Nyoka wangu msanii.
Nyoka wangu mbabaishaji.
> *deiwaka*

nyola n9/10 *ukimwi* AIDS
< ?
Ana nyola yule.
Ana ukimwi yule.
> *mdudu, ngoma*

nyomi n9/10 *shilingi 50 50* shillings
< ?

nyomi n9 *wingi* plentiness
Modification of SS *nomi 'abundance'.
Kituoni tulikuwa watu nyomi.
Kituoni tulikuwa watu wengi.
> *lumbesa, shazi*

nyonyo n5/6 *maziwa makubwa* big breasts
Dysphemistic metonymic extension of SS *nyonya 'suck'.
Yule ana manyonyo.
Yule ana maziwa makubwa.
> *balungi, tikitimaji, mtindi, nido*

nyunyu n5 *harufu ya bangi* scent of a joint
Euphemistic extension of SS *nyunyu 'drizzle'.
Hili nyunyu mh!
Hii harufu ya bangi ni nzuri.

nyuti v *tulia* calm down, settle down
Derivation from SS *nyuti 'slowly, carefully'.
Juma amenyuti.
Juma ametulia.
> *bana, egesha*

oo n *ndevu za mdomo zenye umbo la "O"* moustache
Iconic motivation based on its form as a circle surrounding the mouth.
Amechonga vizuri ikawa oo.
Amenyoa vizuri ikawa na umbo la O.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

> *mustachi*

ondoa kiwingu, toa kiwingu v.phr *ondoka*

make off, run away

Metaphoric extension based on SS *uwingu 'cloud' plus *toa 'take away'.

Toka hapa, niondolee kiwingu kiaina aina.

Toka hapa, uondoke.

> *timua, ishia, chomoa*

opoa v 1. *iba* 2. *ona* 3. *pata* 1. steal 2. see 3. get

Euphemistic extension of SS *opoa 'take out, save, rescue'.

1. *Nipe za kuopoa.*

1. Nipe za kuiba.

2. *Nimekuopoa ukienda gesti na msichana.*

2. Nimekuona ukienda gesti na msichana.

3. *Umeopoa demu.*

3. Umepata msichana.

opoa demu v.phr 1. *lala na msichana*

nyumbani kwa mwanamume 2. *pata*

msichana 1. sleep with a girl in the house of the man 2. get a girl

Metaphoric extension of SS *opoa 'take out, save, remove a magic spell' or LyM

*opoa 'steal' plus LyM *demu 'girl'.

Umeopoa demu.

Umepata msichana.

osha v.caus *fanya mapenzi* enjoy, make love

Semantic extension of SS *osha 'wash'; a

similar extension is attested in older

Swahili slang *ogelea 'copulate' (Ohly

1987a: 65), derived from SS *ogelea

'take a bath'.

Twende tukaoshe!

Twende tufanye mapenzi!

osha kioo v *kuangalia, kutazama* watch, look at

Semantic extension of SS *osha 'wash'.

Njoo kuosha kioo!

Come and watch the video!

osha macho v.phr *kuangalia, kutazama;*

kustarehe watch, look at, stare

Semantic extension of SS *osha 'wash'.

Anaosha macho.

He is staring.

pablo n *muuza madawa* drug dealer

Probably onomastic synecdoche of Spanish

name "Pablo", based on the name of the Colombian drug lord Pablo Escobar (killed 1993).

Ah! Wapi, ni pablo tu yule.

Ah! Wapi, ni muuza madawa ya kulevya tu yule.

pafomu v *cheza, igiza, onyesha* perform

Transfer from SE 'perform'.

Baada ya kumaliza kupafomu ndipo

alipoendelea kuvunja traki nyingine.

(Sani 214:6-7)

Baada ya kumaliza kupiga muziki ndipo

alipoendelea kuimba wimbo mwingine.

pagaisha v.caus *changanya* confuse

Metaphoric extension of SS *pagaa 'be possessed by an evil spirit'.

Unanipagaisha.

Unanichanganya.

Rafiki yangu kuna binti pale amenipagaisha

kweli, mpaka akili haifanyi kazi.

Rafiki yangu, kuna binti pale

ananichanganya kweli, mpaka akili

haifanyi kazi.

> *pagawa*

pagawa v.pass *changanyikiwa* be confused

Metaphoric extension of SS *pagaa 'be possessed by an evil spirit'.

Nimepagawa kweli.

Nimechanganyikiwa kweli.

> *pagaisha*

pailoti n5/6 *dereva* driver

Metonymic extension of SE 'pilot'.

Oya pailoti, weka tuta!

We dereva, simamisha gari!

palichimbika v.phr *kulikuwa na vurugu*

kubwa there was a big quarrel

Metaphorical extension of SS *chimba 'dig'.

Mwanangu, mbona palichimbika.

Mwanangu, mbona kulikuwa na vurugu

kubwa.

palma n *kokeni* cocaine

Metonymic extension of LyM *palma 'hat worn by drug sellers'. Since 2005.

Nafanya biashara ya palma.

Nafanya biashara ya kokeni.

> *bwimbwi*

pamba n/adj 1. *nguo zinazoenda na wakati* 2.

kitu kizuri, chenye fasheni 1. fashionable clothes 2. sth nice and fashionable
Metonymic extension of SS *pamba 'cotton'.

1. *Amevaa pamba.*

1. Amevaa nguo nzuri ya kisasa.

1. *Amevaa pamba nyepesi.*

1. Amevaa nguo nzuri na za bei ya juu sana.

2. *Ah, umepanda daladala pamba sana.*

2. Ah, umepanda daladala nzuri na ya kisasa.

> *ming'aro*

panda kichizi v.phr *kuja juu kwa kasi* get quickly angry

Semantic extension of SS *panda 'climb, rise, go up' and substandard Swahili *chizi 'crook, type'.

> *chizi, kichizi*

pandisha kenchi v.phr *umwa na ukimwi* suffer from AIDS

Metaphorical extension of SS *pandisha 'lift' and transfer from SE 'quench', based on appearance of a wasted person, whose scapulae are prominent and visible, as is the case with people suffering from AIDS or TB.

> *umeme, kanyaga miwaya, mdudu, ngwengwe, ngoma*

pank[i] n5/6 1. *aina ya unyoaji wa nywele wenye sehemu ya juu ya mraba* 2. *kitu chenye sehemu ya juu ya mraba* 1. punk style of haircut 2. anything with a flat, edged top
Transfer from SE 'punk', based on the image of head with angular haircut which is flat at the top, therefore extension to anything which has a flat top, e.g. certain kinds of busses.

Kuna wengine walionyoa panki.

Kuna wengine walionyoa nywele kwa mtindo wa "panki".

> *dungu*

panya n9/10 *daladala ndogo, haisi* small bus, Toyota Hiace

Metaphorical extension of SS *panya 'rat, mouse'.

Tulikula zetu panya na kuingia kati.

Tulipanda daladala ndogo tulipokwenda mjini.

paparazi n5/6 1. *mwandishi wa habari kwa ujumla, hata mpiga picha* 2. *mnoko* 1.

journalist, even photographer 2. denouncer
Dysphemistic extension of SE (< Italian) *paparazzi.

Washirika, tuishie, mapaparazi watatuchukua foto.

Jamani, tuondoke, waandishi wa habari watatupiga picha.

Mnacheke, washikaji, wakati nasevu mapaparazi wakanifotoa picha.

Mnaona, marafiki, wakati nilipotoroka, waandishi wa habari wakanipiga picha.
> *mnoko*

pasha v.caus *kula au kuvuta kitu fulani, hasa bangi; onja* eat or consume something, esp. marijuana; taste

Semantic extension of SS *pasha 'cause to get, cause to have'. Attested in older Swahili slang for the meaning 'explain' (Ohly 1987a: 67).

Pasha pombe!

Kunywa pombe!

Pasha feji!

Vuta sigara!

Njoo tupashe!

Njoo tuvute bangi!

pasnali adj *maridadi* smart, attractive
Transfer from SE 'personally'?

Mshikaji yaani umetoka pasnali.

Rafiki umevaa vizuri na uko maridadi.

pasua mangumi ya jela v.phr *piga mtu vibaya sana* beat sb up

Metonymic extension of 'punch sb like in prison'.

> *klintoni, kosovo*

pata blanketi v.phr *lala na msichana* sleep with a girl

Metonymic extension of SS *pata 'get' and SS *blanketi 'blanket'.

pata sho[r]ti v.phr *pata ukimwi* get infected with HIV

Metaphorical extension of SS *pata 'get' and transfer from SE 'short', the image is linked to SE 'short circuit'.

Ampata shoti.

He/She has been infected with HIV.

patulo n *suluhu, sare* draw
< ?

Gemu ya jana ilikuwa patulo.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Mchezo wa jana ulikuwa suluhu.

paundi n9/10 *sarafu ya shilingi 20* coin of 20 TSh.

Metonymic extension of SE 'pound'.

pedeshee n 1. *bosi, mtu mwenye hela* 2. *mtu anayependa kupendeza* 1. boss, person having money 2. person who likes to please
Transfer from French abbreviation *PDG - *président directeur général*. Not common.

Oya, mchekeki pedeshee yule.

Oya mwone mtu tajiri yule.

> *kibosile, mdosi, mnene*

pedo pusha n.phr *suruali ya kike inayoishia chini ya magoti na isiyo pana sana* 3/4 long trousers for women which are not loose
Transfer from SE 'pedal pusher'.

> *pensi nyanya, nyanya puza*

pensi nyanya n.phr *suruali inayoishia katika au kidogo chini ya magoti na iliyo pana* wide trousers ending below the knees; pant skirt
Transfer from SE 'pants' plus SS *nyanya 'tomato', motivated by form.

Mvulana aliyevaa suruali ya kupanuka mapajani alionekana kana kwamba ni msichana aliyevaa pensi nyanya!

> *pedo pusha, nyanya puza*

peponi adv;n loc *kiwanja cha ndege* airport
Metonymic extension of SS *pepo 'strong wind; winds', or SS *peponi 'in heaven'.

piga v *kupa* give

Semantic extension of SS *piga 'beat, knock'.

Nipige na mia, basi!

Unipe shilingi mia!

piga bao v.phr 1. *funga goli, shinda, zidi* 2. *kumwahi mtu kitu* 3. *fanya mapenzi* 4. *toa manii* 5. *ondoka* 6. *(gari) simamishwa na trafiki* 7. *danganya* 1. score, defeat, win 2. beat sb to it 3. sleep with a girl 4. ejaculate 5. go away 6. (car) get stopped by traffic-police 7. cheat

Semantic extension of SS *kula 'eat' and augmentative derivation of SS *bao 'goal.'

3. *Nimempiga bao demu fulani jana usiku.*

3. Nimefanya mapenzi na msichana fulani jana usiku.

3. *Demu wake amepigwa bao na mwanaume mwingine.*

3. Msichana wake amefanya mapenzi na mwanamume mwingine.

5. *Napiga bao.*

5. Naondoka.

6. *Gari limepigwa bao na trafiki*

6. Gari limesimamishwa pembeni na trafiki.

7. *Nilimpiga bao akanipa fedha.*

7. Nilimdanganya akanipa fedha.

> *kaza, tia, zidi kete*

piga beto v.phr *fanya ugomvi, anzisha ugomvi* start a fight, fight

Expression composed of SS *piga 'hit' plus adaption of SE 'battle'. Obsolete.

We mshikaji, ukileta za kuleta nakupiga beto.

We rafiki, ukileta ujinga nitakufanyia ugomvi.

piga bunda v.phr *ondoka, kimbia* go away, run away

Metaphorical extension of SS *piga 'hit' plus SS *bunda 'bale, bundle'.

Amepiga bunda.

Amekimbia.

Piga bunda, bwana.

Toka hapa, bwana.

> *anza, chomoa, ishia, jiachia, jikata, jisanzua, kipa, kula bunda, lala mbele, tambaa, timka, timua, toa kiwingu, yeya*

piga bushoke n *lala chini katika sakafu* sleep on the floor

Onomastic synecdoche from name of musician, who sang a song about a man who was mistreated by his wife and had to sleep on the floor.

Masela mnapiga bushoke.

Marafiki mnalala chini katika sakafu kwa sababu ya ufinyu wa nafasi za kulala.

piga chabo v.phr *chungulia vitu visivyomhusu mtu, chungulia mtu kwa kumwangelia* peep, spy out "through the keyhole"

< ?

> *kula chabo*

piga chasi v.phr *chungulia vitu visivyomhusu mtu, chungulia dirishani, peleleza mtu, kuwaangalia watu kwa kificho* peep, spy

Semantic extension of SS *kula 'eat'; origin of *chasi unclear.

- Amepiga chasi.*
Amewaangalia watu kwa kificho.
Acha kupiga chasi!
Acha kuangalia watu kwa kificho!
> *kula chasi, piga deo, piga tochi, kula chabo*
- piga chini** v.phr 1. *anguka* 2. *kataa mtu* 1. fall down 2. forbid sb
Metaphorical extension of SS *piga 'hit' and *chini 'down'.
1. *Alipiga chini.*
1. Alianguka.
2. *Alimpiga chini.*
2. Alimkataa.
- piga debe** v.phr *tangaza kwa nguvu* announce energetically
Metaphorical extension of SS *piga 'hit' plus *debe 'tin'.
- piga denda** v.phr *kupa busu mdomoni, nyonya ulimi, kula romansi* French kissing, deep kissing
Metonymic extension of SS *piga 'hit' and *denda 'saliva'.
Mshikaji alimpiga denda demu wake.
Rafiki amempa "deep kiss" mpenzi wake.
> *denda*
- piga deo, piga mdeo, kula mdeo** v.phr 1. *chungulia vitu visivyomhusu mtu* 2. *tazamia kwa mbali* peep, look from far like zooming
Metonymic extension of SS *piga 'beat' plus truncation of SE 'video'.
2. *Hoya, tuache, tule mdeo kwa chati hapa.*
2. Hoya, twende, tuangalie vizuri toka mbali.
> *kula chabo, piga chabo, piga tochi*
- piga desh** v.phr *acha mlo kwa sababu ya bajeti finyu* go without meal for lack of money
Semantic extension of SS *kula 'eat' plus SE 'dash'.
- piga fiksi** v.phr *ongopa, sema uwongo, danganya* tell lies, cheat
Euphemistic metaphorical extension of LyM expression "piga fiksi" 'tidy up, put things in their proper place'
Toka, unatupiga fiksi tu.
Toka, unatudanganya tu.
> *funga (ma)kamba, kamba*
- piga fleva** v.phr *tongoza* flirt with a girl
- Metonymic extension of SS *piga 'hit' and transfer from SE 'flavour'.
- piga jeki** v.phr 1. *kupa mtu msaada* 2. *vaa sidiria* 1. help sb 2. wear a bra
Metaphorical extension of SS *piga 'beat, hit' plus *jeku 'jack'. In 2. dysphemistic extension: like a jack is used for lifting cars, a bra is used for lifting breasts. In KKS 2 with meaning 1.
1. *Nitakupiga jeki.*
1. Nitakusaidia.
2. *Yule kapiga jeki yule.*
2. Yule amevaa sidiria.
- piga kimya** v.phr *nyamaza kabisa kuhusu jambo fulani* be silent
Semantic extension of SS *piga 'hit, beat' plus *kimya 'silence'.
Waliponiuliza kuhusu ishuru ya fedha mimi nilipiga kimya.
Waliponiuliza kuhusu swala la fedha mimi nilinyamaza kabisa.
> *kausha, kauka, kula jiwe, mezea, mikausho*
- piga kipepsi** v.phr *kumpiga mtu kwa kiwiko* hit sb with elbow
Metonymic extension of 'Pepsi Cola', based on form of bottleneck.
Amenipiga kipepsi.
Amenipiga kwa kiwiko.
- piga kirungu** v.phr *omba vibaya, omba pesa* beg from someone, esp. money, cadge for, sponge, ask for money
Hyperbolic semantic extension of SS *piga kirungu 'hit with a club'.
Yule amenipiga kirungu.
Yule ameniomba hela.
Ngoja nimpige kirungu Mzee Hassani.
Ngoja nimwombe pesa Mzee Hassani.
> *bomu, piga mzinga, jamaa wa virungu*
- piga kona** v.phr *fanya mapenzi nje ya ndoa* have extramarital sex
Metaphorical extension of colloquial expression 'hit the corner', meaning 'turn direction'.
Yule baba anapiga kona sana.
- piga maji** v.phr *kunywa pombe, kunywa ulevi* drink alcohol
Metaphorical extension of SS *piga 'beat, hit' plus *maji 'water'. Also attested in older

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

Swahili slang (Ohly 1987a: 67).

Yule anapiga sana maji.

Yule anakunywa sana pombe.

> *maji*

piga mdeo

> *piga deo*

piga mti, piga miti v.phr *fanya mapenzi*

make love, have sex

Metaphorical extension of SS *piga 'hit' plus *mti 'tree' (colloquial for erect penis).

There is no passive *pigwa mti. The phrase cannot be used in family context; preferred among young men for boasting purposes. Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 67).

Alimpiga mti.

Alifanya mapenzi naye.

Hoya, yaani umetoka kupiga miti?

Hoya, yaani unatoka kufanya mapenzi?

> *piga bao, mti*

piga mtu bao v.phr *shinda mtu, fanya*

mapenzi na mwanamke defeat sb, sleep with a woman

Metonymic extension of SS *piga goli 'shoot a goal'.

Shetani amekupiga bao.

Shetani amekushinda.

piga mtu kijembe v.phr *kumtolea mtu*

maneno ya kejeli ambayo yanaweza kuwa ya kweli au siyo mock at sb

Metaphorical extension of SS *piga 'hit' plus *kijembe 'little hoe'.

piga mweleka v.phr *anguka* fall down

Metonymic extension of SS *piga 'hit' plus *mweleka 'wrestle'.

John alipiga mweleka.

John alianguka.

> *lamba mweleka*

piga mzinga v.phr *omba, omba pesa* beg from someone, esp. money, cadge for, sponge, ask for money

Hyperbolic semantic extension of SS *piga mzinga 'fire a cannon'.

Yule amenipiga mzinga.

Yule ameniomba hela.

> *bomu, piga kirungu, jamaa wa virungu*

piga nao v.phr *fanya mapenzi (wanaume)*

make love, have sex (men)

Pronominal form *nao, referring to *uume 'penis' plus SS *piga 'beat, hit'.

Punguza kumpiga nao kila siku.

Punguza kufanya naye mapenzi kila siku.

> *chapa nao, piga bao*

piga ndonga v.phr *cheza ndondi* box

< ?

Yule ni mpiga ndonga.

Yule ni mcheza ndondi.

piga nyeto v.phr *piga punyeto* masturbate (male)

Initial clipping of SS *punyeto 'act of masturbation (male)'

Mshikaji acha kupiga nyeto.

Rafiki, acha kupiga punyeto.

> *piga puri*

piga pafu v.phr *1. vuta sigara 2. kunywa*

pombe kwa vifundo vichache. 1. take a puff

2. take a few gulps of beer

Semantic extension of SS *kula 'eat' and SS *pafu 'lung' or SE 'puff'?

1. Mshikaji, nigege fegi nipige pafu moja, nimekalukwa.

1. Jamaa, naomba sigara nivute kidogo, nimeishiwa.

2. Nilipitia kilabuni nikapiga pafu mbili za kinywaji.

2. Nilipitia kilabuni nikanywa vifundo viwili vya pombe.

piga puri v.phr *piga punyeto* masturbate (male)

Terminal clipping plus suffixing -ri of SS *punyeto 'act of masturbation (male)'

Mshikaji acha kupiga puri.

Rafiki, acha kupiga punyeto.

> *piga nyeto*

piga soo

> *soo*

piga stori v.phr *simulia habari* tell a story, tell stories

Transfer from SE 'story' plus semantic extension of SS *piga 'hit, beat': "hit a story".

Hawakupiga stori nyingi, wakaagana.

Hawakuzungumza sana, wakaagana.

piga tarumbeta v.phr *1. kunywa kutoka*

- kwenye chupa, bila bilauri* 2. *sambaza habari ambazo hazimhusu mtu* 1. drink from the bottle 2. gossip
Metaphorical extension of SS *piga 'hit, play' and *tarumbeta 'trumpet'.
- piga tochi** v.phr *angalia* have a look at, stare at
Hyperbolic metaphoric extension of SS *piga 'hit' plus SE 'torch'.
Mbona unanipiga tochi.
Mbona unaniangalia sana.
> *macho balbu*
- pigana vibuti** v.phr *achana* separate, leave one another
Dysphemistic extension of SS *pigana 'hit one another' plus LyM *vibuti 'little boots'.
Wamepigana vibuti.
Wameachana.
- pigia debe** v.phr *tangazia kitu fulani* make sth known, advertise
Metonymic extension of SS *pigia debe 'hit the tin'
Wanaipigia debe pombe ya Malta Guinness.
Wanaitangazia pombe ya Malta Guinness.
> *pigia debe*
- pigika** v *ishiwa pesa* run out of money
Metaphorical semantic extension of stative derivation of SS *pigia 'beat'.
Nimepigika.
Nimeishiwa pesa.
> *rosti, uawa, mabaga, kalukwa*
- pigilia** v.appl *vaa* wear
Hyperbolic metaphorical extension of SS *pigia 'hit'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 28).
Joy amepigilia nguo safi.
Joy amevaa nguo nzuri.
Yule kapigilia glasi.
Yule amevaa miwani.
> *kula nguo, tinga*
- pigwa bao** v.phr *tapeliwa, danganywa, ibiwa* be cheated, be tricked, be robbed
Semantic extension of SS *pigia 'beat' plus derivation of SS *bao 'goal'.
- pigwa buti** v.phr *achwa* be abandoned
Metaphorical extension of SS *pigwa 'be hit and LyM *buti 'boot'.
Nimepigwa buti.
Nimeachwa.
> *pigana vibuti, tosa*
- pilau** n9/10 *filamu ya X, filamu iliyopiwa marafuku*. X-rated movie
Metaphorical extension of SS *pilau.
Cognitive motivation not clear.
Nilikuwa nimeangalia pilau.
Nilikuwa nimeangalia filamu ya X.
> *bluu*
- pimbi** n5/6 *mtu mfupi* short person
< ? Probably invented by the newspaper "Sani". Also attested for older Swahili slang as *pimbi 'short-statured person' (Ohly 1987a: 68).
Nimeenda bichi nikakutana na pimbi.
Nimeenda bichi nikakutana na mtu mfupi sana.
> *emoro, sista P*
- pina** n/adj *zuri, uzuri* nice, beautiful, beauty
Probably derived from the LyM phrase *chelea pina 'nice, well'.
Demu yuko pina.
Msichana ni mzuri sana.
Umetoka pina.
Umetoka safi.
- pinda** n.phr *kuwa na mambo yasiyo mazuri* be bad, develop in negative way (of affairs)
Metaphorical extension of SS *pinda 'bend'.
Nimepinda.
Mambo yangu siyo mazuri.
- pini** n9/10 *shilingi 100* 100 TSh
Semantic extension based on the augmentative of SS *mpini 'shaft or handle for inserting tool' or SE 'pin'?
Naomba pini.
Naomba shilingi mia.
> *hais, jiti, nyento, nyanga, alasiri*
- pini, mpini** n 1. *mdundo wa muziki* 2. *msichana mzuri* 1. rhythm of music 2. beautiful girl, young woman
Metonymic extension of transfer from SE 'pin', or semantic extension based on the augmentative of SS *mpini 'shaft or handle for inserting tool'?
Pini yangu matata sana.
Msichana wangu mzuri matata sana.

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

> *gashi*

pipa n5/6 1. *ndege ya jeshi* 2. *ndege ya abiria*

1. airforce plane 2. aeroplane for passengers
Dysphemistic metaphorical extension of SS
*pipa 'barrel, tub, cask'.

Leo mchonga kapanda pipa kwenda majuu.

Leo raisi kapanda ndege kwenda ulaya.

*Walami baada ya kupoa hapa Kurio
wataondoka na pipa.*

Wazungu baada ya kukaa hapa Kurio
wataondoka na ndege.

Sasa tomorrow nakwea pipa kwenda majuu.

Sasa kesho napanda ndege kwenda ulaya.

pira n5 *kondomu* condome

Metonymic extension of augmentative of SS
*mpira 'rubber'.

> *buti, soksi, ndomu*

pisto[l] n *nyonga kubwa* large hips

Metaphorical extension of transfer from SE
'pistol', motivated by form of holster
worn on hips in "cowboy-style".

Yule ana pistol.

Yule ana nyonga kubwa.

> *bastola, bunduki, silaha, mvinyo*

poa adv;adj *nzuri* cool, nice, good

Metaphoric extension of SS *poa 'cool
down', calque on SE 'cool'.

Predominantly used in greetings as a
standard reply to *hali vipi. Also attested
in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 28).

Hali vipi? - Poa!

Hali vipi? - Nzuri!

Leo kuna muvi poa sana tukalichekeshie.

Leo kuna video nzuri sana tukaiangalie.

Godi akujalie safari poa.

Mungu akujalie safari nzuri.

> *baridi, joto, byee*

poa v *kaa* stay, rest, pause

Semantico-pragmatic extension of SS *poa
'cool down, calm down'.

*Walami baada ya kupoa hapa Kurio
wataondoka na pipa.*

Wazungu baada ya kukaa hapa Kurio
wataondoka na ndege.

pochi n5 *fedha za noti* paper money

Metonymic extension of SS *pochi 'purse'.

*Ifungue haraka barua yako tulione pochii
alilokutumia.*

Ifungue haraka barua yako tuzione fedha za
noti alizokutumia.

pochoa v *kula sana* eat very much, guzzle

Probably derived from LyM *mapochopocho
'nice food'.

Jana tumepochoa sana.

Jana tumekula sana.

> *jichana*

poda n9/10 *madawa ya kulevya* drugs

Metonymic extension of transfer from SE
'powder'.

Vijana wanakula poda sana.

Vijana wanatumia sana madawa ya kulevya.

pointi tano n.phr *chotara* half cast

Transfer from English 'point five', meaning
1/2. In Sheng *pointi-faiv is attested with
the same meaning (Mbaabu & Nzuga
2003: 21).

pointi tupu n.phr *wazi* to the point

Semantic extension of transfer from SE
'point' and SS *tupu 'unmixed, mere'.

Leo umeongea pointi tupu.

Leo umeongea wazi.

poteza v.caus 1. *kutoelewa* 2. *kufa, fariki* 1.

misunderstand 2. die

Metaphorical extension of SS *poteza 'lose'.

In 2.: Ellipsis of "poteza maisha" 'lose
one's life'.

1. *Hoya unapoteza bwana.*

1. Huelewi, bwana.

2. *Washikaji kujidunga ni noma mnapoteza
bure.*

2. Marafiki, kujichoma sindano za madawa
ya kulevya ni vibaya, mtafariki.

poteza kitumbua v.phr *poteza kazi* lose a job

Metaphorical of SS *poteza 'lose' and
*kitumbua 'rice cake'; expression 'lose
the rice cake'.

*Nilifanya uzembe nikapoteza kitumbua
changu.*

Nilifanya uzembe nikapoteza kazi yangu.

*Msiba wa mama ulisababisha nipoteze
kitumbua changu.*

Msiba wa mama ulisababisha nipoteze kazi
yangu.

poyoyo n5/6 *mwanamume bila nguvu, mjinga,*

bwege henpecked husband, fool

- < ?
Rafiki yangu usiwe poyoyo.
Rafiki yangu usiwe mjinga.
Mapoyoyo ndio waliwao.
Wajinga ndio waliwao.
 > *boka, mbwiga, mnyela, ndula*
- poza** v.caus *kupa hela kidogo* help sb with money
 Metaphorical extension from SS *poza 'cool', based on the image of cooling the hot state caused by any kind of irritation.
Nipoze bwana.
 Nipe hela kidogo.
- promota** n5/6 1. *promota redioni* 2. *mtu ambaye anapiga na kukata simu ya mkononi*
 1. promoter at the radio 2. someone who beeps with mobile phone
 2. Semantic extension of SE 'promoter', based on the song of Mr. II "promota anabeep".
 2. *Kwa nini umekuwa promota?*
 2. *Kwa nini ulipiga simu ukakata?*
 2. *Anayekubipi ndiye promota.*
 2. *Anayekupigia simu, halafu anakata kabla hujajibu, ndiye promota.*
 2. *Ah, promota huyu.*
 2. *Ah, huyu ni mtu ambaye anataka nimpigie simu.*
- propoza** n5/6 *biashara marufuku* illegal traffic
 Semantic extension of SE 'propose'? Attested in older Swahili slang for the meaning 'contraband, bribe' (Ohly 1987a: 69).
Ukipata propoza ya kuuza viatu vipya toka bandarini sawa.
 It is okay if you get illegal traffic to sell shoes from the port.
- punga** n5 *wali* cooked rice
 Hyperbolic extension of SS *mpunga 'unhusked rice'. In older Swahili slang attested with the meaning 'gruel' (Ohly 1987a: 69).
Tufinye punga.
 Tule wali.
 > *mavi ya panya, nyali, punje, ubeche, ubwabwa*
- punguwani** n9/10/6 *taahira* fool
 Semantic extension of SS *pungua 'be reduced'.
Yule ni punguani.
- Yule ni taahira.*
 > *mtambo, some-time-yes-some-time-no*
- punje** n9 *wali* cooked rice
 Metonymic extension of SS *punje 'grain'. In older Swahili slang attested with the meaning 'gruel' (Ohly 1987: 69).
Wacha tufinye punje.
 Wacha tule wali.
 > *mavi ya panya, nyali, punja, ubeche, ubwabwa*
- pupwe** n5 *kiyoyazi* air-conditioner
 Hyperbolic extension based on augmentative of SS *kipupwe 'cold season, cold weather'.
- pusha** n5/6 *mwuza bangi* marijuana dealer
 Transfer from SE 'pusher'.
- puyanga** v *enda visivyo* be unsteady, erratic
 < ?
Hoya mtu wangu acha kupuyanga kama kuku.
 Hoya rafiki yangu acha kwenda ovyo.
- pwaga** v *toa uongo, danganya* lie, cheat
 Metaphoric extension of SS *pwaga 'grind, pound'; attested in older Swahili slang for the meaning 'go away' (Ohly 1987a: 69).
Usinipwage!
 Usinidanganye!
- pótabo** n *mwanamke mwenye umbo dogo zuri* woman with small figure
 Metaphorical extension of transfer from SE 'portable'.
Siku hizi Asha ni portabo.
 Siku hizi Asha ana umbo dogo zuri.
- raba mtoni** n.phr *viatu kutoka nje ya Tanzania* imported shoes, trainers
 Metonymic extension of SS *raba 'trainers' and *mtoni 'Europe, Western country'.
Ana raba mtoni.
 Ana viatu kutoka nje.
 > *simpo*
- rapu** v *gomba* quarrel
 Metonymic extension of transfer from English 'rap'.
Mama karapu leo.
 Mama amegomba sana leo.
- rap[u]** v *zungumza sana* speak a lot, speak

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- non-stop
Metaphorical extension of English 'rap'.
Mwanasiasa anarap huyo.
Mwanasiasa anaongea sana huyo.
- rasta[fari]** n *mtindo wa kusuka nywele aina ya rasta* rasta hairstyle
Transfer (plus truncation) of SE 'rastafari'.
Rastafari Awilo.
Rasta ya mtindo wa Awilo.
- redio mbao** n.phr *mtu ambaye anazungumza sana, msema ovyo, hawezi kuficha siri* person who talks a lot and who can't keep a secret
Onomastic synecdoche of SS *redio mbao
"Radio wood", a small but durable and affordable radio for the rural population with a wooden corpus, in the 1970s.
Jamaa yule, usimwambie siri, yule ni redio mbao.
That guy, don't tell him secrets, he can't keep them.
> *redio saba saba, BBC*
- redio saba saba** n.phr *mtu ambaye anazungumza sana, msema ovyo, hawezi kuficha siri* someone who talks a lot and can't keep a secret
Onomastic synecdoche of SS *redio saba saba, a small but durable and affordable radio for the rural population, in the 1970s, also called "redio mbao", because of its wooden corpus. "Saba saba", July 7th, is a public holiday "Peasant's Day".
Jamaa yule, usimwambie siri, yule ni redio saba saba.
That guy, don't tell him secrets, he can't keep them.
> *redio mbao, BBC*
- roho ya chuma** n.phr
roho ngumu hard-heartedness
Metaphorical extension of SS *roho 'soul' plus SS *chuma 'iron'.
Maggy kidogo alikuwa na roho ya chuma.
Maggy kidogo alikuwa na roho ngumu.
> *roho ya korosho, roho ya kwa nini*
- roho ya korosho** n.phr *roho mbaya, tabia ya kutopenda kutoa cho chote* tight-fisted behaviour, hard-hearted behaviour
Metaphorical extension of SS *korosho

- 'cashew nut', based on the similarity in form between a cashew nut and a question mark. A tight-fisted person is conceived as one who asks "why should I give you?"
Yule ana roho ya korosho.
Yule hataki kutoa cho chote.
> *roho ya kwa nini*
- roho ya kwa nini** n.phr *roho mbaya, tabia ya kutopenda kutoa cho chote* tight-fisted behaviour, hard-hearted behaviour
Metonymic extension of SS *roho 'soul' plus *kwa nini 'why', denoting the habit of stingy persons to ask: "Why should I give you something?"
Yule ana roho ya kwa nini.
Yule hataki kutoa cho chote.
> *roho ya korosho*
- rosti** v *ishywa hela* be broke, have no money
Metaphoric extension of SE 'rust', or "roasted" or even "lost".
Nimerosti.
Nimeishiwa hela.
> *arosto, pigika, uawa, kalukwa, mabaga*
- rosto**
> *arosto*
- ruka majoka** v.phr *cheza muziki (ya aina yo yote)* dance to music (no matter which kind of music)
Hyperbolic extension of SS *ruka 'fly, jump' plus augmentative *joka 'very big snake'. Probably motivated by the body-movements in dancing.
Tumeruka majoka.
Tumecheza muziki.
Niliuendea ukumbi wa kuruka majoka.
Niliuendea ukumbi wa kucheza dansi.
- rungu** n *gongo* kind of hard liquor
Metaphorical hyperbolic extension of SS *rungu 'club', alluding to its quick and powerful effects, in analogy to derivation of SS *gongo from *gonga 'hit, knock'.
- rusha roho** v.phr 1. *jidai, ringa* 2. *taarabu ya kisasa yenye midundo ya kasi na lugha wazi isiyoyana mafumbo* 3. *tembea na mume mtu, hasa wa rafiki* 1. boast 2. modern taarabu with faster beats and open language 3. hook sb's husband

- Metaphorical extension of SS *rusha 'throw' and SS *roho 'soul'.
- safiri** v *imba kwa mtiririko* sing
Metaphorical extension of SS *safiri 'travel'.
Nimesafiri humo kwenye hilo traki.
Nimeimba kwa mtiririko kwenye huo wimbo.
- sambaza nyuki** v.phr *piga risasi* shoot
Metaphorical euphemistic extension of SS *sambaza 'spread' plus *nyuki 'bees'.
- sanamu la michelini** n.phr *mtu, hasa mwanamke mwenye umbo la sanamu ya michelini, yaani mtu ambaye hana kiuno, hana shepu nzuri* person (woman) without taille
Metaphoric extension of SS *sanamu 'figure, statue' plus trade mark "Michelin", referring to the fat figure representing the trade mark.
- sanzuka** v *ondoka* go away
< ?
Ikifika saa saba tutasanzuka.
Ikifika saa saba tutaondoka.
Nikasanzuka zangu.
Nikaondoka zangu.
>
- sarandia** v *fuatilia jambo kwa bidii mpaka kulipata* follow up an issue seriously
Metonymic extension of transfer from SE 'surround'.
Nilimsarandia demu mpaka akakubali.
Nilimfuatilia demu mpaka akakubali.
Alimsarandia mtalii mpaka akafanikiwa kupata dili.
Alimfuatilia mtalii mpaka akafanikiwa kumpeleka mahali.
- sasambua** v *vua nguo au onyesha sehemu ya mwili mbele ya watu* strip off clothes
Onomastic synecdoche of name of one part of the wedding celebrations, where only women are admitted (kitchen party): A woman stands on a table showing the gifts for the bride, including clothes. She puts some of the clothes on. Therefore some "striptease" is involved. Also song of Mr. Nice on his album "Bahati". A dance style is also called "sasambua".
Nguo zinasasambuliwa.
- Nguo zinavuliwa.*
Sasambua ya kicheni pati ya jana ilikuwa ya nguvu.
Kuonyesha zawadi katika kicheni pati ya jana kulikuwa safi sana.
- saula** v *vua nguo* undress
< ? Also in Kihore (2004: 9).
Jane alimsaulia nguo Juma, kisha wakafanya mapenzi.
Jane alimvulia nguo Juma, kisha wakafanya mapenzi.
- sauz / saus** n *Afrika kusini* South Africa
Elliptic use derived from SE 'South Africa'.
Nataka kuzamia sauzi nikatafute maisha.
Nataka niende Afrika Kusini bila kibali, nikatafute maisha.
> *bondeni*
- sembe** n5 *ugali wa mahindi yaliyokobolewa* porridge made of maize flour from husked maize
Metonymic extension of SS *sembe 'maize flour'. Also attested in older Swahili slang with meaning 'stiff porridge' (Ohly 1987a: 72).
> *bondo, dona, dongo, nguna*
- serikali ya mseto** n.phr *tabia za malaya* promiscuous behaviour
Metaphoric extension of SS *serikali ya mseto 'coalition government'. Cognitive motivation: in a coalition there are many parties, not only one. Degera explains: "hii hapa ina maana kwamba msichana ambaye hufanya mapenzi na kila mtu kwa fedha (malaya) leo huyu kesho yule, ni serikali ya mseto au mpito".
- sero, selo** n *jela, gereza* prison, jail
Transfer from SE 'cell'?
Walimpeleka selo juzi.
Walimpeleka jela juzi.
> *lupango, neti, shimoni*
- sevu** v 1. *hifadhi kitu, saidia mtu* 2. *ondoka, kimbia, toroka* 1. save sth or sb 2. run away
Transfer from SE 'save'.
1. *Nilimsevu.*
1. *Nilimsaidia.*
2. *Sevu hapo sasa.*
2. *Toka hapo sasa.*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

2. *Unacheki, bloo, basi, nikabutuka nikawasevu.*
2. *Unaona, rafiki, basi, nikash[i]tuka nikawatoroka.*
2. *Mnacheki, washikaji, wakati nasevu mapaparazi wakanifotoa picha.*
2. *Mnaona, marafiki, wakati nilipotoroka, waandishi wa habari wakanipiga picha.*
- shaa shaa** adv/id? *upesi upesi!* quick quick!
Abbreviation of SS *chapu chapu 'quick quick'?
- shangingi** n5/6 1. *gari kubwa na ya kifahari*
2. *mwanamke mwenye mwili mnene sana na ambaye matendo yake si mazuri; mwanamke anayependa starehe na ana umbo mkubwa* 1. big luxurious car 2. very fat woman who likes to enjoy the good things in life
> ? New entry in KKS 2.
Hoya, kamata shangingi hilo.
Hoya, kamata mama yule mwenye mwili mkubwa.
> *gubeli, jimama*
- shankupe** n *mwanamke mwenye umri mkubwa anayejipodoa kwa kuwatamanisha wanaume* old woman who uses cosmetics to attract younger men
< ?
Yule ni shankupe.
Yule anajifanya anapenda kufanya mapenzi na watu wa chini ya umri wake.
> *jambazi, shugamemmi*
- shavu** n5 1. *sehemu ya uke ya mwanamke* 2. *simu* 1. female genitals 2. telephone
1. Euphemistic extension of SS *shavu 'cheek' 2. Metonymic extension of *shavu 'cheek', based on the fact, that the telephone is held to the cheek.
1. *Shavu lake ni kubwa.*
1. *Sehemu yake ya uke ni kubwa.*
2. *Ukifika nipe shavu.*
2. *Ukifika nipigie simu.*
- shazi** n5 *wingi* plentiness
< ?
Wamekula shazi la haja.
Wamepata faida kwa wingi.
> *lumbesa, nyomi*
- shega** adj *zuri, sawa, safi, salama* fine, okay
< ? There is also the variant *shegaz.
- Vile vitu safi vyote? - Viko shega tu.*
Vile vitu viko safi vyote? - Viko vizuri tu.
Yule msichana shega kweli yule.
Yule msichana ni mzuri kweli yule.
- shem** n9 *shemeji* bother or sister in law
Terminal clipping of SS *shemeji 'brother / sister in law'. Also attested in Kihore 2004: 117. Common.
Karibu shem! Mambo?
Karibu shemeji! Mambo?
- shepu** n9 *umbo mzuri, hasa ya mwili wa binadamu* good shape, especially of human body
Transfer from SE 'shape'.
Yule hana shepu nzuri.
Yule hana umbo mzuri.
- sheshe** n5 *matatizo* trouble, something problematic, shit
Augmentative derivation of SS *kasheshe 'trouble'.
> *kasheshe, kimeo, kizaazaa, noma, sheshe, soo, zali*
- shi** n5/6 *msichana mzuri* beautiful girl, young woman
Transfer from SE 'she'. Since about 2003.
Yule ni shi wangu.
Yule ni mpenzi wangu.
- shika pembe** v.phr *ishia kuona tu bila kula chakula chenyewe, angalia kitu bila uwezo wa kukipata* see nice food without being allowed to eat, see sth without being able to obtain it
Metaphorical extension of SS *shika 'hold' plus SS *pembe 'horn', based on the image of someone who wants to milk, but holds the horns of the animal, instead of the udder.
Umeshika pembe.
Umekosa kitu.
- shikia bango** v.phr *simamia jambo kwa nguvu hadi kufanikiwa* stand for an issue until success
Metaphorical extension of *shika 'hold' plus *bango 'transparent, poster', expression: "hold up a big poster for something" (like in a demonstration).
Nilimshikia bango mpaka akafukuzwa kazi.
Nilisimamia lile swala lake mpaka

akafukuzwa kazi.

shikishwa ukuta v.phr *firwa, fanywa*
mapenzi kinyume cha maumbile act as a
 homosexual man who receives penetration
 Metonymic extension of SS *shikishwa 'be
 caused to hold' and *ukuta 'wall'.
Yule anashikishwa ukuta.
 Yule anafirwa.
 > *choko, mjengo*

shimoni n.loc *jela, gerezani* in prison
 Dysphemistic metaphorical extension of SS
 *shimo 'pit'.
Wamewekwa shimoni.
 The were arrested.
 > *sero / selo, shimoni, lupango, neti*

shingo feni n.phr *tazama kwa kugeukageuka*
 look at by twisting one's neck, spin around to
 look at
 Dysphemistic metaphorical extension of SS
 *shingo 'neck' and SS *feni 'fan', based
 on the movement of the fan from one
 side to another, not on the movement of
 the propeller. Used especially in elliptical
 saying "macho balbu, shingo feni".
 Popularised through a song by Vijana
 Orchestra "Penzi haligawanyiki". The
 chorus has "Vipi sasa we bwana waleta
 matata / Kwa vile napendeza na
 nimetakata / Kila nikipita macho
 yakutoka / Utadhani balbu, bwana we
 bwana e / Kila nikipita wageuza shingo /
 Utadhani feni, bwana e bwana e"
Yule mtu, macho balbu, shingo feni.
 Yule mtu anatazama sana kwa
 kugeukageuka.

shiti v *tojali, acha* do not care at all
 Dysphemistic extension of transfer from SE
 *shit.
Kazi ya ubaharia nikaipata halafu nikaishiti.
Kazi ya ubaharia nikaipata halafu nikaiacha.
Yule nimemshiti.
 Yule nimeachana naye.

shoo n9/10 *onyesho, tamasha* show
 Transfer of SE 'show'.
Shoo ilifanyika katika ukumbi wa FM club.
 Tamasha ilifanyika katika ukumbi wa FM
 club.

shobo n9/10 *tatizo* problem

< ?

Hii haina shobo.
 Hii haina tatizo.
Hamna shobo.
 Hamna matatizo.
Gari likatuletea shobo kwa hiyo
tukateremka.
 Gari likatuletea matatizo, kwa hiyo
 tukateremka.
 > *jumba bovu, kinaa*

shobo za kisista duu n.phr *tabia za kike*
 homosexual behaviour
 Expression composed of LyM *shobo
 'problem' plus *sista duu 'girl, woman'.
Nas'kia ana shobo za kisista duu kama demu.
 Nasikia ana tabia za kike kama msichana.

shobokeya v *jipendekeza, jisogeza kwa mtu*
kwa kusumbua chum up, smarm over sb,
 endear os to sb, smooth-talk sb, stalk
 Derivation of LyM *shobo 'trouble'.
Yule ananishobokeya.
 Yule anajisogeza kwangu kwa nguvu.

sholi, shori n *msichana mzuri, mpenzi*
 beautiful girl, girlfriend
 < ?
Juma alikuwa akimchombeza sholi wake.
 Juma alikuwa akimbembeleza mpenzi wake.

shost, shosti n5/6 *shoga, rafiki wa kike wa*
mwanamke, na hata rafiki wa kiume wa
mwanamke, kama hakuna uhusiano wa
kimapenzi female friend of a woman, and
 even male friend if there is no sexual
 relationship
 Distortion of SS *shoga 'female friend?'
Aisei, shosti leo umepigilia pamba, umetoka
bomba.
 Aisei, rafiki, leo umevaa nguo nzuri,
 umetoka mzuri kabisa.
Njoo shosti, tubonge.
 Njoo shoga, tuongee.

shugamemmi, shugamama n5/6
mwanamke mwenye umri mkubwa ambaye
anatembea na watoto wadogo elder woman
 who has young boyfriends
 Transfer from SE 'sugarmummy'.

shuka mnazi v.phr *piga punyeto* masturbate
 Euphemistic metaphoric extension of SS
 *shuka 'descend' and *mnazi 'coconut'

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

- tree'.
- shusha** v.caus *leta dharau* despise
Metaphorical extension of SS *shusha 'bring down'.
Wakaona eti tunawashusha.
Wakaona kwamba tunawaleta dharau.
- shusha mistari** v.phr *imba nyimbo za "rap"*
rap verses
Metaphorical extension of SS *shusha 'drop' plus *mistari 'lines'.
Ameshusha mistari.
Ameimba mistari ya wimbo.
> *achia mistari, chana mistari, dondosha mistari*
- shuta shuta** adv *upeski, haraka, chapu chapu!*
quickly, fast, quick quick!
Metaphorical extension based on transfer from SE 'shooter'?
Nenda shuta shuta.
Nenda haraka.
> *fasta fasta, shaa shaa*
- shuzi** n *tako kubwa* big behind
Dysphemistic metonymic extension of SS *shuzi 'fart'.
Yule ana shuzi.
Yule ana mataka makubwa.
> *bambataa, haja kubwa, kibinda, mkundu, ndómbolo, taarabu, tukunyema, wowowo*
- shwaini** n5/6 *mtu mwenye tabia mbaya; nguruwe* pig, person with bad manners
Transfer from German *Schwein 'pig'.
Shwaini we!
Nguruwe wewe!
- sidii, CD** n5/6 *msichana, mwanamke mwenye tabia mbaya ya kihuni* girl, young woman, who has many boyfriends
Abbreviation of LyM *changudoa.
Hoya, msela, huyo ni cd.
Hoya, rafiki, yule ni malaya.
> *changudoa*
- silaha** n9/10 *nyonga kubwa* large hips
Metaphorical extension of SS *silaha 'gun', motivated by form of holster worn on hips in "cowboy-style"
Yule anamiliki silaha.
Yule ana nyonga kubwa.
> *bastola, bunduki, pisto[l], mvinyo*
- simama dede** v.phr *shangaa* be surprised
Metaphoric extension of SS *simama dede 'stand uncertainly like a child just beginning to walk'.
Ukimwona utasimama dede.
Ukimwona utashangaa.
- simamia** v.appl 1. *bana, fuatilia* 2. *uza* 1. force, follow up 2. sell
Semantic extension of SS *simamia 'direct, manage, superintend, supervise'?
1. *Mwalimu alinisimamia mpaka nikasema.*
1. Mwalimu alinibana mpaka nikasema.
2. *Juma kasimamia viatu.*
2. Juma kauza viatu.
> *songola*
- simpo** n *viatu kutoka nje ya Tanzania, raba mtoni* imported shoes, trainers
Transfer from SE 'simple'. Recent.
Hoya, Babu, John amekula simpo kali!
Hoya, rafiki, John amevaa viatu vizuri sana.
> *raba mtoni*
- sing'lendi** n *T-shati au fulana bila mikono* sleeveless top
Transfer from SE 'single hand'
Umevaa kising'lendi.
Umevaa fulana bila mikono.
> *kaoshi*
- sirikali** n9 *serikali* government
Charade strategy in deformation of SS *serikali, imposing a fake etymology 'hot secret' based on SS *siri 'secret' and *kali 'hot, sharp'.
Sirikali nyingi za Afrika hazizingatii haki za binadamu.
Serikali nyingi za Afrika hazizingatii haki za binadamu.
- sista du, sista duu** n.phr, 5/6 *msichana mzuri* girl, beautiful girl, towngirl, modern girl
Metonymic extension of SE 'sister' and LyM interjection *du.
Masista du wa Bongo wanazidi kupanda chati. (Prof. Jay in song "Bongo Dar es Salaam", 2002)
Wasichana wa Dar es Salaam wanazidi kuwa watanashati.
- sista P** n.phr *chupa ndogo ya Coca Cola* 200 ml bottle of Coca-Cola
Onomastic synecdoche based on the name of the *Bongo Fleva* star Sista P. who is

- quite a short person.
> *emoro*
- sizi** v 1. *kaa kimya bila kuongea kitu cho chote, kama mtu amelala usingizi* 2. *lewa* 1. be quiet without saying anything, as if being asleep 2. be drunk
Transfer from SE 'cease'.
1. *Jamani, amesizi.*
1. Jamani, anasinzia.
2. *John Degera leo amesizi sana.*
2. John Degera leo amelewa sana.
- skani** n *kijiweni* meeting place of (jobless) youths
Initial clipping of SS *maskani 'home, settlement'.
Deile mi' natimba skani.
Kila siku mimi naingia kijiweni.
- skendo** n5/6 *tafrani* scandal
Transfer from SE 'scandal'.
Skendo la Miss Tanzania.
Tafrani ya Miss Tanzania.
- skonga** n5/6 *shule, chuo* school
< ?
Naenda skonga.
Naenda shuleni.
- sleng** n9 *Kiingereza* English
Transfer from SE 'slang'.
Sleng yake kali.
Kiingereza chake kizuri.
- sleng** v *sema Kiingereza* speak English
Transfer from SE 'slang'.
Yule anasleng.
Yule anasema Kiingereza.
- smati** adj *safi, zuri* nice, smart
Transfer from SE 'smart'.
Vaileti alitokea smati mwenye kuvutia.
Vaileti alitokea safi mwenye kuvutia.
- soo** n5/6 1. *matatizo* 2. *aibu* 1. trouble, something problematic 2. shame
Truncation of LyM *songombingo, or of SS *soni 'shame, shyness'? Attested for the meaning 'money; 100 Tsh' in older Swahili slang (Ohly 1987a: 73).
1. *Soo bloo, wacha noma!*
1. Ni matatizo kaka, usilete balaa!
1. *Jamani, mtaa fulani leo kuna soo.*
1. *Jamani, mtaa fulani leo kuna matatizo.*
2. *Vipi mbona hamnigei stori, kuna soo au noma, washikaji?*
2. *Vipi mbona hamnipi habari, kuna aibu au matatizo, marafiki?*
2. *Usione soo.*
2. *Usione aibu.*
1. *Acha kupiga soo!*
1. *Usilete balaa!*
> *msala, kimeo, kizaazaa, noma, kasheshe, songombingo*
- soba, somba** v *chukua, tia gerezani* take, put in prison
Metonymic extension of SS *somba 'carry'?
Ipo dei fulani mamwela walinijia kutaka niwagee ganja ili wanisobe rupango.
Ipo siku fulani polisi walinijia kutaka niwape bangi ili wanichukue gerezani.
- soda** n9 *rushwa* bribe
Euphemistic metonymic extension of SS *soda 'soft drink'. Like with *chai, the bribe is conceptualised as the necessary preliminary which sets things in motion.
Anataka soda!
Anataka rushwa!
> *chai, kitu kidogo*
- soksi** n9/10 *kondomu* condom
Metaphoric extension of SE 'socks'.
Popularised in a song by Remmy Ongala "Mambo kwa soksi". Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 31).
Nisaidie soksi.
Nisaidie kondomu.
> *buti, ndomu*
- somesha** v. *caus eleza, tumia mbinu*
kumlainisha mtu ili akubaliane na matakwa
explain, tell, use tactics to bring sb to agree with one's wishes
Euphemistic metonymic extension of SS *somesha 'educate, instruct, teach'.
Poa nitamsomesha mshua kuhusu nini imetokea skonga.
Nitamweleza baba kuhusu nini imetokea shuleni.
- songombingo** n *fujo, kitu kisicho na mpangilio, kitu ambacho hakipo kwenye mstari mnyoofu* chaos, disorder, zig-zag-line
Compound of SS *songo 'braid, coil, loop'

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

(or *songa 'press, squeeze'); etymology of *mbingo (< *binga?) unclear.

Amenisuka songombingo.

Amenisuka nywele kwa mistari isiyonyooka.

Mambo yanakwenda songombingo.

Mambo yanakwenda ovyo.

Jana ilibidi nisafiri lakini mambo yakawa songombingo, sikuwahi.

Jana ilibidi nisafiri, lakini mambo hayakukaa sawa, sikuwahi.

> *bebebebebe*

sopsop[u] n -*enye sura nzuri* good-looking
Semantic extension of SE 'soap'.

Yule jamaa yuko sopsopu.

Yule jamaa ana sura nzuri.

spesheli adj -*a namna ya pekee* special

Transfer from SE 'special'. Also attested in older Swahili slang (Ohly 1987a: 73).

Hii ni spesheli.

Hii ni ya namna ya pekee.

spidi mia ishirini (nshaa) n.phr *kasi sana*

bila ya kutulia, haraka haraka very fast

Metaphorical extension of elliptical transfer of SE 'speed of 120 km/h'. Has taken the place of "spidi tisini" in older LyM.

Leo naendesha kipindi hiki kwa spidi 120.

Leo naendesha kipindi hiki bila ya kutulia.

staili n9/10 *mtindo* style

Transfer from SE 'style'.

> *dizaini*

stimu n9 *hisia kutokana na kuvuta bangi au madawa ya kulevya, hisia nzuri, shauku* state of being high (form drugs), good mood
Metaphorical extension of transfer from SE 'steam'.

Kula kitu kikupe stimu.

Vuta bangi ikupe hisia nzuri fulani.

Hoya, usinipotezee stimu yangu.

Hoya, usinitolee hisia zangu, niko fresh.

> *mishangashanga*

stori n9/10 *habari, masimulizi* news, tale
Metonymic extension of SE 'story'. Also attested in Sheng (Mbaabu & Nzuga 2003: 32).

Vipi mbona hamnigei stori, kuna soo au noma, washikaji?

Vipi mbona hamnipi habari, kuna matatizo au aibu, marafiki?

Vijana wa vijiwani wanapiga stori.

Vijana wa vijiwani wanapashana habari.

suka n5/6 *dereva* driver

Metonymic extension of truncation of SS *usukani 'steering wheel'.

Suka anaendesha gari taratibu.

Dereva anaendesha gari taratibu.

sumu n9 1. *uji usiyo na sukari, hasa katika shule za bwani* 2. *maneno mabaya ya uchonganishi(fitina)* 1. light porridge without sugar, esp. in boarding schools 2. bad gossip

1. Dysphemistic extension of SS *sumu 'poison'.

2. Metaphorical extension of SS *sumu 'poison'.

1. Hoya, si umu ya leo ni mukide.

1. Hoya, uji wa leo ni afadhali kuliko siku nyingine.

2. *Anatema sumu.*

2. Anatoa maneno ya fitina.

2. *Ana sumu kali huyo.*

2. Ana maneno mabaya sana ya fitina.

sunda v 1. *kula vizuri sana, kufaidi kwa chakula* 2. *ficha mbali, k.m. katika sehemu za siri* 1. eat very good food, enjoy food 2. hide sth very well, e.g. in private parts < ?

1. Njoo tusunde!

1. Njoo, tule vizuri!

2. *Waliiba mishiko wakaisunda matakoni.*

2. Waliiba pesa wakazificha matakoni.

> *jichana, chikichia*

supa, super adv *zuri sana* super, very good, extraordinary

Transfer of SE 'super'. Restricted to response in greetings.

Mambo supa.

Mambo safi.

> *mambo mtibwa, mambo ya isidingo*

supastaa n5/6 *msanii au mwimbaji mashuhuri* superstar

Transfer of SE 'superstar'.

Unajua mustakabali wa masupastaa wa Bongo? (Prof. Jay in "Bongo Dar es Salaam", 2002)

Unajua mustakabali wa wasanii mashuhuri wa Dar es Salaam?

supu ya mawe, supu la mawe n.phr *pombe kali haramu, gongo* illegally distilled hard liquor

Metaphorical dysphemistic extension of SS *supu 'soup' and *mawe 'stones'; expression "stone soup".

Anapenda kutumia supu ya mawe.

Anapenda kunywa gongo.

> *machozi ya simba, maji makali, nipa*

suru n5/6 *suruali* trousers

Final truncation of SS *suruali.

Mshirika, ipo dei tutawamba masuru ya jeans.

Rafiki, ipo siku tutavaa suruali za jinsi.

> *gamba*

susia v.appl *kupa, patia, toa* give

Metonymic extension of SS *susa 'abandon'.

Oya, nisusie mapene yangu.

Oya, nipe pesa zangu.

> *gea*

sweka v 1. *ficha* 2. *weka ndani, weka*

gerezani 1. hide 2. put (inside), put in jail < ?

1. *Amesweka pesa zake.*

1. Ameficha pesa zake.

2. *Wameswekwa rupango.*

2. Wamewekwa ndani.

2. *Amemsweka rumande.*

2. Amemweka rumande.

taahira n9/10 *mtu aliyepumbaa akili* mad person, lunatic

Metonymic extension of SS *taahira 'postponement, delay'?. In KKS 2.

taifisha v.caus *iba, chukua kitu kwa mtu au*

watu, dai kuwa mwenyewe steal, take sth away from so, claim to be owner of sth

Metonymic and euphemistic semantic extension of SS *taifisha 'nationalise'

Ameitaifisha.

He took it as his.

taiti v *bana* force, press, fit tightly

Transfer from SE 'tight'.

Majita wamenitaiti.

Wahuni wamenibana.

Alivaa fulana nyeusi iliyomtaiti.

Alivaa fulani nyeusi iliyombana.

taiti adj *safi* nice

Transfer of SE 'tight', or 'tidy'?

Juma alikuwa taiti jana.

Juma alikuwa safi jana.

> *smati*

taiti n9/10 *sketi fupi inayobana matak*o tightly fitting miniskirt

Transfer from SE 'tight'.

Yule amevaa taiti.

Yule amevaa sketi fupi ya kubana matak

tambaa v *ondoka* go, go away

Metonymic extension of SS *tambaa 'crawl'.

Tuliona wanatuyeyusha tukawaambia watambae.

Tuliona wanatudanganya tukawaambia waondoke.

> *anza, chomoa, ishia, jikata, jisanzua, kipa, timka, timua, toa kiwingu*

tantarila n9/10 *maneno mengi yasiyo na busara* a lot of words without meaning

Probably semantic extension of name of Reggae song "tantarilla" by Don One

Crew on Album "Watch the ride" (1998).

Acha tantarila zako we kinabo.

Acha maneno yako yasiyo na busara, we mshamba.

tapeli n5/6 *mtu anayelaghai watu ili*

awadhulumu mali au haki zao swindler

Transfer from French *tapeur 'cadger'

(Graebner 1995: 266). Popularised through song by Vijana Jazz Band

"Ogopa matapeli", in the late 1980s.

> *msanii*

tapeli v *laghai, iba kwa kulaghai* swindle, steal by swindling

Transfer from French *tapeur 'cadger'

(Graebner 1995: 266).

Alitaka kunitapeli.

Alitaka kunilaghai.

Ametapeliwa.

Ameibiwa na tapeli.

taraa numeral *tatu* three

< ?. Obsolete.

Nipe sigara taraa.

Nipe sigara tatu.

Nipe chumvi ya chuma taraa.

Nipe chumvi ya shilingi tatu.

> *bee, dala*

LUGHA YA MITAANI IN TANZANIA

taarabu n9/10 *matako makubwa ya mwanamke* woman's behind, big buttocks, fat bottom

Metonymic extension of SS *taarabu?, based on dance movements.

Manzi huyu ana taarabu.

Msichana mdogo huyu ana matako makubwa.

Taarabu imo humo.

Matako yapo.

> *bambataa, haja kubwa, mkundu, ndómbolo, shuzi, tukunyema, wowowo*

tarakishi n5/6 *kompyuta* computer

< ?

techele disc *poa, safi* good

< ? Used as a standard reply to greetings such as *hali vipi.

tega v *tamanisha* seduce

Metaphorical extension of SS *tega 'trap'.

Acha kunitega wewe demu.

Acha kunitamanisha kwa ngono, wewe msichana.

tega antena v.phr *sikiliza kwa makini* listen attentively

